

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Sita – Tarehe 9 Novemba, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tano na kikao cha leo ni Kikao cha Sita.

Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: -**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1.      Toleo Na. 36 la tarehe 03 Septemba, 2021;
2.      Toleo Na. 37 la tarehe 10 Septemba, 2021;
3.      Toleo Na. 38 la tarehe 17 Septemba, 2021;
4.      Toleo Na. 39 la tarehe 24 Septemba, 2021;

5. Toleo Na. 40 la tarehe 01 Oktoba, 2021;
6. Toleo Na. 41 la tarehe 08 Oktoba, 2021;
7. Toleo Na. 42 la tarehe 15 Oktoba, 2021;
8. Toleo Na. 43 la tarehe 22 Oktoba, 2021; na
9. Toleo Na. 44 la tarehe 29 Oktoba, 2021.

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Katibu!

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini.

Na. 59

**Zahanati ya Ihalula kuwa Kituo cha Afya – Njombe Mjini**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-**

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Zahanati ya Ihalula kuwa Kituo cha Afya baada ya kukidhi vigezo vyote kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Dkt. Dugange tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliipandisha hadhi zahanati ya Ihalula kuwa Kituo cha Afya mwaka 2018/2019 na kupewa namba ya utambulisho 101604-7. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilipeleka Shilingi Milioni 500 kwa ajili ya ukarabati wa majengo mengine likiwemo jengo la upasuaji ambalo sasa linatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kimekuwa kikilipwa fedha za Mfuko wa Bima ya afya kama zahanati kutokana na baadhi ya taratibu ambazo zilikuwa hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zimekwishalifanya kazi na barua rasmi itapelekwa ndani ya mwezi huu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Dugange yaani sasa hivi mnajibu vizuri moja kwa moja, hongereni sana. Mheshimiwa Mwanyika nimekuona, ulikuwa hujui kama Kituo hiki ni cha Afya? Swalii la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa lakini bado kuna sintofahamu kuhusiana na *status* ya hiki Kituo. Nitaomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie kwa karibu kwa sababu, wananchi wale wenye Bima wanashindwa kupata huduma kwa sababu wanasema *officially* hakijawa *registered* kwa hiyo kuna sintofahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili, pamoja na Kituo hiki lakini Njombe tuna vituo vingine viwili vya Afya ambavyo havina vifaa ambavyo tumeahidiwa kwa muda mrefu, Kituo cha Makoo pamoja na Kituo cha Kifanya. Mawaziri wametembelea pale lakini tumepewaa ahadi na hatuelewi. Sasa je, Serikali inaweza ikatoa kauli kuhusiana na hivyo vituo viwili? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Festo John Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Ihalula imekwisha pandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya na imekwishapewa namba ya usajili kama Kituo cha Afya. Kwa hivyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo sintofahamu ilikuwa kwa sababu hatukuwa tumepata namba rasmi ya usajili kuwa kituo cha Afya ili *National Health Insurance Fund* waanze kuilipa moja kwa moja. Kwa hiyo, sasa limeshafanyika, lakini kama kuna changamoto nyingine zote tutakwenda kuzifuatilia kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma za ngazi ya Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, tumekuwa na ujenzi wa Vituo vingi vya Afya, vikiwemo Kituo cha Afya cha Makoo na Kifanya; na mpango wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha za ununuzi wa Vifaa Tiba na Makoo ni moja ya vituo ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Nchi alitembelea, aliahidi Vifaa Tiba na utaratibu unaendelea kuhakikisha Vifaa Tiba vinafika pale. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili linafanyiwa kazi. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya TAMISEMI, Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

Na. 60

**Halmashauri ambazo hazipeleki Asilimia 40 kwenye  
Shughuli za Maendeleo**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziwajibisha halmashauri nchini ambazo zinajiweza kimapato lakini hazipeleki asilimia 40 ya mapato ya ndani kwenye shughuli

za maendeleo kama zinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria na badala yake zimekuwa zikiwalazimisha wananchi wake wachangie?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tupo kwako Mheshimiwa Dkt. Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Uandaaji wa Bajeti unaotolewa kila mwaka na Serikali unatoa maelekezo kwa halmashauri zote nchini kutenga sehemu ya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Halmashauri zenyet mapato yasiyolindwa chini ya shilingi bilioni tano zinapaswa kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani na Halmashauri zenyet mapato yasiyolindwa zaidi ya shilingi bilioni tano zinapaswa kutenga asilimia 60 ya mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha fedha shilingi bilioni 216.4 kimetumika kwenye shughuli za maendeleo sawa na asilimia 70.87 ya fedha zilizopaswa kutumika kwenye miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 kiasi cha shilingi bilioni 279.7 kimetumika kwenye miradi ya maendeleo sawa na asilimia 92 ya fedha zilizopaswa kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwisha wachukulia hatua watumishi 63 wakiwemo Wakurugenzi na Wakuu wa Idara, kwa kushindwa kutekeleza maagizo haya na utaratibu huu ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha Maelekezo haya yanatekelezwa kwa ufanisi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Niishukuru Serikali kwa majibu mazuri lakini niseme kitu kimoja tu kwamba Serikali Kuu inajitahidi sana kupeleka fedha. Sasa tusipokuwa makini kama hizi halmashauri tutaziacha kutopeleka hizi asilimia 40, kwa kweli maendeleo ambayo tunakusudia hatutayapata; na michango itazidi kuwa mingi sana kwa Serikali. Kwa hiyo, niishukuru Serikali kwa hatua iliyochukua naipongeza. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, una cha kusema Mheshimiwa Dugange? Kwa kuwa ameshukuru enhee, ahsante.

Mheshimiwa George Mwenisongole Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi. Hebu kule Jimboni kule hebu kidogo dozee! Dozee! dozee! Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni. (*Makof/Kicheko*)

Na. 61

### **Kuhamisha Kambi ya Jeshi katika maeneo ya wananchi Zanzibar**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

(a) Je, kwanini Serikali isihamishe Kambi za Jeshi la Wananchi (JWTZ) Zanzibar ambazo zipo katikati ya makazi ya watu kutokana na kasi ya maendeleo ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza? na

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za kumaliza mgogoro wa muda mrefu wa mpaka kati ya wakulima na JWTZ kambi ya Kisakasaka?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Waheshimiwa Wabunge Waziri wa Ulinzi anajibu nadhani kwa mara ya kwanza sasa. Kwa hiyo, anastahili mumkaribishe. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Kwa kunitfea kuwa Mbunge na hatimaye kunitfea kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Lakini pia na kwako kwa ushirikiano ambao nimekuwa nikiupata tangu niteuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Makambi na Vikosi vya Ulinzi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania yameundwa kwa Mamlaka ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa Na. 24 ya Mwaka 1966, ambayo imefanyiwa marekebisho na Sheria Na. 192 ya Mwaka 2002. Makambi haya na Vikosi yamejengwa kimkakati kukabiliana na tishio lolote dhidi ya Nchi yetu. Maeneo haya ni muhimu sana kwa ulinzi na usalama.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa migogoro baina ya Jeshi na wananchi wa Vijiji vya Sheha za Kisakasaka, Mwangani, Kombani, Fuoni na Kondemaji. Kwa nyakati tofauti serikali imefanya jitihada za kutatua mgogoro huu. Hivi sasa Wizara yangu inatekeleza Mkakati maalum wa miaka mitatu wa kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya ardhi baina ya Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Mpango huu, Wizara imepanga kufanya upimaji na uthamini katika maeneo haya niliyoyataja katika robo ya pili ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo ni robo hii. Wizara inawaomba wananchi

kuendelea kuwa na subira wakati Wizara ikiendelelea na utekelezaji wa Mkakati huu wa upimaji na uthamini wa maeneo yote ya Jeshi.

(c) Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe rai kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya Jeshi, kuacha kuvamia maeneo hayo kwani ni hatari kwa usalama wao, na ni vigumu kwa Jeshi kuhamisha makambi kwa kuwa makambi hayo yamejengwa kimkakati. Nawasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, nimekuona.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, amenijibu kuwa Serikali ina mpango wa kufanya upimaji na kufanya tathmini. Je, wakati itakapofika kufanya tathmini na upimaji, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari na mimi niambatane naye kwenda kwenye zoezi hilo? (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Jana masuala ya kuambatana ambatana, Mheshimiwa Waziri majibu tafadhali. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mheshimiwa Mbunge ni mdau wetu na tutakuwa tayari kuongozana naye wakati zoezi hili likiendelea. (*Makofi*)

**SPIKA:** Enhee kuongozana ruksa lakini kuambatana hapana. Mheshimiwa Esther Matiko, nimekuona swali la nyongeza. (*Kicheko*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Wananchi wa Bugosi na Kenyambi kule Tarime Mjini walichukuliwa ardhi yao na Jeshi la Wananchi wa Tanzania tangu 2008, na jeshi hili au Serikali ilifanya tathmini mara ya kwanza 2013, 2017 wakafanya tathmini tena, 2019 na mara

ya mwisho na ulitilia mkazo hapa Bungeni walikwenda kufanya uhakiki Juni, 2021 na wakatoa namba ya malipo na wakaahidi kwamba kufikia Agosti, 2021 watakuwa wamelipa lakini mpaka sasa hivi hawajawalipa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni lini sasa wananchi hawa wa Kenyambi na Bugosi watalipwa fidia zao, ili wapishe Jeshi la Wananchi wa Tanzania waende sehemu zingine kufanya makazi na shughuli za kimaendeleo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Stergomena Tax, tafadhalii.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Esther Matiko kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika mkakati huo wa miaka mitatu tayari tumeshafanya tathmini na uhakiki katika maeneo yote isipokuwa maeneo ya Zanzibar ambayo ndiyo tutayafanya *quoter* hii. Kinachoendelea sasa baada ya huu utathmini ni kufanya uhakiki na uhakiki unaendelea katika maeneo yote ambayo yamefanyiwa tathmini na uhakiki ili tukishakamilisha uhakiki taratibu nyingine zitafuata. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Maji, sasa Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela.

Na. 62

### **Kuhuishwa kwa Sera ya Maji**

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahuisha Sera ya Maji ili iendane na wakati kwa kukidhi mahitaji halisi kwani kwa sasa haiendani na viwango vya kimataifa na imepitwa na wakati?

**SPIKA:** Majibu kutoka Wizara ya Maji nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Maji ndiyo mwongozo unaotumika katika kutekeleza jukumu la Serikali la kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji na kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. Lengo la Sera ya Maji ya mwaka 2002, ilikuwa ni kuweka mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza na kusimamia kikamilifu rasilimali za maji. Kupitia Sera hii, umekuwepo ushirikishwaji wa walengwa wa huduma ya maji katika hatua zote za utekelezaji, uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilianza utaratibu wa kuhuisha Sera ya Maji hiyo ambayo imetekelvezwa kwa takribani miaka 19 ili iweze kukidhi mahitaji ya Mipango iliyopo ambayo ni; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Awamu ya Tatu 2021 – 2026; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2015 – 2030; na Mageuzi ya Viwanda Awamu Nne (*Fourth Industrial Revolution*).

Mheshimiwa Spika, matarajio ni kukamilisha hatua zote ifikapo mwezi Juni, 2022 na Sera mpya ya Maji ianze kutumika ikianzia mahitaji halisi na kufikia malengo ya Uchumi wa Kati na Maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kyela.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa sera yetu sasa itachukua muda kuihuisha mpaka mwaka 2022; na kwa kuwa mpaka sasa kuna miradi mingi sana ya maji inaendelea na kwa kuwa pamoja na Sera hii kuna uhitaji wa maji wa kila mwananchi anahitaji kiasi gani kwa siku. Je, miradi inayofuata kwa sasa, Serikali imejipangaje kuhakikisha inakuwa endelevu?

Mheshimiwa Spika, la pili, mradi mmojawapo ambao umeathirika sana kwa Wilaya ya Kyela na hii Sera ya Maji ya watu 250 kuchota kwenye kituo kimoja ni Mradi wa *Ngana group*. Serikali imejipangaje sasa kuhakikisha mradi huu unaufufuliwa na unakuwa katika viwango vya sasa ili kukidhi matarajio ya wana Kyela? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo kwako Mheshimiwa Mhandisi Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mlaghila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa miradi ambayo inaendelea sasa hivi ni miradi endelevu na tayari tunajitahidi kuhakikisha kuona kwamba tunapata vifaa vya kufanya uchunguzi kabla ya kuingia kwenye miradi na tumshukuru kabisa kwa kipekee Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuititia fedha ambazo tumepewaa tayari tumeagiza mitambo saba kwa ajili ya kuchunguza maeneo ambayo yatatuletea vyanzo endelevu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa Mradi wa Ngana *Group* tayari umeshafuliwa, wiki hii fedha zaidi ya shilingi milioni 500 tunaelekeza huko, ili kuona kwamba shughuli za awali zinaanza kutekelezwa. (*Makof*)

**SPIKA:** Bado tuko Wizara ya Maji. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani kwa niaba yake Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la Namtumbo.

Na. 63

### **Hitaji la Maji baadhi ya Vijiji – Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA K.n.y. MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupelekea maji katika Vijiji vya Lingusenguse, Lusewa, Namwinyu, Mchomoro na Luchiri Wilayani Namtumbo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko kwako Mheshimiwa *Engineer*.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa maji inaboreshwu katika Wilaya ya Namtumbo, ambapo kwa sasa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani humo ni asilimia 69. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji katika Halmashauri hiyo ambapo katika Vijiji vya Lingusenguse, Lusewa na Mchomoro kazi zinazoendelea ni pamoja na ukarabati wa pampu ya mkono, ujenzi wa chanzo, ukarabati wa tanki la ujazo wa lita 50,000, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji (16) na ulazaji wa bomba la kusambaza maji urefu wa kilomita tisa. Kazi zote zinatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kijiji cha Namwinyu ujenzi wa mradi utaanza robo ya tatu ya mwaka 2021/2022 na utahusisha uchimbaji wa kisima kirefu, vituo vinne (4) vya kuchotea maji, ulazaji wa bomba kilomita tatu (3) na ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji la lita 90,000.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Luchili wananchi wa Vijiji vya Namanguli, Misufini, Chengena na Kilangalanga wanapata huduma ya maji kuititia visima 24 vinavyotumia pampu za mkono. Katika mwaka 2021/2022, Serikali kuititia RUWASA itachimba visima virefu viwili (2) na kujenga miundombinu ya kusambaza maji. Kazi hizo zinatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hiyo kutaondoa tatizo la maji katika vijiji viliviyotajwa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa nimekuona.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, bado Mji wa Namtumbo una uhaba mkubwa wa maji na kwa kuwa kuna fedha hizi za UVIKO zinazohusiana na sekta ya maji, Serikali inaweza ikaelekeza fedha hizo RUWASA wakazielekeza katika ukarabati wa chanzo cha maji kinacholeta maji Namtumbo na kutandaza bomba la maji jipya? Kwa sababu, chanzo hicho ni cha toka mwaka 1980 ili kutatua tatizo la maji ya pale Namtumbo Mjini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa pia tuna miradi ya maji ya Luhimbaililo na Ikesi na maji ya Kumbala, Litola, miradi hii imekuwa kizungumkuti bado hatujui itaisha lini. Je, Serikali mnaweza mkaja mkatusaidia kuona nini kinachokwamisha ucheleweshaji wa miradi hii miwili? (*Makofii*)

**SPIKA:** Hivyo vijiji Mheshimiwa Naibu Waziri atavijua kweli huko ungonini huko? Mheshimiwa Naibu Waziri Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani yaliyoulizwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, fedha za UVIKO kutumika kwenye kuboresha chanzo cha maji. Hizi fedha za UVIKO sisi kama Wizara tumeelekeza kwenye miradi ambayo itakwenda kukamilika na kuleta huduma mara moja kwa jamii. Tunataka miradi ambayo inaleta majawabu kwa haraka hivyo, namna ambavyo Mkoa umeelekeza ile fedha ni sahihi. Kuhusiana na kazi hii ya kukifanyia hiki chanzo cha maji kinachotegemewa pale Namtumbo, tutatumia fedha za Mfuko wa Maji kuhakikisha kwamba tunakuja tunahakikisha chanzo kinatumika kikamilifu kwani vyanzo ni vichache. Hivyo, tunapopata vyanzo kama hiki tutakitumia kikamilifu ili kuleta tija kwenye jamii yote ya Namtumbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Vijiji vya Ikesi pamoja na hivyo vingine, Serikali inatoa jicho la kipekee kabisa kuona kwamba maeneo haya ambayo kwa muda mrefu yamepata shida ya maji, tunakuja kuleta ufumbuzi na maji bombani yatapatikana kwa wananchi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa ni Mwalimu huyu? Endelea kuuliza swali lako.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jimbo la Songwe ni pana ni kubwa na lina vijiji viko *very scattered* na kutoka kijiji kwenda kijiji baadhi ya vijiji kuna Mito kama Maleza au Rukwa na Some. Sasa, tuko Novembra sasa na tayari watu wa RUWASA wanatuambia tumeshapata fedha kwa ajili ya kupeleka maji kwenye vijiji hivyo. Lakini mpaka sasa hatujaona wakandarasi kuanza kazi sehemu hizo na sehemu nyingi Tanzania nzima watu wa RUWASA wanasema wanafanya manunuzi lakini wanachelewa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali naomba ituambie ni lini hasa Wakandarasi wataanza kumwagika kwenye Wilaya zetu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji? Ukizingatia tunaenda kwenye wakati wa mvua? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Phillipo Mulugo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maji na Usambazaji wa Maji Vijijini *RUWASA* ni kweli palikuwa na changamoto katika eneo la ununuzi lakini tayari Mheshimiwa Waziri amewaaagiza na wamejipanga. Kipekee nimpongeze *Engineer Kivigalo* anafanya kazi nzuri ambaye ni *DG* wa *RUWASA*. Usimamizi wa kufanya manunuzi yaende kwa wakati sasa hivi utakuwa umeshaboreshw. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lini tunakuja tayari tupo kazini sisi Wizara ya Maji, katika eneo lako huenda ndiyo limechelewa tu kupata wakandarasi lakini maeneo mengi kazi zinaendelea. Hivyo, nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuonane tuone tunaweka sawa mambo kazi zikaanze mara moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho katika eneo hilo, Mheshimiwa Grace Tendega. Mheshimiwa Kunti, samahani nilimuona wa nyuma yako.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dodoma takribani sasa ni miezi mitatu mfululizo kumekuwa na mgao wa maji usiokuwa na taarifa. Leo mitaa mbalimbali kwenye Kata ya Ipagala, Kata ya Dodoma Makulu, lakini Kata ya Nzuguni wana siku ya tano hakuna maji.

Nataka kupata kauli ya Serikali ina mkakati gani madhubuti wa dharura wa kuondoa changamoto hii kubwa inayowakumba wakazi wa Dodoma, lakini na wagoni mbalimbali wanaoingia kwenye Jiji letu hili kufanya shughuli zao mbalimbali? Kwa sababu, imekuwa ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri yaani hakuna maji siku ya tano Dodoma hapa hapa na wewe mwenyewe upo. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji kuna maelezo kweli kwa wana Dodoma? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Jiji la Dodoma tumepitia kidogo changamoto katika mitambo yetu ya Mzakwe na pale Mailimbili. Tatizo kubwa ilikuwa ni umeme na tumewasiliana kwa karibu sana Mheshimiwa Waziri Aweso, pamoja na Mheshimiwa Makamba. Wamefanyia kazi hili suala kwa pamoja kuona kwamba *lane* ile ya umeme inayofanya uwezeshaji pale kwenye vile vyanzo usiwe *disturbed*. Kwa sababu, imekuwa *disturbed* huko mbele kulingana na ugawaji huu wa umeme wa REA, lakini sasa hivi wanaendelea kufanya maboresho ili kuona kwamba umeme usikatike kwenye vyanzo vyetu.

Mheshimiwa Spika, kwa dharura sana pale inapobidi sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira hapa Dodoma anajitahidi kuona kwamba maboza yanazunguka huko kutoa huduma pale inapobidi sana, lakini tayari maji yanarejea katika mfumo wake baada ya umeme kidogo kuwa unapatikana.

**SPIKA:** Labda Mheshimiwa Waziri kwa kuunganisha tu. Kwa kuwa ufumbuzi wa uhakika ni maji haya kutoka Ziwa Victoria, nini kinaendelea hivi sasa kutoka Ziwa Victoria kuja Mji wa Dodoma? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuja hapa Dodoma ni katika miradi yetu mikubwa ambayo tunategemea fedha kutoka nje. Wiki iliyoisha siku ya Ijumaa Wizara (wataalam) waliweza kuketi na *World Bank* kuendelea kufanya mazungumzo kuona huu mradi sasa unaingia kwenye utekelezaji.

**SPIKA:** Haya, kumbe mmehamia huko tena, sisi tulifikiri mnajenga kwa fedha za ndani. (*Makofi*)

Tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii. Uliza swalilako Mheshimiwa *Engineer Ezra*.

Na. 64

### **Mgogoro kati ya Hifadhi ya Burigi – Chato na Wafugaji**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Burigi – Chato ili waache kuingiza Mifugo ndani ya Hifadhi na kumaliza mgogoro kati ya wananchi hao na Hifadhi hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swaliliko, Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swaliliko Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *TANAPA* imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Taifa ya Burigi - Chato. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi 20,836,200 zilitumika kutoa elimu ya uhifadhi katika vijiji 37, ambapo katika Wilaya ya Biharamulo elimu hiyo ilitolewa kwa vijiji sita vya Kiruruma, Nyabugombe, Ngararambe, Kabukome, Katerela na vya Kitwechembogo.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga jumla ya Shilingi Milioni 96.7 kwa ajili ya utoaji wa elimu ya uhifadhi katika maeneo ya vijiji 38 vinavyopakana na hifadhi hiyo vikiwemo vijiji 10 vya Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utoaji wa elimu kwa vijiji, Serikali imejipanga kutumia makundi maalum wakiwemo viongozi wa dini, wanasiasa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ili waweze kusaidia katika kuelimisha faida za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chiwelesa, nimekuona.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo kubwa sana katika eneo hili la hifadhi hii ya Burigi Chato na tunashukuru kwa fedha ambazo zimetolewa na kutoa elimu kwa umma unaozunguka hifadhi ile. Kumekuwa na kesi kubwa sana pale za mifugo ya watu kukamatwa ndani ya hifadhi lakini baada ya kukamatwa zinapopelekwa kesi mahakamani, watu wale wamekuwa wanatozwa *fine* ya Shilingi 100,000/= kwa kila ng'ombe na wengi wanalipa baada ya kutozwa ile *fine*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa shida imekuja unatoza *fine* mahakamani ulikamatiwa ng'ombe 100 unapopewa barua ya mahakama, umeshalipa fedha ya Shilingi Milioni 10 ukarudishiwe ng'ombe wako unaenda unakuta ng'ombe wako 70, ng'ombe wako 80 badala ya ng'ombe waliookamatwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kusikia kauli ya Serikali juu ya vitendo hivi ambavyo vimesababisha wananchi wa Biharamulo kuteseka na hatimae kupoteza fedha zao na ng'ombe hao amba wamekuwa wanapotea huko. Nisikie kauli ya Serikali juu ya hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kumekuwa na kesi pia wananchi wananiufuata ninapokuwa Jimboni, saa nyingine wanapiga simu na kwa DC kesi zipo. Mwananchi anakuja

analalamika kwamba, Mheshimiwa Mbunge nimekamatiwa ng'ombe wangu 50 bado tuna kesi mahakamani, lakini ng'ombe wangu nimewaona kwenye mnada wanauzwa. Sasa naomba kusikia kauli ya Serikali juu ya hili jambo ambalo limesababisha watu sasa wanaona taabu kabisa na wanatuchonganisha na wananchi. Tukisikia kauli ya Serikali juu ya hili pia hao ng'ombe ambao wamekuwa wanauzwa kwenye mnada je, hatuoni haja ya Serikali kuunda Tume Maalum, kwa ajili ya kwenda kuangalia hivi vitendo vya wananchi kulalamika? Kwamba, ng'ombe wao wanauzwa kwenye mnada na ilhali bado kesi zinaendelea mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer Ezra Chiwelesa*, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niendelee kutoa pole kwa wale wananchi ambao wameendelea kukutana na kadhia hii, ya kudhulumiwa mifugo yao na kumekuwa ndiyo na malalamiko mengi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walishawahi kunifuata kwamba, kuna baadhi ya wahifadhi wasio waaminifu ambao inapelekea mifugo yao kutotimia kama ambavyo imekamatwa awali.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tunafahamu Sheria za Utumishi wa Umma, watumishi hawa tumekuwa tukiwachukulia hatua wale ambao wanahuksika na kadhia hii ikiwemo upotevu wa mifugo. Lakini pia kumekuwa na changamoto ya baadhi ya mifugo ambayo huwa inakuwa wakati ikiwa inasubiri kupelekwa Mahakamani kwa maana ya kesi inapochukua muda mrefu Mahakamani inapelekea baadhi ya mifugo kupoteza maisha. Lakini kwa upande mwagine ambao amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba mifugo mingine inaonekana iko minadani, basi Serikali

itaendelea kufuatilia na wale watumishi ambao wanahusika na changamoto hizi tutawachukulia hatua. Na inapothibitika basi wengine tunawasimamisha kazi na hata kufukuzwa kazi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge ambao wana changamoto hii, niwaombe pale kuna mfugaji ambaye amekutana na changamoto hii basi watusaidie kutupa hizi taarifa. Lakini pia niwaombe Waheshimiwa tuendelee kuelimisha hawa wafugaji pia, wakifuga kwa kufuata Sheria na taratibu za nchi ninaamini kabisa kadhia hii tutaipunguza kabisa ama kuimaliza. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Kule Msekwa nimekuona Mheshimiwa Yahaya Mhata, uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, katika harakati za Serikali kuhifadhi mazingira na maliasili yetu ilihamasisha wananchi kufungua mabucha ya wanyamapor. Wananchi wa Jimbo langu walihamasika na walifungua mabucha tatizo ni upatikanaji wa leseni kutoka Wizara husika.

Je, ni lini wananchi wangu watapatiwa leseni ili shughuli hii ya kuuza nyamapor iweze kuanza ndani ya Wilaya yangu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeendelea kutoa leseni za mabucha kwenye maeneo mbalimbali ya hapa nchini na hizi bucha ni kwa ajili ya wanyamapor. Mwaka wa fedha 2020/2021 tuliweza kutoa leseni zaidi ya 46 na tuna masharti ya namna ambavyo wanapaswa kuomba hawa wafanyabiashara wanaofanya biashara hizi za

wanyamapori. Lakini kumekuwa na changamoto ya ukosefu wa wanyamapori wenyewe, kwa maana unapowinda *kunta-target* ambazo wanazifahamu wawindaji. Sasa kumekuwa na malalamiko kwa wale wenyewe leseni wanakosa nyama na matokeo yake wanarudisha wanashindwa kuendelea na biashara hii.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kama kuna yeote ambaye anahitaji leseni, Wizara ya Maliasili na Utalii iko tayari wakati wowote kutoa leseni. Lakini changamoto inayojitokeza ni kwamba upatikanaji wa wale wanyama wenyewe ndiyo changamoto halisi inayojitokeza. Kwa sababu, uwindaji kuna maeneo ambayo tunayatenga lakini inapokosekana basi malalamiko yanarudi kwa Serikali, lakini leseni zipo tunawakaribisha wafanyabiashara wote waje. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba jirani na Burigi Chato.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa, ukosefu wa vitalu vyatufugia mifugo na maeneo ya malisho ndio sababu kubwa ya kipeleka mifugo hifadhini na kwa kuwa, elimu inayotolewa na Wizara ya Maliasili inatolewa kwa binadamu na siyo ng'ombe na kwa vile ng'ombe wao wanataka kula majani na wakati wa kiangazi hakuna sehemu ya majani na majani yako porini.

Je, Wizara ina utaratibu gani ama ina mpango gani wa kuhakikisha eneo lile la hifadhi linamegwa, tunapata vitalu kwa ajili ya kufugia mifugo yetu ng'ombe kwa upande wa Biharamulo na Ngara? Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya ukosefu wa malisho na imepelekeea kuwepo na migogoro baina ya Wahifadhi na Wafugaji. Serikali inatambua changamoto za ukosefu wa maeneo ya mifugo, lakini kupitia Kamati ya Mawaziri Nane ambao tumekuwa tukizunguka nchi nzima, tayari Serikali imetoa maeneo ambayo yatamegwaa kwa ajili ya wananchi kutumia. Hivyo tunaendelea kuelekeza wananchi wayatumie vizuri ikiwemo kutenga maeneo hayo kwa ajili ya malisho na kuanda matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya wafugaji na matumizi kwa ajili ya kilimo. Hivyo, Serikali imeshalionia hili na tumeendelea kutoa elimu lakini pia kumega maeneo ya hifadhi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inatosha. Nawaoneni lakini siku nydingine. Tuendelee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

Na. 65

### **Hospitali ya Kanda ya Kusini Kuanza Kutoa Huduma**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni lini Hospitali ya Kanda ya Kusini itaanza kutoa Huduma kwa Wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Mlapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara imewekewa jiwe la msingi tarehe 26/07/2021 na

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na huduma zimeanza tarehe 1 Oktoba, 2021. Ahsante.

**SPIKA:** Hili jibu *classic* kabisa. Mheshimiwa Tunza, bado hujaelewa tu jibu hilo liko moja kwa moja? Swali la nyongeza tafadhali Mheshimiwa Tunza Malapo. (*Makof!*)

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli Hospitali hiyo ya kanda imeanza kutoa huduma, lakini lengo la Hospitali ya Kanda ni kutoa huduma za rufaa. Huduma hizo hazijaanza kwa sababu hakuna vifaa na hakuna madaktari bingwa. Sasa swali langu: Ni lini vifaa na madaktari bingwa wataletwa katika hospitali hiyo kwa sababu hiyo ndiyo shida yetu sisi watu wa kusini hususan Mkoa wa Mtwara? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Ukiangalia mazingira ya nje ya hospitali ile, bado yapo shaghala baghala, ni lini yatawekwa katika mandhari ambayo inaendana na mandhari ya hospitali? Nakushukuru. (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri sana; na kweli mawazo mazuri aliyojatoa ndiyo mwelekeo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza hospitali hiyo imeanza na ni kweli bado watumishi hawajafikia idadi aliyoisema. Tumegawa uanziswaji wa hiyo hospitali. Ukiangalia hospitali yenyewe sasa ina umri wa mwezi mmoja na siku nane, lakini tumegawa uanzishwaji wake kwa *phase* tatu, maana yake tumeanza *phase* ya pili ambayo sasa wanaenda kuwekwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya hospitali hiyo na tayari shilingi bilioni tatu zimeingia kwa ajili ya kununua *CT-Scan* na *MRA*. Kuna *specialist* mmoja na mwezi ujao wanapelekwa 4 ili wafikie 5. Mpaka mwezi wa Pili ambapo tunaenda kwenye *Phase* ya tatu ya uanzishwaji wa hospitali, tutakuwa na watumishi 217. Kwa hiyo, Mheshimiwa ukitembelea mwazi wa tatu utakuta imeanza kama ulivytaka wewe.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ni kuhusu mazingira ya Hospitali. Kweli nimeyaona na mimi wakati jiwe la msingi linawekwa, bado mazingira yaliyozunguka siyo safi. Wakati tunaendela kwenye *phase* hizi, tunaendelea kuhakikisha vile vile na usafi unafanywa.

Mheshimiwa Spika, *OC* imetengewa shilingi milioni 600. Kwa hiyo, watatumla kwa ajili ya kuhakikisha mambo mengine yanakuwa sawa na kufikia lengo ambalo Wana-Mtware wangetegemea kuona.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, nimekuona umesimama.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Nami napenda kuiuliza Serikali: Ni lini itaimarisha utoaji wa huduma kwa magonjwa yale ambayo yalikuwa hayapewi kipaombele; magonjwa ya kitropiki, kwa maana ya *neglected tropic diseases* kwenye hospitali hii ya Kanda ya Kusini? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Spika, kwanza ukisikia tunaanzisha *specialists* mbalimbali, tunazungumzia magonjwa yote hayo. Ukisikia tunasema tunaongeza watumishi, ni kwa kuzingatia hayo. Ndiyo maanda unaona sasa kuzunguka nchi nzima, utaona kila Mkoa sasa unafanya wahamasa kuhusu magonjwa

ambayo ameyazungumzia. Juzi Arusha nilimwakilisha Waziri wa Afya kwenye kuzindua swala hilo kitaifa. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuhamie Wizara ya Elimu, swali linaulizwa na Mbunge wa Handeni Mjini, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa tafadhalii.

Na. 66

### **Ujenzi wa VETA – Handeni**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Handeni?

**SPIKA:** Naibu Waziri Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omar Kipanga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga Vyuo vya Ufundisti ikiwa na lengo la kuwa na Chuo cha Ufundisti katika kila ngazi ya Mkoa na Wilaya. Tangu mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetenga zaidi ya shilingi bilioni 76 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundisti 33, ambapo vyuo 29 ni vya ngazi ya Wilaya na vyuo vinne ni vya ngazi ya Mkoa. Mpaka sasa vyuo hivyo viko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Handeni kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Handeni ambacho pia kinatoa mafunzo ya ufundi stadi. Katika chuo hiki Serikali

ilifanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu uliogharimu jumla ya shilingi millioni 599.6 na kwa sasa Chuo kinaendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea na juhudzi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* wilayani humo, nashauri wananchi wa Handeni kuendelea kutumia vyuo vilivyopo nchini, ikiwa ni pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi wa Handeni. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa, nimekuona.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwenye swali langu la msingi. Kwa kuwa Serikali imewaelekeza wananchi wa Handeni kuendelea kutumia Chuo cha Wananchi cha Maendeleo kilichopo Handeni wakati tukingoja ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya yetu: Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa vya kufundishia kwenye chuo hiki cha *FDC* kwa maana ya vitabu, mitambo na mashine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali haioni umuhimu wa kukiendeleza chuo hiki cha *FDC* kilichopo ili kifiki kwa katika hadhi ya Chuo cha *VETA*? Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOGIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjii kama ifuaavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 10/10/2021 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliubainishia Umma kwamba tumepata fedha zile ambazo zinatokana na namna gani tunaweza kuondoa changamoto ya Uviko 19.

Katika fedha hizo, jumla ya shilingi bilioni 6.8 zimetengwa kwa ajili ya kupeleka vifaa pamoja na mitambo ikiwemo na vitabu katika vyuo 34 vya *FDC*. Miongoni mwa vyuo hivyo 34, kimojawapo ni hiki chuo cha Handeni.

Kwa hiyo, nimtoe wasiwaso kwanza Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga vizuri, tunakwenda kupeleka vifaa pale ili kuhakikisha tunaboresha mazingira ya ufundishaji pamoja na vifaa ili vijana wetu waweze kupata taaluma yao katika eneo lile. (*Makofii*)

Katika eneo la pili anazungumzia namna gani tunaweza kuboresha chuo kile labda kiweze kuwa na hadhi ya *VETA*. Vyuo hivi vya *FDC* vilianzishwa kwa mkakati maalum wa kuhakikisha tunapeleka maendeleo katika maeneo yale. Hatuna sababu ya kuvibadilisha vyuo hivi kwenda kuwa *VETA*, ingawa bado vinatoa mafunzo haya ya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa vile Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga *VETA* katika kila Wilaya katika mipango yetu ya baadaye, chuo hiki tutaendelea kukiimarisha ili kiweze kutoa mafunzo na tija katika eneo hili ambalo limekusudiwa na Serikali wakati Serikali inajipanga kutafuta Chuo cha *VETA* katika eneo hilo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi sasa, swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Mbunge wa Singida Kaskazini.

Na. 67

### **Ujenzi wa Barabara ya Iliongero – Mtinko –Hydom kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ABEID I. RAMADHANI** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Singida kuititia Mji Mdogo wa Iliongero – Mtinko hadi Hydom ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Singida, Manyara na Simiyu.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya llongero – Mtinko hadi Hydom kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe.*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya llongero – Mtinko hadi Hydom yenye urefu wa kilometra 93.3. Mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa mwezi Oktoba, 2021 na kazi inatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2022. Mara baada ya kazi ya Usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Singida Kaskazini, uliza swali lako tafadhalii.

**MHE. ABEID I. RAMADHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri yenye natumaini ya Serikali lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba mkataba umeshasainiwa tangu Oktoba, 2021 ambapo utachukua mwaka mzima mpaka 2022 mwishoni. Kwa nini sasa upembuzi yakinifu uchukue muda mrefu hivyo kwa kilomita 93 tu wakati tayari fedha zipo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Kwa kuwa hadi sasa sijaona chochote kinachoendelea katika barabara hii, Waziri yuko tayari kuongozana nami hadi *site* kwenda kuona na kusimamia utekelezaji wa kazi hii uanzé ipasavyo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na uchukuzi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Mbunge wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilomita 93.3 ni kilomita nyingi na tunachofanya siyo tu upembizi yakinifu ni upembezi yakinifu na usanifu wa kina ambao ndiyo utatoa sasa gharama ya hii barabara itahitaji kiasi gani. Kwa hiyo, baada ya hilo nadhani pengine kwa bajeti itakayofata ndiyo sasa tutakuwa tumepata gharama ili kuanza kuingiza kwenye mpango kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge ambaa barabara hii inawahusu, mara baada ya kikao hiki cha Bunge nitatembelea Mkoa wa Singida kwani natambua barabara hii inaunganisha Singida, Manyara hadi Simiyu.

Kwa hiyo, nimejipanga kutembelea hii barabara, Mheshimiwa Mbunge awe tayari kwamba tutaongozana kuangalia hii barabara. Ahsante. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsatne sana. Nimekuona Mheshimiwa Godwin Kunambi, uliza swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kupitia bajeti ya mwaka huu wa fedha (2021/2022), Serikali imepamga kujenga barabara kwa kiwango cha lami Morogoro - Njombe Boda walau kwa kuanza na kilomita 50. Swali langu: Je, ni lini Serikali itatangaza zabuni walau ujenzi huu uanze kwa kilomita 50 hizi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko kwako Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge nataka nikuhakikishie kwamba barabara zote ambazo zimetengewa fedha tayari ziko kwenye michakato ya manunuzi. Kwa hiyo, mara tu hizo hatua zitakapokamilika, nikuhakikishie kwamba zitatangazwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Haya twende Kigoma, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kuuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Ujenzi kwamba katika kazi zilizotangazwa na zilizoanza kufanyika sasa hivi na TANROAD kule Kigoma, nyingi zimekwama kwa sababu *GN* hazijatolewa. Je, mna mpango gani wa kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha kuhakikisha *GN* hizo zinatoka kabla mvua nyingi hazijaanza kunyesha katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya mawasiliano na Wizara ya Fedha na tunapoongea hivi nina hakika muda siyo mrefu *GN* zitakuwa zimetoka ili tuweze kuanza kutekeleza hiyo miradi haraka kabla ya mvua hajakolea. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, labda kama kuna barabara ambayo ni *specific* ama kuna shida, hiyo haitatoka *GN* mpaka wajiridhishe kwamba kila kitu kimecaa sawa. Ila kwa barabara nyingine nina hakika siyo muda mrefu zabuni zote zitatangazwa baada ya kutoka hiyo *GN*. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la mwisho, tunakwenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, wewe mwenyewe.

Na. 68

### **Utafiti wa Uvunaji Mafuta Ziwa Tanganyika**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

(a) Je, nini matokeo ya Utafiti wa mafuta uliofanyika katika Ziwa Tanganyika zaidi ya miaka mitatu iliyopita?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvuna mafuta hayo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati Mheshimiwa Stephen Byabato, tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti wa mafuta katika Ziwa Tanganyika umegawanywa katika vitalu viwili; Kaskazini na Kusini. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, *TPDC* ilikusanya taarifa za uvutano wa usumaku zenyе jumla ya urefu wa kilomita 24,027 za mstari katika kitalu cha Ziwa Tanganyika Kaskazini. Tathmini ya taarifa hizo pamoja na taarifa za kijiolojia na kijifozikia zilizopatikana katika eneo la mradi zimevezesha kugundua na kutenga maeneo yenye uwezekano wa kuwepo kwa mashapo ya kuhifadhi rasilimali (*petroleum*).

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo Nchini (*TPDC*) kwa kushirikiana na Mwekezaji kutoka Kampuni ya *Beach Petroleum* ilifanya utafiti wa mafuta katika kitalu cha Ziwa Tanganyika Kusini kuanzia

mwaka 2010 mpaka mwaka 2017. Taarifa za utafiti huo ziliwezesha kubaini miamba yenyewe uwezekano wa kuhifadhi mafuta. Hata hivyo, changamoto za uchimbaji kisima katika Ziwa Tanganyika zilizomkabili Mwekezaji alishindwa kusafirisha vifaa veya kuchoronga kutokana na kina kirefu cha maji katika Ziwa Tanganyika na upatikanaji wa fedha zilisababisha Mwekezaji kushindwa kuendelea na utafiti na hivyo kulazimika kurudisha kitalu kwa Serikali mnamo mwaka 2017 kwa kuzingatia sheria zetu za mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa viashiria vizuri veya mafuta katika vitalu veya Ziwa Tanganyika, mpaka sasa Serikali hajagundua mafuta wala gesi katika eneo hilo. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 *TPDC* inatarajia kuendelea kufanya tathmini ya kina ya takwimu za usumaku kwa Kitalu cha Ziwa Tanganyika Kaskazini. Takwimu hizi zitatumika kutengeneza mpango wa kukusanya takwimu za mitetemo kwa ajili ya kuainisha na kuhakiki uwepo wa mashapo ya kuhifadhi mafuta na gesi. Nakushukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enga.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuzingatia taarifa iliyoolewa na Serikali ni kwamba kampuni iliyoleta inafanya utafiti ya *Beach Petroleum* tangu mwaka 2017 imeshindwa kuendelea na kazi hiyo kutokana na kina kirefu cha maji na wenyewe kushindwa gharama hiyo:-

Je, Serikali imetafuta mwekezaji mwingine katika eneo hilo tokea hiyo 2017? Kama hivyo ndiyo, wananchi wategemee lini utafiti huo kukamilika?

**SPIKA:** Majibu ya maswali haya.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2017 pale ambapo kitalu kilirudishwa na mwenzetu wa *beach petroleum* mtakumbuka kwamba kulikuwa kuna upiatiaji wa mikataba ya uvunaji na ushirikiswaji (*PSA*) na hivyo tangu kipindi hicho Serikali haijatangaza vitalu wazi kwa ajili ya wawekezaji kuja kufanya utafiti katika maeneo hayo. Hivyo, baada ya *PSA Review* kuwa zimekamilika sasa Serikali iko tayari kuanza kutanganza ili watu sasa waweze kuja kuwekeza katika maeneo hayo kwa ajili ya kufanya utafiti na baadaye kubaini uwepo wa mafuta na kuanza kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kilumbe Ng'enga kwamba Serikali iko katika hatua za kuhakikisha inakamilisha hiyo taarifa ya *PSA Review* na baada ya kufanya reviews zikakamilika, itaweza kufungua kwa ajili ya kuweza kukaribisha sasa watu kuja kuendelea na utafiti. Itakapofanya hivyo, basi taarifa ya nini kimepataikana itatolewa. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la mwisho kabisa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Utafiti kama huo ambao umefanyika Ziwa Tanganyika umewahi kufanyika pia katika Ziwa Eyasi katika Jimbo la Karatu kuhusu upatikanaji wa mafuta katika ziwa hilo. Je, utafiti huo umekamilika au bado na je, matumaini ya kupata mafuta yapo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Stephen Byabato, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunalo bonde linaitwa Bonde la Eyasi Wembere ambalo linatoka Singida, linapita Tabora, linapita Simiyu na kipande cha Manyara pia kipo. Utafiti katika

bonde hilo unafanywa na Shirika letu la *TPDC* na kwenye Bonde la Eyasi-Wembere bado tunaendelea na utafutaji wa awali wa kujuwa maeneo ambayo tunaweza tukapata mafuta au gesi katika maeneo hayo. kwa hiyo, utafutaji bado unaendelea na utakapokuwa umekamilika, basi utapata matunda ya kuweza kuvuna gesi na mafuta.

**SPIKA:** Muda wa maswali umekamilika na maswali yameisha ndani ya saa moja ileile iliyotakiwa. Sasa niwatambue wageni ambao tunao katika Jukwaa la Spika ambao pia, ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Tuna Waambata wa Jeshi toka nchi mbalimbali za Afrika, Marekani pamoja na Viongozi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kwa upande wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania tunao makamanda wafuatao; Brigedia Jenerali Furahisha Ntahena, Tunaye Kanali Agneta Mapunda. Tunaye Meja Stephen Ukugani. Tunaye Meja Abuu Msofe. Tunaye Kapteni Lulu Chiago. Tunaye Sajenti Stanslaus Isangi. Ahsante sana na karibuni sana maafande wetu. (*Makofii*)

Pia, tunao wageni kama nilivyosema, waambata jeshi kutoka nchi mbalimbali; kutoka Uganda tunaye Meja Jenerali Stephen Kashaka, ahsante sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa, wageni wetu hawa tunatakiwa tuwapokee vizuri, si ndio jamani eeh? Sisi si ni wakarimu eeh?

Tunaye kutoka Zambia Brigedia Jenerali Mutila Musonda. Kutoka Angola tunaye Brigedia Jenerali Jose Clementino. kutoka Kenya jirani yetu tunaye Kanali Salash Kantai. Kutoka Misri tunaye Kanali Sheriff Fahad. Kutoka Rwanda jirani, Kanali Stanslaus Gashugi. Kutoka Burundi tunaye Kanali Sebastian Banderubosa. Kutoka Malawi tunaye Kanali Olton Msukwa. Kutoka Angola tunaye Luteni Kanali Anjo Gabriel Gimne. Kutoka Marekani tunaye Luteni Kanali Serge Metes. Msaidizi wa Mwambata wa Jeshi la Marekani Collin Soli na Msaidizi mwingine Madam Sharon Spoon. Ahsanteni sana wageni wetu kutoka Balozi mbalimbali na

wale wa kutoka jeshini kwetu, tumefurahi sana kupata ugeni huu hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri wetu wa Ulinzi yuko hapa kwa hiyo, karibuni sana. (*Makof*)

Tuna wageni 11 wa kutoka Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Kwanza kwa ujumla wenu karibuni sana, tunapopata wawakilishi kututembelea tunafarijika sana, karibuni sana. Karibuni sana, lakini nitawainua mmojammoja; naomba tuanze na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi, Dkt. Mwinyihaji Makame. Makamu wa Mwenyekiti, Dkt. Mohamed Said Mohamed. Mjumbe Ndugu Afadhal Taib Afadhal, Mjumbe wa Kamati Kuu huyu. Karibuni sana. (*Makof*)

Mjumbe mwingine Seif Shaban Seif. Mjumbe mwingine Khatib Haji Khalid. Mjumbe mwingine Khadija Ahmed Omar. Mjumbe mwingine Hidaya Ali Makame. Katibu wa Tume Mahmoud Ahmad Haji. Afisa Msaidizi wa Tume Ndugu Khamis Silima Juma. Afisa Msaidizi wa Tume Mboja Ali Shekhe na Sekretari wa Tume, Moza Seif Juma. Karibuni sana, inaelekea Tume ya Baraza la Wawakilishi pia nayo inatoka nje ya Baraza, inaelekea kama maana majina mengi haya nayaona kama sio ya mle ndani, lakini tutaeleweshana baadaye, kufahamishana. (*Makof*)

Karibuni sana mjisikie mko nyumbani. Tume yenu itakuwa na kikao nanyi, lakini pia mkihitaji jambo lolote kutoka uongozi wa Bunge na Wabunge tuko tayari kufanya maandalizi.

Tunao wageni watatu kutoka *United Bank of Africa (UBA)* au wengi tumezoea kuita *UBA*; ni *Branch Manager* Ndugu Joseph Mnembuka. Yuko *Relationship Manager* Ndugu Shufaa Yussuf na pia, *Relationship Manager* Ndugu Fahim Zubeir. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge hii Benki ya *UBA* iko hapa Dodoma pia. Ni benki ya kimataifa na mambo yake ni mazuri, muwatatembelee tembelee wana mambo mazuri sana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 63 wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao ni viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Rufiji wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo Ndugu Rajab Mbconde. Karibuni sana ndugu zetu kutoka maeneo mbalimbali ya Rufiji; naamini wengi wenu mnatoka pale Utete na maeneo mengine ya Rufiji. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mimi enzi zangu niliwahi kuishi Matingi kule Kingupira kule Rufiji. Kwa hiyo, nami ni Mrufiji mwenzenyu ndugu zangu, nilipokuwa Selous. Mheshimiwa Waziri yuko hapa, Mheshimiwa Mchengerwa anachapa kazi bila wasiwasi wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rajabu Mbconde yuko wapi? Mwenyekiti Rajabu Mbconde? Ooh, karibu sana Mwenyekiti. Hongera sana, tunakutakia kila la heri uchaguzi wa keshokutwa, *In Shaa Allah*. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ambao ni wadau wa maendeleo kutoka *Bright African Primary and Secondary School*, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo Ndugu William Komba. Wale wa kutoka *Bright?* Sijawaona. Basi karibuni kama mko popote pale au mko njiani mnakuja.

Wageni saba wa Mheshimiwa Salum Musa Omar ambao ni wajasiriamali kutoka Jimboni Gando, Kaskazini Pemba, wakiongozwa na Msimamizi wa Vijana, Ndugu Salum Kaim. Kutoka Gando, aah, karibuni sana wageni wetu kutoka Pemba mpaka hapa mbali kidogo. (*Makofi*)

Wageni nane wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Babati Vijijini, Mkoani Manyara, wakiongozwa na Ndugu Yona Sino. Wale kule, karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge uzoefu unaonesha kwamba, kwenye Bunge hili kwa sababu, baada ya Mkutano huu wa Tano, Mkutano wa Sita utakuwa *around* mwishoni mwa Januari, Februari mwakani.

Kwa hiyo, wakati huu huwa tunajaza fomu zile za Maadili ya Viongozi wa Umma, zile fomu za tamko la viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni na kuzipeleka ama Ofisi ya Spika ama yule mwenye uwezo anapeleka kule Tume moja kwa moja.

Nawakumbusheni basi wale ambaeo watakuwa tayari kupitia pale Ofisi ya Spika, kwenye Jengo la Utawala, kuchukua zile fomu ili kuweza kuzijaza kuhusu mambo haya. Inachosha kidogo, lakini ni sheria kwamba, kila mwaka tujaze mali na madeni, na kadhalika, kwa hiyo, tufanye hivyo.

Kwa yule ambaye, muda bado lakini, ukiona una muda unaweza kwenda zako, lakini ukumbuke tu ile *deadline* ya tarehe 31 Disemba, isipite kwa sababu, kuna *consequences* katika jambo hili. Ujazaji wake ni vizuri kuweka kumbukumbu unapojaza ukapiga *photocopy* ukatunza ikusaidie mwakani kwa sababu, mwakani huna sababu ya kurudia vile ulivyoviandika mwaka jana, unaviandika vipyta, sio kila siku unaanza upya ooh.

Mimi nina eka mbili mahali, kila siku eka mbili; itaonekana kama vile zinaongezeka kumbe unaongelea zilezile tu. Ukishajaza mara ya kwanza sasa unajaza vinavyoongezeka, vilivyoongezeka, isipokuwa *account* yenyewe unajaza fedha *as that day* ambazo ziko katika *account* na kadhalika. Kwa hiyo, ujazaji wake sio una, unakwenda hivyo, unaenda na mabadiliko yallyojitokeza. (*Kicheko*)

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Tatu kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo.** (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to keep the Law updated with some challenges observed in its implementation*)

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana nilipokea, kutoka kwa Mheshimiwa Rais Muswada wa Dharura, ambao umekuja katika Hati Iillyosainiwa na yeye mwenyewe ktuomba Waheshimiwa Wabunge tuitie Muswada huu wa Sheria, kama ulivyosomwa na Katibu wetu. Ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2021.

Kwa hiyo, kwa kuwa, umeshasomwa mara ya kwanza, naupeleka kwenye Kamati ya Bajeti, ni Muswada unaohusu masuala ya fedha na kwa hiyo, baada ya hapa, kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti huchangii nitakuomba mara moja mwende kwenye ukumbi wenu wa kawaida. Kwa kuwa, Waziri wa Fedha yuko hapa basi atajua mwenyewe namna atakavyogawa watu wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataona ni nini cha kufanya, lakini Kamati ya Bajeti *immediate* nikimaliza matangazo haya muanze kwenda ili muanze kuzingatia mapendekezo yaliyoletwa. Kwa kipekee Mheshimiwa Rais kwa usikivu mkubwa alionao katika mabadiliko ya sheria hizi pia, ameleta mapendekezo kwamba, tufute ile sheria iliyotunga asilimia mbili ya *withholding tax*. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili lina watu wavivu kweli, sheria hii ni kero kubwa namna hii mnipaiga makofi hayo kweli? Naomba makofi kwa Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Ndiyo, *unless* ninyi sio wawakilishi wa wakulima jamani? Kama ni wawakilishi wa wakulima hii ni kero kubwa sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa pendekezo hili, sasa mpira uko kwetu labda tukatae sisi, kwa sababu, pendekezo ndio hili ambalo nawaomba Kamati ya Bajeti waende wakazingatie na hizo mbili nytingine, ziko sheria tatu. Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti mnaweza mkaanza kwenda.

Pia niwaeleze kwamba, ile ratiba yetu imebadilika kidogo sasa, ambapo kesho tutakuwa na ile Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo, kesho Jumatano jioni, halafu keshokutwa Alhamisi tutaingiza haya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na.6, halafu Ijumaa kufunga Bunge. Wale wenye semina za asubuhi nao wataendelea kama kawaida. (*Makofi*)

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**SPIKA:** Kamati ya Mipango.

### **KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Leo hatutachangia wote, ndio shida ya wanaopenda kuchangia mwishoni, wanaopenda kusikiliza wenzao halafu wao nao ndio wanapata wazo la kuchangia. Kwa hiyo, mtakapoishia ni hapohapo kufuatana na muda tulionao.

Tunaanza moja kwa moja bila kupoteza muda na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ali Mchungahela.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata hii nafasi. Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa Serikali nzima ikiongozwa na Rais wetu kwa kazi nzuri na kutupatia Mpango wa kujadili. Pili, kwa sababu, hapa sipaswi kuongea mambo ya jimbo sana na Ndugu zangu wa Musoma Vijiji wanajua mambo yetu yanaenda vizuri kasoro barabara zetu ambazo nimeongea na *TANROADS* watabadili mbinu tuweze kupata lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yameongelewa, tunapaswa kutoa ushauri. Hapa napenda kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayaongea haya ikiwa kama wahusika watapendezwa wataona yana uzito, basi wanaweza wakayaingiza kwenye mpango ambaao wametuletea; kwanza kabisa wakati tunajadili hivi tujue hii ni sehemu ya Mpango ambaao unatuelekeza mwaka 2025 tutakuwa tunakamilisha miaka yetu ile mitano ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambacho ni kikubwa sana tukifika 2025 tukiwa watu milioni 70 pato letu la Taifa linapaswa kuwa karibu zaidi ya bilioni 210 ikiwa kama pato la mtu mmoja mmoja kweli litafika dola 3,000 kwa mwaka, ndio malengo yetu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tufike huko kwa kupitia huu mpango mimi nilitaka kwanza mpango wetu watakavyoenda kuutekeleza uwe na malengo. Malengo hasa ni nini tukiwa tunaelekea 2025 na hii ni *transit period?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachotaka kuona kinawekwa msisitizo ni ukuaji wa uchumi, lengo kubwa hilo, *growth*. Tumeshuka nne, tutaenda tano, sasa tujitahidi kama tunataka kuondoa umasikini nchi hii tujitahidi uchumi uvuke asilimia saba na wanasema ukiwa asilimia nane duniani kote ndio umaskini unapungua. Ukiwa chini ya nane

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tujue umasikini bado una sisi. Tukitaka kwenda vizuri sana mpango tuelekeze kwenye ukuaji wa asilimia 10 na zaidi ndio tutasema sasa uchumi unaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la pili ni kuwafanya wananchi waishi kwa neema yaani *wealth creation* sijui kiswahili chake lile ni lengo la pili la muhimu sana. Lengo la tatu, kwenye huu Mpango ni suala la ajira tulipaswa kueleza ajira ndani ya mwaka huu mmoja tutatengeneza ajira ngapi? Na tunakoelekea 2025 tunadhani tutakuwa tunatengeneza ajira ngapi kila mwaka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni huduma kwa jamii hayo sasa ni maji, umeme, barabara, hizo ni *community service* huu Mpango unapaswa kutueleza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho sikukiona sijakisikia lengo letu tunataka shilingi yetu iwe kubwa, tuna *gold refineries* mbili mpya tumesema tuanze kuwa na akiba ya dhahabu *gold reserve* naomba huu Mpango nao useme kwenye huu mwaka unaokuja tutaanzaje? Tutaendaje kwa sababu sasa tuna *refineries* ambazo zinaweza zikasafisha dhahabu kufikia zaidi ya asilimia 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ndiyo maeneo ambayo tunategemea yawe kwenye Mpango. Lakini nini cha kufanya kutekeleza hayo malengo nini cha kufanya cha kwanza kabisa kimeongeleta na kila mtu ni suala la kilimo hicho ndicho cha kufanya sasa wengi wameyaongea sitaki kurudia huko tena kilimo. Lakini tukisema kilimo tunachukua maana ya mifugo, uvuvi yote hiyo tunaweka kwenye kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni suala la elimu Taifa lote duniani kote hata mataifa yaliyoendelea kila mwaka yana mpango wa elimu na sisi tunataka tufate huu mwaka mmoja tutakuwa na shule ngapi mpya tutaajiri walimu wangapi tutakuwa na vyuo vitatoa wangapi? Mpango wa elimu lazima ujulikane uwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni afya tunajenga vituo vya afya tunajenga zahanati lakini kwenye Mpango useme kwamba kwa huu mwaka tunakuwa na zahanati kadhaa, vituo vya afya kadhaa, hospitali za rufaa kadhaa. Kingine ni miundombinu ambayo tumesema kamati ya bajeti naishukuru kwa staili ya kilometra tano tano, tatu tatu kila mkoa hiyo siyo mbinu nzuri ya kujenga barabara zetu. Lakini Mpango utueleze utashughulikaje na mambo ya miundombinu hasa mabarabara ya vijiji ambayo yanaenda kuleta mazao kutoka vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na cha muhimu zaidi Mpango uongelee mambo ya mazingira na tabia nchi ni vitu viwili tofauti *environment and climate change* ni vitu viwili tofauti mazingira na tabia nchi. Mpango sidhani kwamba umejieleza dunia inasema tushuke chini ya nyuzi 1.5 lakini sehemu zingine za Tanzania *temperature raise* inafika mpaka *three degrees celosias* kwenye *Indian ocean* imeshavuka 1% *celosias* mpango ueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango sasa ikiwa hayo ndiyo maeneo na malengo, tutoe wapi fedha nadhani hiki ndiyo kitu muhimu sana *financial resources* cha kwanza ambacho Mpango unapaswa kuegemea kabisa na mapato mengi yatatoka kwenye kilimo na kilimo kama nilivyosema mwezi Februari lazima tuwe na *priority* hatuwezi kwenda na mazao yote kwa mpigo lazima tuchukue mazao ambayo yanahitajika duniani sasa hivi tuko karibu watu bilioni 8 na watu wanakula mchele kila siku wanatumia ngano kila siku wanatumia mahindi kila siku, wanatumia muhogo hayo mazao manne ndiyo ya muhimu halafu na mazao ya *horticulture* hayo matunda ma-*avocado* na nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu utueleze tutazalisha mahindi kiasi gani? Ngano kiasi gani? Mihogo kiasi gani? Na hiyo *horticulture* kiasi gani hatuwezi kuwa tunaongelea *avocado* hata haujui hauna *projection* kwamba utazalisha *avocado* kiasi gani. Chanzo cha pili cha fedha na bahati mbaya sana hakijajadiliwa watanzania naomba nizidi kuwasihii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Professor* muda tayari.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Nilikuwa naongelea mambo ya gesi *economy*, kutumia *methyl* kutumia *helium* nilitaka kuongea mambo ya *mining* kuingia kwenye madini mapya yanayotakiwa sasa hivi duniani *especially* hii gesi ya *helium* duniani sisi tukishindwa kuichimba wengine wameweka *contracts* wanataka kwenda kuichimba mwezini kwa hiyo ya kwetu tunaweza kuwa nayo tunajadiliana itabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilitaka kumalizia hayo huko tunakokwenda ni kutafuta hizi fedha za *climate fund* halafu vile vile nilitaka kumalizia kwa kusema kwamba Mpango huu kitu ambacho hatujakipata pale ni *yard stick* tutapimaje tumefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kusema ili tujue tumefanikiwa huu mpango utueleze tunapunguza umaskini kwa kiasi gani? *GDP per capita/inaongezeka* kwa kiasi gani? Halafu watu wangapi wamepata kazi? Viwanda vingapi tumevijenga? Yaani hizo naongea kwa ujumla lakini hapa *we need facts and figures* wakati tutakuja ku-*interrogate* mafanikio ya mpango huu halafu *gold reserve* inatia huruma mtu wa kwanza mwenye *gold reserve* duniani ni Marekani nilishangaa kuona hata Malawi ina *gold reserve* niki-*check* Tanzania *gold reserve* ni zero huu mpango unatuezaje ndani ya mwaka mmoja tukielekea 2025. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *Professor* ahsante sana.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kujenga viwanda vyetu vyta mbolea Mpango utueleze tunajenga pale Kilwa Mpango haujasema tunajenga na Mtwara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha hukuwepo hili tulisisitiza sana kwa kuhangaika kwetu kwa mbolea hivi lazima Mpango useme kwenye kuelekeea kwenye kujenga viwanda vyta mbolea tunafanyaje.

Mheshimiwa Mchungahela nilishakutaja jitahidi muda unakimbia haraka.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehma kwa kuniweka hai mpaka hivi leo na watu wa Lulindi wako wakinisikiliza kutaka kuwaongelea jambo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kama muongeaji aliyejita natamani kuishauri Serikali kama itawapendeza basi waweze kuchukua na hiki ninachokusudia kuwashauri kukiweka katika mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejielekeza sana kwenye kilimo kama vile ambavyo wenzangu waliotangulia lakini nimejielekeza katika muonekano mmoja kwamba kama tutahangaika vizuri tu na kilimo biashara bila shaka matatizo makubwa ya kiuchumi lakini pia ya ajira yanaweza yakawa yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee eneo moja eneo ambalo linahusu maeneo ninayoishi kule kwetu Mtwara kwa maana ya Lulindi korosho. Korosho ni kitu ambacho inailetea pato nchi hii pesa nyingi sana nashindwa kuelewa kigugumizi kiko wapi kwamba Serikali bado haiweki juhudhi ya kutosha kuhakikisha kwamba korosho zinapatikana kama vile ambavyo wao wanavyotarajia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusudio kwa mfano ya bajeti hii inayokaribia kuja Serikali ilijaribu kuelekeza kwamba korosho zipatikane takriban tani laki saba. Sasa tani laki saba ndugu zangu haziwezi kuja hivi hivi kwa maneno lazima tuwe tumejipanga vizuri na kwenye Mpango humu sioni wapi kwamba kuna kitu cha namna hii kitakachotuwezesha zao la korosho zipatikane tani laki saba, na kwa nini tani laki saba kwa sababu mpaka sasa hivi ambapo ni kiasi cha korosho kinapungua hakifiki hata tani laki tatu Serikali inapata pato la *dollar* takriban milioni 500 ambayo ni triliioni 1.3 kwa maana kama kweli lengo la tani 700,000 litafikiwa ina maana hapa

ni zaidi ya *dollar* milioni moja ni kiasi cha triliuni tatu na zaidi mnaweza mkaona kwa jinsi gani hapa suala la kupata pesa ya kuingiza kwenye uchumi ilivyokuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi hii *dollar* milioni 500 *plus* ambayo ni triliuni 1.3 mmeona athari yake kwenye uchumi nchi nzima kila mahali sasa hivi watu wanahangaika tunajenga kule tunajenga kule uchumi unaingia pale uchumi unaingia pale. Mnaweza mkaona hii *dollar* milioni moja ambayo Serikali ina *i-target* kupitia korosho tani laki saba inaweza ikawa ina athari kiasi gani? Sasa kwa hali hiyo hapa panahitajika kuwekeza kitu kidogo tu na chenyewe ni kitu kama hivi kwangu panahitajika kuingiza pembejeo za kutosha lakini mapema kabisa tena ambazo haziwezi zikazidi hata bilioni 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini halikadhalika kuwezesha jambo hilo pia liende vizuri tunahitaji pia ile barabara ya kutoka Mtwara kupitia Nanyamba kwenda Newala, kwenda Lulindi kwenda Masasi kwenda Nachingwea ambayo ni takriban kama bilioni 300 hivi. Hivi jamani hapa ukichukua hapo makadirio inaweza ikawa kama bilioni 400, bilioni 400 ukiwekeza ukapata takribani triliuni tatu hivyo jamani tunahitaji kitu gani? Shida ninayoona ninaona kwamba sisi tunafikiria sana vitu vikubwa mno baada ya kufikiria vitu vidogo vidogo ambavyo viko pale wala havihitaji kazi kubwa kuvitekeleza vikatupatia pesa. Kama tungekwenda kwa mtindo huu tukaenda kwenye eneo jingine la kilimo tukafikiria katika mtizamo huu bila shaka suala la kilimo kuwa uti wa mgongo lingekuwa lina maana sana na lenye tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kutoa ushauri huo nataka niipongeze Serikali kwa kazi yake kubwa ambayo imejaribu kuionyesha katika maeneo yale muhimu ambayo yanaweza pia kusaidia kwa namna moja au nyingine kuleta matokeo ya uchumi ya haraka. Maeneo mengi ambayo watu wengi wameshaanza kuyasema huko mwanzo kama vile uwekezaji wa reli ya *Standard Gauge* ninaiomba Serikali kusisitiza kwamba hili suala la *Standard*

Gauge katika eneo letu la Mtwara kutoka bandarini kwenda Mbamba Bay nakupitia katika maeneo yale mawili ya Mchuchuma na Liganga yaani tunasema kwenye matawi itawezesha sana bandari ya Mtwara kutumika na kuingiza uchumi mkubwa katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani sasa hivi tumetumia pale takriban bilioni 157 lakini ni kama zimelala tu bado hakujawa na kitu chochote cha maana cha kuifanya bandari ile ichangie kikamilifu kama vile tunavyotarajia na tunaweza tukaitumia bandari ile katika maeneo yote yale kule ya nchi za kusini kama vile *Mozambique* ambavyo kwa sasa hivi wanashida kwa sababu hawatumii bandari yao kutokana na hali yao ya matatizo ya migogoro yao lakini halikadhalika Malawi na Zambia wanaweza wakaitumia vizuri sana bandari ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali itumie nguvu nyingi sana kuhakikisha bandari ile inatumika kikamilifu, mambo haya yasiishie kwenye karatasi tu tumekuwa wepesi sana wa kuongea lakini kuthubutu kufanya maamuzi ya kutekeleza ni wagumu sana nashindwa kuelewa sababu za msingi sijui ni kwanini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hizi tunazokaa hapa mara nyingi sana wengi wanaona kama ni sehemu tu ya kuja kuigiza tunakaa tunachangia na kutoka tukishatoka hapa utekelezaji unakuwa mgumu sana unakuta kiongozi ambaye muhusika msimamizi wa Wizara fulani unavyojaribu kumfuata kutaka kufuata utekelezaji wa jambo fulani ambalo mmelizungumza pale halitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mfano nataka nizungumzie suala la mawasiliano kule kwangu. Bajeti hii iliyoko sasa hivi nilihakikishiwa kwamba takriban kata nane katika kata 16 maana yake kata 16 katika jimbo langu hazina mawasiliano kabisa ya simu wala redio. Kwa hiyo nilihakikishiwa takriban kata nane kwamba nitapewa mawasiliano na sababu kubwa ni nini? Kwamba lile Jimbo liko mpakani kabisa wa *Mozambique* mpaka ambao una

shida ndugu zangu na tujue kabisa mawasiliano ni njia pia mojawapo ya ulinzi ni ulinzi namba moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lakini mpaka sasa hivi hakuna chochote kinachofanyika kila ukiuliza wahusika hawana hata majibu yaani hata hawaelewi kitu gani wanaweza wakakwambia bwana kweli Mheshimiwa tulipanga hivyo lakini hili jambo halijatekelezwa kwa sababu gani sababu hazieleweki nashindwa kuelewa sasa hapa Bungeni tumekuja kuigiza au kweli tumekuja kufanya mambo kwa maana ya manufaa ya wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela mwaka haujaisha

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Sawa lakini angalau hata dalili zionekane

**MWENYEKITI:** Najua hasira yako lakini mwaka wa fedha bado haujaisha

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli naelewa lakini angalau dalili zionekane jambo *tendering* ifanyike uone kwamba kuna *tender* imefanyika hapa kwa ajili ya huu mradi hakuna, ushaona kuna sehemu nydingine kwa mfano kule kumejengwa mnara ule mnara ni mfupi yaani unakaribia yaani kama ufupi wangu ulivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unashindwa kuelewa hivi mnara...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela muda hauko upande wako.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ahsante naomba kuunga mkono hoja lakini nawaomba wahusika watekeleze haya yote ninayojaribu kuwakumbusha ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kundo kama yupo na Mheshimiwa Ashatu hii minara yenyeye urefu wa Mheshimiwa Mchungahela kwa kweli. Mheshimiwa *Engineer Chiwelesa* atafatiwa na Mheshimiwa atafatiwa na Mheshimiwa Tarimba na Mheshimiwa Esther Bulaya ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa MwenyeKITI, nashukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia nadhani niende moja kwa moja kwenye hoja na hasa tunapojadili mapendekezo haya ya mpango. Kwa sababu kauli mbinu yetu ya miaka mitano hii ya Mpango wa Maendeleo tunasema kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Nita-*base* kidogo kwenye viwanda zaidi sasa nimejaribu kupitia Mpango na Taarifa ya Kamati niwapongeze sana watu wa Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa MwenyeKITI, lakini pia kwa upande wangu nilikuwa nataka kujikita kwenye viwanda kama nilivyosema na hasa kwa kuangalia kwenye llani yetu ya chama tumesema kwamba tunataka kutengeneza ajira na ajira nydingi zaidi ziko vijijini na viwanda siku zote tumekuwa tunasema hapa kaulimbiu yetu ni kuhakikisha tunakuwa na viwanda vitakavyotumia mazao ya kilimo, mazao ya mifugo uvuvi kwenye madini na sehemu nydingine.

Mheshimiwa MwenyeKITI, lakini kwa sababu ya athari za UVIKO nimejaribu kuwa nafuatilia *trend* ya biashara inavyoenda kwenye dunia kwa sababu sisi tuko na wenzetu na tunafanya kazi na mataifa mengine duniani na hasa kwa sasa tunaona kwa sababu ya *effect* ya Amerika kujifungia na kufanya nini tumeona kwamba gharama kubwa za usafirishaji wa bidhaa nydingi duniani zimepanda kwa sababu *demand and supply* imekuwa kubwa sana hasa kwa USA.

Mheshimiwa MwenyeKITI, sasa tukirejea hata kwa upande wetu bidhaa nydingi ambazo tunatoa nje. Kwa mfano kusafirisha Kontena moja ya bidhaa ya 20 ft kutoka China, ilikuwa ni *dollar* 2100, *dollar* 2000 mpaka *dollar* 1900 as we speak juzi nadhani Jumatatu nilikuwa najaribu kufuatilia

baadhi ya sehemu sasa hivi kontena moja ya 20 ft imefika *dollar* 4900 kuitoa China kuileta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye 40 ft inaenda dola 9800 mpaka dola 10000. Sasa zote hizi zina *effect* kwenye upande mmoja hasa kwenye upande wa biashara hasa viwanda wanapokuwa wanaagiza malighafi za kuleta hapa zinakuja kuleta shida sana kwa sababu *cost of production* itaongezeka kwa sababu ya ile *transportation* ambayo ipo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiangalia kwenye upande wa kilimo tumekuwa na kelele nyingi sana za mbolea hapa wote mnaelewa lakini mbolea haikupanda kwa sababu ya Tanzania imepanda kwa sababu ya hii hali ambayo inaendelea na hasa usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa nawaza kitu kimoja wakati tunaongelea ule mpango wa kutengeneza eneo huru la biashara la Afrika niliongelea kwamba wenzetu ambao tupo nao kwenye sehemu moja hii ya biashara wapo tayari kwenye *GMO products*. *GMO products* ambazo zinatumika kwenye viwanda na baadhi ya sehemu nyingi hasa mazao kama pamba na vitu vingine wenzetu wameshatoka kwenye teknolojia ya kawaida huko wapo kwenye teknolojia ya mbele zaidi. Kwa sababu wote tunajua *advantage* ya zile *product*, leo tunasema kwamba tunaingia kwenye ukame tuna- *expect* mvua zinaweza zikawa zimebungua, lakini unapokuwa kwenye upungufu wa mvua ukawa na *products* zile za *GMO* mbegu zile kinachosaidia ni nini, kwamba ile mbegu inaweza ikavumilia ukame, lakini mbegu ile haihitaji mbolea nyingi kama leo ambavyo tunahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nasema kwamba katika Mpango Serikali ijaribu kuangalia pia kwa sababu tunaongelea jambo la 2022 kwenda 2023 tuone hii hali ya sasa hivi kwenye bajeti ya sasa hivi tumeshaiaachaa, lakini tunapoenda mbele tujaribu kuona kama Serikali *can we adopt this technology?* Maana hii teknolojia itatusaidia

kwanza kuwa *competitive* na pia kuweza kuhimili hali ya hewa kama hii ambayo inabadilika badilika kwa sababu hatujui baada ya hapa kitakachotokea nini. Kwa hiyo, nilomba hili jambo tuliangalie ili tusiathiri viwanda vyetu hivi ambavyo vina-deal/na mazao ya kilimo na ambavyo vimeajiri watu wengi na watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mpango kuna jambo moja nilikuwa naliangalia tumewekeza fedha nyingi sana kwenye miradi mingi ambayo inaendelea. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa pesa ambayo imepatikana kuna pesa nyingi zimeenda kwenye miradi ya maji na nyingine zinaendelea kutoka kwenye bajeti yetu, lakini nimekuwa najaribu kuangalia *trend* kila ukiangalia milioni 500, milioni 400, milioni 500, milioni 400 fedha ambazo zinapelekwa kwenye miradi ya maji, nikawa najiuliza katika *best engineering practice* hakuna kitu ambacho unakifanya bila kuwa na *plan* ya kuki- *maintain* baada ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwenye upande wa barabara tumekuwa tunatenga pesa kupitia *road fund* lami hizi hizi ambazo tumezijenga kwa hela nyingi bado ipo pesa ya kuendelea kuzi- *maintain* nikajiuliza *what is the plan* hasa kuhusu miradi ya maji mikubwa ambayo tumeifanya kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu unajenga kituo cha afya cha milioni 250 yupo Daktari pale na wapo watu wanaendelea kuki-*maintain* kile kituo. Ukiengena madarasa Walimu wapo pale wanaendelea kuya-*maintain*, lakini miradi ya maji ambayo inatumia pesa nyingi za Watanzania wote ni mashahidi hakuna watu ambao ni *technical or qualified people* ambao wana *technical knowledge* wanaosimamia ile miradi ya maji. Zaidi ya kuunda ma-group tunasema ma-group ya watumiaji wa maji, vyama vyta watumiaji wa maji unakuta pale ni Mwenyekiti wa Kijiji na Mtendaji wa Kijiji ndiyo wanaosimamia, *technically* hawajui kile kitu, kinachokuja kujitokeza ni nini miradi hii itakuja kututoa jasho baada ya miaka mitano baada ya miaka sita miradi itakufa tutaanza kuwekeza pesa nyingine tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tumejenga vyuo vingisana vya VETA kila anayesimama hapa anaomba chuo cha VETA kwenye Jimbo lake, kila anayesimama anaomba chuo cha VETA kwenye Jimbo lake tunao vijana wale, wale vijana gharama yao siyo kubwa, wanaweza wakafanya kazi katika mazingira yale ya chini kwa sababu ndiyo kada ya chini kabisa kwenye ufundi ambayo inaweza ikafanya zile kazi.

Sasa tuombe Serikali mjikite kwenye kufikiria ajira za vijana hawa ambao tunawatengeneza kupitia vyuo vyetu vya VETA tuwapeleke vijiji ni wakakae kule wao ndiyo wawe mafundi wa ngazi ya chini wa kusaidia miradi ile maji ambao tunaweka hela nyingi wailinde na waweze kui-*maintain*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimezunguka kwenye Jimbo langu kuna baadhi ya sehemu vilichimbwa visima, pesa nyingi imetumika baada ya miaka mitatu kisima kimekauka. Lakini kama una mtu ambaye *is a technical qualified person* yule mtu ange-*inspect* kwamba hapa kuna shida akajaribu kujulisha hata kama maji yanapungua usiunguze hata ile pampu vile visima havifanyiwi *service*, pampu ile ukiichimbia kule chini mpaka siku ikiharibika ndiyo unakuja kuangalia baada ya muda inaharibika na ina-*cost* hela nyingi. Pampu ambayo inakuja ku-*cost* shilingi milioni mbili, milioni tatu, milioni nne, tungeweza kui-*maintain* kwa shilingi laki moja, laki mbili tukaitoa tukaipeleka sehemu tukasafisha tukairudisha. Lakini yote hiyo ni lazima kuwe na a *best plan* ya kuhakikisha vitu hivi tunavyovifanya pesa tunazowekeza ziwe na watu wa kuzifuatilia na kuzisimamia na by the way ni sehemu ya kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi yangu yalikuwa hayo nilitaka tuone mpango mzuri kwenye hasa upande wa maji wakusimamia hii miradi mizuri ambayo tunaifanya baadae miradi hii isije ikatutokea puani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ezra Chiwelesa. Mheshimiwa Tarimba Abbas atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana na mimi nipate nafasi ya kuchangia katika Mapendekezo haya ya mpango ambayo yameletwa na mwananchi Mheshimiwa Mwigulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kuunga mkono hatua iliyofikiwa hadi sasa naunga mkono mapendekezo haya. Vilevile niipongeze Kamati ya Bajeti tulifanya kazi nzuri sana ambayo hata Waheshimiwa Wabunge humu wameikubali na kwa hali hiyo ningeomba Mheshimiwa Waziri ayachukulie kwa uzito stahiki kabisa mapendekezo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia katika vile vipaumbele na ningeanza na maendeleo ya watu. Kwenye Jimbo langu la Kinondoni sisi hatulimi, hatuna bahari hatuvui, sisi ni watu wenye shughuli ndogo ndogo na tunawamachinga wengi sana na mimi sitaki nizungumzie eneo la wamachinga kama liliyoyozungumziwa ile timua timua, upangaji, hapana mimi nakubaliana na Serikali hatua walizochukua. Nataka niliangalie eneo hili hasa pale ninapolinganisha na mpango kwamba mpango wenyewe huu haujabainisha hali ya umaskini kiwazi kabisa na jinsi gani mpango unakwenda kuhangaika na taratibu za kuondoa umaskini, hii inaunganisha na wamachinga kwa sababu hili kundi limejitokeza mionganoni mwetu na ni kundi ambalo yawezekana kabisa na naamini Serikali haijawahi kufanya utafiti kulijua kundi la wamachinga lina nguvu kiasi gani katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana tunawaona tu barabarani wakitembea ama wakijenga mabanda yale ya plastiki, lakini nataka nikwambie kwamba hawa watu kwanza wamewaondolea mzigo Serikali ya kuwatafutia kazi ni watu ambao wameamua kujajiri wao wenyewe, lakini kama itafanyika tafiti ili kuonekana kwamba hawa wamachinga

ni kwa jinsi gani wana-support baadhi ya viwanda vidogo vidogo nchini, baadhi ya wakulima wanaouza matikiti utakuta kwamba sasa hivi biashara imeshuka kidogo kwa sababu hawajakaa vizuri zaidi maana yake nini maana yake wanamkono katika uchumi, wana mkono katika biashara katika Taifa letu kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri mpango huu ujaribu kuunda utaratibu wa kwenda kufanya utafiti wa kina *very independent* ili kuliangalia hili kundi hili la wamachinga ni kundi la aina gani lina nguvu kiasi gani katika uchumi ili kama ikiwezekana waliingize katika utaratibu wa kulipia hata kodi wajulikane wanafanya shughuli gani na wapo wapi na akina nani ili nao waweze kuchangia katika Pato la Taifa la nchi yetu, lakini vilevile katika kodi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nizungumzie ukurasa 25 na 26 za Mheshimiwa Waziri wakati alivyokuwa akitoa hotuba yake juu ya kuwasilisha kwa mapendekezo haya na hii inagusa vipaumbele vifuatavyo:

Kuchochaea uchumi shindani, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, utoaji huduma na kukuza biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote haya ukiyaangalia yanagusa mwenendo wa kibashara na hasa *private sector* na kwa kuwa *private sector* ni tegemeo kubwa sana katika kodi za Taifa hili kiasi kwamba zaidi ya trillion 22 zinatarajiwa kutoka kwao. Kwa hali hii nilikuwa naangalia ni kwa jinsi gani basi hivi vipaumbele vitatu vinaweza vikaleta mafanikio bila ya kuangalia ni kwa jinsi gani *private sector* inakwenda kusaidiwa. Hebu tuangalie nijaribu kukumbusha huko nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa *road map for improvement of business and investment climate* baadaye ikaja *big results now* sasa tuna *blue print*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zote hizi ni *documents* ambazo zilikuwa zinajaribu kutatua na kuleta hali bora ya uendeshaji wa biashara katika Taifa hili. Nimeangalia katika

huu mpango suaona vizuri ni kwa kiasi gani *blue print* imefyonza katika Mpango huu suaona yaani ikaja wazi wazi kabisa, kwa sababu *blue print* yenye ni majibu ya matatizo tuliyonayo katika kuifanya *private sector* ikawa *vibrant* na ikaendelea kuchangia kiasi kikubwa, trillioni 22, kwa Tanzania ya leo ilivyo ni fedha ndogo mimi ninaamini kabisa, laiti kama tungeshika *certain buttonstukaminya* vitufe ambayo pengine hatuvijui au tunavijua kupitia kwenye *blue print* utakuta kwamba uchumi wa Tanzania utafunguka hasa katika kipindi sasa Tanzania tumejenga imani huko nje, tumejenga imani ndani, kwamba sasa Tanzania unaweza ukafanya biashara vizuri. Ingawa Tanzania kufanya biashara ni kugumu kidogo kwa sababu hata kwenye *indexile* ya *easier of doing business* bado hatujafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba mpango huu uje na hatua za kutunasua kule kufanya vibaya katika ufanyaji wa biashara tuondoke katika ile nafasi ya 141, tupande juu ili tuweze kuwavutia watu wengi sana. Kutohana ninaomba mpango uje kiwaziwazi uonyeshe ni kwa jinsi gani tutakwenda kuondoa urasimu wa ufanyaji na mifumo ya usimamizi wa biashara katika nchi yetu, *regulator reforms* lazima zifanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tusaidie Mpango uweze kuja wazi wazi utuondolee gharama nzito za kufanya biashara, leo hii ukifanya biashara *regulators* walio wengi watakufta, wewe ukisoma ile sheria ya *OSHA* peke yake kuna kodi ya kucheka, kuna kodi ya kuchukia yaani ni hatari ni hatari kabisa, ukitoka hapo ukienda kwenye *fire* nao wana mambo yao yaani ni balaa balaa, hebu tufanye ufanyaji wa biashara katika nchi hii usiwe na gharama kubwa ili tuweze kuwavutia watu wetu wengi wafanye biashara, Watanzania na hata wale wa nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la *reduction...*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu sana Kaka yangu Tarimba Mheshimiwa Mbunge, lakini naomba tu tuwe *realistic* katika sheria zote ambazo zimetungwa na sheria hii, hamna tozo yoyote iliyowekwa na Serikali ambayo inamtoza mtu kwa kucheka, inamtoza mtu kwa kukasirika ama kuchukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tukiacha hivi *records* zetu zitakuwa zimerekodi kitu ambacho hakina uhalisia kwa hiyo nilikuwa naomba nimpe taarifa kodi hizo ndani ya Serikali hatuna. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Unajua Yanga hawa wana shida sana, Mheshimiwa Tarimba unapokea taarifa. (*Kicheko*)

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipokea. Unajua alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Michezo, tulikuwa pamoja sina haja ya kushinda naye ni kweli hakuna kodi hiyo lakini inaonesha vile vikodi vidogo vidogo vya kuangalia ngoja kuna kodi ya *vision* sijui kufanya nini wanakupima macho, kama kampuni kama mtu, kuna vikodi vingi vingi hata Mheshimiwa akitaka nimkumbushe, nimuoneshe, nitamuonesha, lakini zipo kodi zinazoudhi ninachojaribu kusema ni kodi zinavyoudhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa nione huu mpango unakuja na ile dhana ya kuongeza *confidence* kwa *investors* wa ndani na wa nje, watu waliumiaumia hapa katikati hivyo, ningeomba mpango huu uweze ukasaidia.

Kwa hali hiyo, kwa kuwa nimeyazungumza yale ambayo nilikuwa nataka kuzungumza niseme naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kutumia muda vizuri. Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikikupendeza Bunge lako Tukufu liweze kuagiza Serikali ituletee taarifa sahihi ya miradi yote ya kimkakati inaendeleaje. Kwa sababu unakuta miradi mingi *either* tunajenga kwa pesa zetu mwenyewe au kwa mikopo ambayo mwisho wa siku Watanzania ndiyo wanakuja kulipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wewe unajua kwenye miradi mingi ya barabara Mkandarasi anapochelewa kukamilisha mradi, *I mean* Serikali inapochelewa kumlipa Mkandarasi na kusababisha mradi kuchelewa unakuta Serikali inalipa mabilioni ya shilingi kwa sababu mradi umechelewa kukamilika. Sasa nilikuwa nataka njue *statusya* mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ikoje, tuliambiwa ngonjera ngonjera nydingi tu, lakini kwa habari nilizonazo sasa hivi mradi uko asilimia 45 na ulipaswa mpaka sasa hivi uwe asilimia 99 ambayo leo ni siku ya 834 mradi unapaswa kukamilika Juni 14, 2021. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda kwenye vipengele vingine unakuta kukamilika kwa ujenzi wa tuta kwenye bwawa ni asilimia 43 ambayo leo ilitakiwa iwe asilimia 88, kukamilika njia ya kupokelea maji kwenye mitambo sasa hivi ipo asilimia 57, wakati ilipaswa kuwa asilimia 94, kituo cha kupokea na kusafirisha umeme kazi mpaka sasa hivi ni asilimia 50 ilipaswa kuwa asilima 99, kuna mwingine kuna upande mwingine asilimia 29 ilitakiwa kuwa asilimia 98, hii ni kinyume na mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuambiwe na kuna taarifa mradi huu ukaenda mbele zaidi kuliko mkataba, lazima tuambiwe kwa kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kinyume na mkataba Serikali yetu itamtoza Mkandarasi kiasi

gani kwa siku kwa sababu hizi pesa ni za Watanzania na mkopo...

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya ni taarifa unapewa.

## TAARIFA

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa msemaji anayeongea ningependa kumpa taarifa kwamba mradi huu ulichelewa kwa sababu nyangi mbalimbali, lakini moja ya sababu ilikuwa ni sababu za kimazingira ambazo zilipelekea kuwekana sawa na wadau wetu mbalimbali wa mazingira ili mradi ule uweze kutekelezwa katika eneo lile, lakini sababu ya pili ni uwepo wa *COVID-19* ambayo ilichelewesha baadhi ya mitambo kuingizwa nchini kutokana na viwanda vingi duniani kufungwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake.

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa Ester Bulaya. Sasa Mheshimiwa Ester Bulaya unapokea taarifa hiyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kuchelewa yote yalikuwa ndani ya miezi sita ulitakiwa ukamilike kwa miezi 36, umeenda 44 na ndiyo mpaka hiyo Juni 14, 2022.

Kwa hiyo, walizingatia huku na *deadline* iko pale pale kwa hiyo tunachotaka tujue tutamtoza kiasi gani kwa kuchelewesha huu mradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye kazi yenye, wewe unajua tangu niingie kwenye Bunge hili kila taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali imekuwa ikielezea hali

mbaya ya mifuko yetu kujidoresha, kuweza kulipa mafao, lakini hii yote ni kutokana na Serikali kukopa bila kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesoma ukurasa wa 29 wa Mheshimiwa Waziri amesema atalipa Trilioni Mbili kwa *non-cash bond*, nikukumbushe Kamati yako ya *PAC* baada ya Serikali huwa inasema hatudaiwi kiasi hiki, hatudaiwi kiasi hiki, Kamati yako ya *PAC Report* ya 2014 iliunda kikosi kazi kuchunguza deni na ikaleta ripoti tarehe 10 mwezi wa Kwanza 2015 ikaonesha deni la 1999 ni Trilioni 7.1 mwaka 2014. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa mbwembwe zote baada ya miaka 22 bila aibu fedha za watumishi tunaanza kupewa Trilioni 22. Sasa nikija kwenye deni kuu la mifuko mnalipa Trilioni Mbili, nikija kwenye deni kuu la mifuko ambayo ni Trilioni 19 mnahitaji miaka mingapi mkamilishe kulipa, deni la Mifuko Hifadhi ya Jamii ambayo huku ndiyo kuna hatma ya watumishi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu hivi kwanini tukikopa mikopo ya kibashara nje mnakimbilia kulipa haraka kwa sababu mnawaogopa wale mabeberu, lakini pesa za wazawa wanazokatwa kwa ajili ya akiba baada ya maisha yao ya kulitumikia Taifa lao kwa muda mrefu kwenye 1999 tu baada ya miaka 22 mnatoa trillioni mbili mnadaiwa trillioni saba, bado huku kwenye Trilioni 19 kwa deni la ujumla sijui mtalipa kiasi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie, kwa taarifa nilizonazo, maana hapa tulikuwa tunaambiwa biashara ya *actuarial*, najua ya mwisho iliyofanyika 2016 ndiyo tumeambiwa Serikali inadaiwa shilingi trillioni 19. Inawezekana mambo hapa yameongezeka zaidi ndiyo maana mifuko inashindwa kujidoresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa taarifa nilizonazo, *consultant* amemaliza kazi tangu mwezi wa Tano, imebaki Serikali kutoa maoni, wanaficha nini? Wanaogopa kusema mifuko ina hali mbaya au deni limeongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Juni, 2020 inaonesha Mfuko wa *PSSSF* ilikusanya ili michango shilingi triliioni 1.3. Ilikuwa inatakiwa kuwalipa wastaafu shilingi triliioni 1.5, yaani *cash* walikuwa nayo kidogo kwa mahitaji ya kuwalipa wastaafu kwenye Taifa letu. Walichofanya, walienda kwenye *government Security* wakachukua shilingi bilioni 300, wakaongezea shilingi bilioni 190 wakalipa wastaafu na nyingine ndiyo wakaenda kuwekeza. Aibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Pokea taarifa Mheshimiwa Ester Bulaya.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tu nimwambie Mheshimiwa Ester Bulaya, kama Serikali iliweza kupata fedha na kuwalipa wastaafu, nadhani angepasa kupongeza kwamba kumbe Serikali ilipata fedha na ikawalipa wastaafu. Hilo ni suala la kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Ester ni kwamba Serikali wala haina nia ya kuficha hiyo ripoti na siyo kweli kwamba Serikali inaficha hiyo ripoti ambayo Mtathmini Mkuu ameshamaliza kufanya utathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti inapokuwa tayari ina utaratibu wake katika kuiweka wazi. Naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu, ripoti hii ni mali ya wafanyakazi, mali ya waajiri, mali ya Serikali na Watanzania wote kwa ujumla, wala siyo ripoti ya Serikali. Sasa kwa taarifa yake, baada ya mtathmini kumaliza hiyo kazi, sasa hivi ndiyo tuko kwenye

vikao vya utatu; wafanyakazi, waajiri na Serikali, ili kuitathmini hiyo ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu kumpa taarifa kwamba hayo maneno siyo kweli Mheshimiwa Ester Bulaya, kwamba Serikali inaficha hiyo ripoti. Nadhani ni lazima tuwe tunaweka mambo wazi na tuyazungumze kwa msingi wake. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa Mheshimiwa Ester Bulaya?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kwa sababu hili goma limeisha siku nyingi, huu ni mwezi wa sita wanakaa na taarifa yao, wanaficha nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa kwamba mfuko uko hohe hahe, lakini mbali na yote na kutokulipa madeni, wanaendelea kuwapa kuwapa mizigo ya kuendelea kuwekeza kwenye viwanda 35. Wakati hawalipi madeni, bado wanawatwika mzigo, wenye we wanachokusanya wanakosa, leo mifuko imetoa shilingi bilioni 339 kwenda kuwekeza kwenye viwanda 12, wakati huku mifuko yenye we inakosa fedha ya kwenda kuwalipa watumishi wa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa uliongelea kitu kizuri tu, ukaelezea ni namna gani Sheria ya Kikokotoo kuwa mbovu mpaka ongezeko la watu wanaostaifu kwa hiari limeongezeka. Nikaenda kutafuta; sasa nikwambie, baada ya Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli kutangaza kusitisha kile kikokotoo cha mwanzo na ile sheria kupita, ongezeko la watu wa fao la kujitoa limeongezeka na ongezeko la watumishi wanaostaifu kwa hiari imeongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kikokotoo kipyा, watu waliokuwa wakistaifu kwa hiari ni 2,562; baada ya kikokotoo kipyा watu 4,730 wa fao la kujitoa walikuwa wamelipwa shilingi bilioni 21. Baada ya sheria, wamelipwa

shilingi bilioni 53. Wastaafu kwa hiari kabla ya kikokotoo walilipwa shilingi bilioni 158; baada ya kikokotoo, wamelipwa shilingi bilioni 352. Walikuwa wanawahi wachukue chao mapema kwa sababu wanajua Serikali hamtabiriki, hawajui mtakuja na hatima gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja kubwa sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja kubwa sana ya kulinda maslahi ya watumishi wa Taifa hili. Tuachenii bla bla, tutimize wajibu wetu. Hakuna mgomo mbaya kama wa watumishi kwa sababu hawaoni wala hawezi kujisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Mtemvu, utafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Mapendelekezo ya Mpango wa mwaka 2022/2023. Nitajielekeza katika maeneo mawili tu muda ukinifaa sana; eneo la mapato katika sehemu ya mawasiliano na eneo lingine ni mwenendo wa riba hapa nchini na hasa eneo ambalo halijazungumzwa na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya; sehemu kubwa wamesema wengine, lakini kwa jinsi anavyotuheshimisha kwenye majimbo yetu.

Pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana kwa usikivu kama ambavyo nimeendelea kusema, Waziri mwenye

dhamana ya Wizara hii, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi nzuri ya usikivu anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakushukuru sana Mheshimiwa Spik ana Naibu Spika. Kwa kweli sisi tunaendelea kujifunza sana kila siku na kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofanywa na Kamati ya bajeti mimi nikiwa ni Mjumbe wa Kamati inayoongozwa na kaka yetu Mheshimiwa Daniel Sillo na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Omari Kigua, tunaamini Waheshimiwa Wabunge wameiona na wameipongeza, nasi tumefarijika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu, katika eneo hili la makampuni ya simu, kuna changamoto sana. Tunakubali sana kwamba eneo hili la *mobile sectors* limechangia sehemu kubwa sana kwenye nchi yetu. Kwa uchache sana, katika kipindi cha miaka miwili wamechangia takribani Dola za Kimarekani milioni 441, takribani shilingi trillioni moja za Kitanzania. Vilevile wana mchango kwenye *GDP* takribani asilimia 5.2 na ziada ya mchango wao kwenye ajira kwenye sekta hii ni takribani watu 1,500,000. Hii ni karibu asilimia 2.6 ya idadi ya watu wetu wote wa takribani watu milioni 60 hadi 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo hapa ambalo nataka kusema na kubwa ni eneo linaloonekana kuna upotevu mkubwa sana wa mapato katika eneo la mawasiliano. Liko jambo ambalo ukiliangalia kwenye takwimu za miaka karibu nane, tisa; mwaka 2013 hao wenzetu kwenye sekta hii waliwahi ku-*declare*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *average revenue per user*; kiwango cha mtu moja moja katika kipato anachokipata kwa haya makampuni; kwa mtu mmoja kwenye idadi ya watu wote, ilikuwa ni takribani dola 5.5, kama 12,000 hivi. Katika kipindi hiki cha miaka miwili iliyopita, wame-*declare* tena punguzo takribani dola 2.3, yaani kama shilingi 5,000 au shilingi 6,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali linakuja hapa. Huo wakati ambao wanasema hayo kwa mtu *average revenue per user* ni 12,000, tulikuwa hatuna *data* wala tulikuwa hatuna mambo ya kuhamisha miamala ya kifedha. Leo tunajua wote idadi ya watu ni zaidi ya asilimia takribani milioni 60, 64. Nao wanasema takribani watu asilimia 42 ya *population* nzima wameji-*engage* kwenye *mobile service*. Sasa unaiona siyo chini ya milioni 30, lakini punguzo hili linatoka wapi kama leo tume-*engage* kwenye *data*, kwenye *mobile transfer* (miamala ya fedha)? Iko shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimejitembeza kwenye nchi kadhaa kwenye jambo hili, nikakuta takribani nchi saba zilitutuka juu ya wizi mkubwa au upotefu wa mapato makubwa katika eneo hili, wakafanya *Forensic Audit*. Nchi kadhaa, mimi nitataja chache sana; baada ya kufanya *Forensic Audit* wamekuta upotefu mkubwa sana wa mabilioni ya namba. Hizi ni nchi kama Ghana, Kenya, Uganda, Rwanda, Malawi na nyine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwepesi, nchi nydingi zimeanza kufanya ukaguzi huu kuanzia mwaka 2003. Ndugu zetu Kenya na Uganda walifanya mwaka 2003. Uganda walifanya mwaka 2009. Hawa walikuta upotefu wa zaidi ya asilimia 300, *increase*; na waliweza kurudishiwa fedha zilizopotea kwa Kenya tu ni zaidi ya shilingi bilioni 600; kwa Uganda ni zaidi ya shilingi bilioni 600 na yenyewe.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwa haraka, Ghana ambao juzi, mwezi wa Nane mwaka 202,1 wamefanya *Forensic Audit* kwenye *data* na *mobile money transfer* na wamemaliza juzi tu, wamekuta upotefu wa zaidi ya asilimia 300; Dola za Kimarekani milioni 418, hizi ni takribani shilingi triliuni moja za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, sisi huwa tunachelewa sana. Leo Serikali ikaone inayo sababu ya kwenda kufanya *Forensic Audit* kwenye miamala hii kwenye haya makampuni yetu ya simu. Ni ukweli, wanafanya kati ya miezi mitatu hadi sita, wala siyo muda mrefu, watakuja

kutuambia kwenye Bunge lako hapa ni kiasi gani tumeokoa kwenye *declaration* zao za *revenue* kila mwaka? Ni kiasi kikubwa sana tunapoteza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika chache kama nitaweza, niseme kidogo juu ya eneo hili la mwenendo wa riba. Maeneo mengi wamesema *BoT* imefanya kazi nzuri, Serikali imeingiza shilingi trilioni moja ili kupunguza zile riba na mambo mengine. Nataka kusema kuna wizi mkubwa hapa, nitumie tu hiyo lugha. Katika eneo hili wananchi wanaumizwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu viwili vinaitwa: moja, *credit life insurance* na nyingine ni *takeover loans penalties*. Niseme kwa haraka hili la kwanza, tutagundua Waheshimiwa Wabunge wote, tukichukua mikopo tunakatwa *credit life insurance at once*. Mikopo utachukua wa miaka mitano, lakini tunakatwa bima ya miaka mitano mara moja. Huu ni wizi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikilisema hili, linaenda sambamba na suala la *takeover loans penalties*. Hawa Waheshimiwa Wabunge hapa wamechukua mikopo inawezekana kwa asilimia 13 au 14, lakini kuna benki nyingine zinatoa mikopo kwa asilimia 12. Katikati ya mwaka, katika mikopo wangu wa miaka mitano unapoamua kuuhamisha, unau-*takeover*, unau-*liquidate* pale, unauhamisha kwenye benki nyingine, kwa sababu ya faida ya *difference of interest rate*. Wanaku-*charge* asilimia tatu hadi tano bila wewe kujua. Hii ni kitu kibaya sana. Maana yake *customer* wanaumizwa na haki yao ya msingi ya kuhamisha mikopo wao kwa faida ya *interest rate* walizoziona kwingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwenye eneo hili, sana ni mambo mawili; moja, atoe *clear directive* kwamba hakuna *penalty* ambayo inastahili kulipwa wakati mteja anahamisha mikopo wake. Hili muhimu sana, itawasaidia Watumishi wa Umma, itawasaidi Waheshimiwa Wabunge na wengine na wengine wengi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, hizi *insurance*, kama nimechukua mkopo unanikata miaka mitano kwa mara moja, leo nauhamisha mwaka wa pili, napeleka kwenye benki nyininge, naenda kukatwa *insurance* tena, wakati wewe umechukua yote ya miaka mitano. Kwa nini isifanywe kwa *pro-rata*; miaka yako miwili chukua, nikihami miaka mitatu kwenda benki nyininge, kule nikakatwe makato yale yale ambayo nilikuwa nimeshayapeleka kwenye benki ya awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Huo ulikuwa mchango wangu wa leo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia wakati huu wa Mpango. Nimesoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri, pia nimesoma na taarifa ya Kamati ya Bajeti, nami niungane nao na niunge mkono taarifa hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba kukazia baadhi ya maeneo ambayo nilitamani sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* atueleze wanafikiria kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Kamati ya Bajeti, wamesema wazi kwamba pesa ya Mfuko wa Jimbo kwa zaidi ya miaka sita, saba sasa hivi haijaongezwa. Kwa hiyo, fedha tuliyokuwa tunaipata mwaka 2015/2016 ndiyo hiyo hiyo inayopatikana sasa hivi wakati *inflation* imekuwa inaongezeka kila mwaka. Kwa hiyo, tunaomba ifanyiwe *adjustment* ili fedha hii iweze kuwa na manufaa yaliyokusudiwa pale mwanzoni. /

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetolea tu mfano wa Jimbo la Ndanda, tunapokea shilingi milioni 42, ambayo ni wastani wa shilingi milioni 2.6 kila kila Kijiji. Sasa katika vijiji 77 unataka upeleke shilingi milioni 42 ili wale watu uweze

kuwagusa wote kwa ajili ya miradi, unaweza ukachagua miradi michache, lakini wengine wanaweza wasielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumeona, na ninaishukuru sana Serikali, imetoa fedha nyngi kwa ajili ya kwenda kujenga madarasa. Naishauri tena Serikali kwamba madarasa haya yanayokwenda kujengwa takribani 15,000 yaende sambamba na ajira zitakazotolewa. Kwa sababu kama unajenga madarasa 15,000, tafsiri yake unakwenda kuongeza wanafunzi kwenye shule zetu, unakwenda kuongeza na madarasa, lakini kama idadi ya walimu na watumishi itabaki pale pale, basi itakuwa ni tatizo. Hilo ni sawa sawa na jambo ambalo lipo kwenye vituo nya afya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuishauri pia Serikali ni kuhusiana na mitambo pamoja na magari yaliyozagaa nchi nzima, kwenye Halmashauri zetu, kwenye hospitali zetu pamoja na kwenye Serikali Kuu. Magari haya yanazidi kuoza na mitambo hii inazidi kuoza. Kama Serikali wana nia njema, ni bora wakauza mapema kwa sababu tayari walishafanya tathmini ya vitu hivi, kwa hiyo, *TR* atoe kibali mapema yauzwe japo ipatikane fedha kidogo, lakini pia itapunguza kwenye *asset* badala ya kuonesha Serikali ina magari mengi, ina mitambo mingi ambayo ipo kwenye vitabu vyake, haitumiki, yanabaki kama makuukuu na mengine yanakuwa sasa kama vijumba nya majambazi huko kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, niwaombe sana waiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, mimi naomba, nawe ni Mwenyekiti wetu, niliona siku moja picha yako umeanza kilimo cha korosho. Sasa utusaidie sana wakulima wa korosho tumekuwa kwenye adha kwa muda mrefu sana kwenye suala la *Export Levy*. Imefikia mwaka huu hapa ninapoongea nawe mkulima anakatwa takribani shilingi 979/=? Katika hii shilingi 979/= mgawanyo wake uko hivi: *Export Levy* peke yake inakatwa shilingi 499/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa sheria hii iletwe ndani ya Bunge na Mheshimiwa Waziri wa Fedha akae

na Wizari ya Kilimo wajaribu kuipitia hii sheria na walete mapendekezo ili sheria hii ibadilishwe, kwa sababu imekuwa inakandamiza sana wakulima. Kwa mfano, hiyo *Export Levy* ni shilingi 499 kwa bei ya mnada huu uliopita. Kwa hiyo, mkulima jumla anakatwa *almost* shilingi 979. Kati ya hizi, *direct deduction* ni shilingi 260 au shilingi 270; na kiasi chote kinachobaki huwa anakatwa *indirect* kwa kupitia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria hii ya *SDF* ambayo ilitungwa hapo nyuma kwa ajili ya kutaka kusaidia wakulima, imekuwa kama ni marudio kwa sababu ukiangalia kuna *direct deduction* ambayo ni pesa ya ushirika shilingi 100, pesa ya *CBT* shilingi 25, pesa ya *TARI* shilingi 25, pesa ya Halmashauri shilingi 56, lakini pia kuna pesa ya mchango wa elimu shilingi 30, pesa ya Halmashauri ndiyo sawa na mchango wa elimu, *almost*, lakini pia ukilinganisha na usafirishaji ni shilingi 50. *So in total*, unapata karibia shilingi 979.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tuwashauri hawa ndugu zetu, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha wajaribu kuipitia hii sheria na wailete hapa ndani Bungeni tuibadilishe. Korosho siyo zao la mkoa mmoja au mikoa miwili, mitatu; korosho limekuwa zao la Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la madeni. Kuna madeni mengi sana ya ndani, mengine yanayotokana na mazao ya kilimo, lakini mengine yametokana na maamuzi ya Serikali. Kwa mfano, ukienda kwenye korosho, madeni ya Bodi pamoja na Vyama vya Ushirika ni takribani shilingi bilioni 40. Tunaomba sana madeni haya yahamishiwe Hazina kwa sababu Bodi haiwezi kuyalipa na vyama vile vya msingi kule kwetu hawawezi kuyalipa, yamekuwa mzigo kwao, yanachafua vitabu vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Bodi ya Pamba, wanadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 60. Pia ni sawa sawa ukienda kwenye tumbaku. Kwa hiyo, tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri aridhie madeni haya yachukuliwe na Hazina yaweze kulipwa kwa sababu ni mitaji ya watu

waliokuwa wanafanya biashara na Serikali na maeneo mengine kutohama na maelekezo ya Serikali. Kwa hiyo, Wakandarasi wa ndani wanao-supply vitu mbalimbali kwenye huduma za kilimo, kwenye huduma za mashule kwa mfano, Shule ya Sekondari Ndanda, Shule ya Sekondari Chidya watu walipeleka pale chakula, sukari, unga kwa ajili ya wale Watoto na Halmashauri zetu zinaelemewa, hawawezi kulipa tena. Tunaomba Hazina wachukue haya madeni na wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema hapo mwanzoni, kuna miradi mikubwa sana ya kimkakati iliyoelekezwa kwa upande wa kusini. Kwa mfano reli ya Kusini hatujui mpaka sasa wamefikia hatua gani na nini kinakwenda kufanyika? Tuna barabara zetu za kiuchumi ambayo ni barabara inayoanza Mtwara kufika Newala - Masasi - Nachingwea kwenda Lwale kuja kutokea Lupillo kuja kutokea mpaka Morogoro kwa maana ya kutaka kufungua ukanda huu wa kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutamshukuru sana Mheshimiwa Rais, endapo wazi kabisa ataamua sasa kufanya kazi na hii barabara, kwa sababu pia ndiyo barabara inayotokea Songea kupitia Namtumbo kwa sababu tunatamani sisi wakati fulani siyo lazima tufike Dar es Salaam tunapoamua kuja huko, lakini pia ni sehemu ya kufungua ukanda huu wa kusini, tusiwe na barabara moja tu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utakumbuka kulikuwa na suala hapa la Mtwara *Corridor* ambayo ilikuwa ni makusudi mazima ya kwenda kuboresha Bandari ya Mtwara. Katika mikakati ya sasa inayotajwa, naona kama habari za Mtwara *Corridor* zimesahaulika kabisa. Sijasikia ikiwa inatajwa karibuni ndani ya Bunge kwa sababu sisi Wabunge tunaongea kidogo, lakini hata Wizara nayo hajjawahi kutuambia habari hii na sijaiona huko.

Kwa hiyo niwaombe sana, kama inawezekana turudishe tena huu utaratibu wa *Mtwara Corridor* ili kuweza

kusaidia Mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho kabisa niliseme na kwa kusitiza, tuendelee kuangalia sasa, tumeona hapa Mheshimiwa Rais wameridhia sasa na wameondoa ile *withholding tax* kwenye mazao mbalimbali. niipongeze sana Serikali kwa hatua hii. Pia tunaomba, sisi hasa tunaotoka kwenye maeneo yanayolima korosho waangalie na uwezekano wa kuja kufanya maboresho kwenye Sheria ya *Export Levy* kwa sababu imekuwa yenyewe maumivu makubwa kwa wakulima na haina tija tena kama ambavyo ilikusudiwa mwanzoni, kwa hiyo sasa hivi ije ikiwa na utaratibu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na naomba Serikali wazingatieve hayo machache kama sehemu ya mchango wangu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Cecil Mwambe. Ni kweli Kanda ya Kati sasa hivi tunalima korosho, na Kanda ya Kusini mjiandae, zao hilo tunalichukua, ninyi hamieni kwenye ufuta na mambo madogomadogo haya. Ahsante sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti yetu. Awali ya yote, pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia naomba nitoe pongezi nyingi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Sita, hasa kwa mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameweza kusimamia uendelezaji wa miradi yote mikubwa ambayo imeanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pia nampongeza sana kwa jinsi ambavyo ameweza kutusimamia na kutupelekea miradi mikubwa hasa ya vituo vyta afya na ujenzi wa miundombinu

ya madarasa. Kwa kweli wananchi wanashukuru sana na hili limepunguza adha na maswali mengi kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge. Kwa kiasi kikubwa imeturahisishia kazi, hasa tunapojiandaa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwezi Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti iliyopita michango mingi sana ilijikita kwenye ujenzi wa miundombinu, hasa barabara. Kwenye mapendekezo ambayo tumeyasoma kupitia Mpango huu wa Serikali tumeona kwamba kuna barabara nyingi ambazo zilikuwa zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu na nyingine zilishatangazwa, bado ujenzi haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya barabara hizo ni ya kutoka Kilosa kupitia Ulaya kwenda Mikumi, barabara ambayo ni muhimu sana kiuchumi na naamini kuna barabara nyingi za aina hiyo. Sasa ombi langu ni kwamba mipango hii inapokuja mipyä inapaswa kuzingatia barabara zile ambazo zilikuwa kwenye mpango uliopita zinakamilika kabla hajajikita katika maeneo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mpango huu haujazungumza kilio cha Wabunge wengi hasa kuhusiana na hii *service road* ambayo inahudumia ujenzi wa barabara ya *SGR*. Barabara hii ambayo kazi yake ni ujenzi na kusafirisha vifaa vya ujenzi kwa ajili ya *SGR* imefungua vijiji vingi sana vya nchi hii kuanzia Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Tabora mpaka kule Mwanza. Kuna maeneo ulikuwa huwezi kufika hata kwa pikipiki, lakini kwa sababu ya ujenzi wa reli yetu barabara hii imefungua vijiji vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, lakini hatujaona mpango wa uhakika wa Serikali, unakwenda kuihudumia vipi barabara hii kuwa moja ya njia za uhakika ambazo zitapitika mwaka mzima bila kujali masika au kiangazi. Tunajua kwamba reli hii inakwenda kukamilika, lakini nini *future* ya barabara ambayo inahudumia reli hii? Itaendelea kutumika kwa wananchi; Serikali inaichukua au ina mpango gani na hii barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu moja ya vitu ambavyo tunavizungumzia ambavyo Bunge letu hili limejipa jukumu ni kwenda kufanya mapinduzi ya kilimo. Barabara hii inasaidia sana katika mapinduzi haya ya kilimo kwa kuunganisha vijiji vyetu na barabara kuu na masoko. Kwa hiyo pamoja na mpango mzuri, naomba kupata uhakika ni kwa jinsi gani Serikali inakwenda kuichukulia barabara hii kama maeneo ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu maendeleo vijiji. Viji vyetu vingi ambavyo vinajikita kwenye kilimo havihitaji barabara ya lami, vinahitaji kufikika mwaka mzima, masika na kiangazi. Shughuli zinazofanyika kule ni nydingi na ni kubwa na ni muhimu kwa uchumi wetu. Kikwazo chao ni kimoja tu; wana uwezo wa kuzalisha, lakini hawana uhakika wa kufikisha bidhaa zao sokoni kwa sababu tu barabara haziflikiki. Kwa hiyo naomba huu Mpango wa Maendeleo au Mpango wa Bajeti ujikite katika kuhakikisha barabara zetu za vijiji ambazo zinakwenda kwenye maeneo ya uzalishaji zinapitika mwaka mzima, siyo kwa lami, kwa kiwango cha changarawe tu kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mchango wake ni mkubwa sana kwenye uchumi wa hii nchi na tukifanya hivyo naamini kilimo chetu kinakwenda kuongeza thamani yake, lakini pia umuhimu wake katika kuzalisha ajira za vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia hap ani umuhimu wa kilimo chetu na hasa kuweka mafungamano na sekta binafsi. Benki Kuu imejitahidi, imetoea fedha zaidi ya trillioni moja kwa mabenki ya biashara na lengo hapa ilikuwa ni kusimua sekta binafsi, na hasa sekta ya kilimo. Hata hivyo, tunaona kwamba pamoja na fedha zote hizi ambazo zimebekwa kwenye mabenki ya biashara kusimua kilimo chetu, bado ukuaji wa kilimo ni wa kusuasua kwa maana hakukui zaidi ya asilimia tatu mpaka nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii siyo ishara nzuri katika nchi ambayo zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wake wamejiajiri katika sekta ya kilimo. Hii ni mbaya zaidi

ukilinganisha na ukuaji wa sekta nyingine kama ujenzi ambayo inakuwa kwa zaidi ya asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu; kwanza tusiishie tu kuzungumza kwamba, kilimo ni uti wa mgongo, kilimo kwanza, kilimo ni siasa; hizi *slogans* haziwezi kutufikisha tunakotaka. Kilimo chetu kinahitaji mkakati wa kweli, kwanza wa kuboresha miundombinu kwa maana ya barabara, lakini pia pembejeo, viuatilifu, mbegu na mwisho uhakika wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukivifanya hivi vyote kwa uhakika naamini mkulima wa Kitanzania hahitaji kuamshwa asubuhi, atakwenda kulima, atajituma kwa sababu ana uhakika wa kupata pembejeo kwa wakati, ana uhakika wa kupata viuatilifu kwa wakati na ana uhakika wa kupata masoko ya bidhaa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba kuna maeneo mengi tumefanikiwa kwenye uwekezaji, lakini eneo la pembejeo za kilimo siyo eneo ambalo tunapaswa kujisifia. Naomba mapendekezo ya Mpango wetu yaje na mkakati ni namna gani tunakwenda kuhamasisha wawekezaji wadogo, wa kati na wakubwa katika uzalishaji mkubwa wa mbolea na viuatilifu ndani ya nchi na makampuni binafsi ya uzalishaji wa mbegu. Haya yakifanyika yatasaidia katika kuhamasisha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la usalama wa chakula. Waswahili wanasema adui yako mwombee njaa, kwa sababu tumbo lenye njaa huwa mara nyingi halina busara. Katika hilo wakati Taifa letu tunasema kwamba tunaweza kwenda kukutana na ukame mwakani, ni vyema tukajandaa kuhakikisha kwamba tuna hifadhi ya kutosha ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili tumezungumza kwenye mapendekezo kwamba tunahitaji kuiwezesha *NFRA*. Naomba kusema kwamba hatuhitaji kuiwezesha *NFRA*, tunahitaji kuilipa madeni yake. Serikali inadaiwa na *NFRA*, ni lini inakwenda kulipa madeni haya kwa *NFRA* ili itumie fedha

hizi katika kuwekeza maghala na kuwekeza katika ununuzi wa mazao ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba kulizungumzia ni suala zima la Serikali kuwekeza kwenye *innovation* kwa maana ya vijana wetu kujiajiri katika kuendeleza *technology* ndogondogo, lakini pia kuwekeza kwenye viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawekeza sana kwenye viwanda vikubwa, lakini wananchi wetu hawana mitaji mikubwa, wanahitaji msaada wa Serikali *ku-facilitate* kuwekeza katika viwanda vidogovidogo ili viwanda vikubwa viwe *facilitator* wa viwanda vidogo, viwanda vikubwa vitegemee viwanda vidogo katika uwekezaji wake. Najua hili liko ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumzia maendeleo ya kilimo, ni lazima tuzungumzie sekta ya maji. Hifadhi yetu ya maji siyo nzuri, vyanzo vyetu vinateketea. Wakati tunazungumzia maendeleo yetu ni vyema tukaja na mkakati wa Kitaifa kuona ni jinsi gani tunakwenda kulinda vyanzo vya maji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ingawa siyo kwa umuhimu, Jimbo la Mikumi ni jimbo la giza, halina mawasiliano. Sisi tunaomba minara midogo kwa kimo cha Mheshimiwa Mchungahela ambayo hatuna. Afadhali ya yeze ana minara mifupi, sisi hatuna kabisa kule katika Jimbo la Mikumi, kwa hiyo ikiipendeza Serikali wakati tunakwenda katika mapinduzi ya tano ya viwanda ni vizuri wakafikiria umuhimu wa mawasiliano katika kuwezesha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja. Nitachangia katika maeneo mawili; eneo la kwanza nitachangia kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa kwenye kikao hiki kwa ajili ya kupanga mpango wa maendeleo, lakini maendeleo ni elimu. Yaani elimu yetu kama Taifa ndio inachora ramanii ya maendeleo. Tunazungumza, tunajadili, lakini kama hatutazungumza elimu, tutakuwa hatujatendea haki Taifa hili. Muda sasa tumekuu tukijadili kuhusiana na kurekebisha Sera ya Elimu nchini ambayo ni ya mwaka 2014 na kurekebisha mtaala wa elimu ambao ni *competence-based* lakini 2005 mara ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sisi kama Wabunge ambaao tunapewa hizi nyaraka na tunasoma, tuone kama uhalali wetu wa kujadili haya upo, tunatakiwa tuyaone katika Mpango. Siyo kwenye bajeti wala siyo kwenye Mpango huu wa mwaka mmoja Wizara imetenga hata senti moja kwa ajili ya kufanya mchakato wa mapitio ya sera na mapitio ya mtaala wa elimu. kwa kifupi mpaka sasa Serikali haijatenga hata shilingi moja kwa ajili ya *ku-facilitate* wanaofanya mchakato wa mapitio ya sera na mapitio ya mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ratiba yako, wewe unafahamu zaidi na namna ambavyo tunapanga mambo yetu, unajua kwamba *possibility* ya kufanikisha tunachokizungumza kila siku ni ama 2023 au 2024 kwa sababu watu hawawezi kwenda kufanya kazi ngumu ya kukusanya maoni na kufanya mapitio, kuita wadau ambaao ni *professionals*, ambaao ni Watanzania ambaao wanaitakia mema nchi hii, bila kutumia ghamra. Haiwezekani! Kwa hiyo hapo nimesema kwa kweli kwa kutoa masikitiko yangu sana kwa sababu nilitegemea mpango uwe na *at least* hata pesa kidogo kwa ajili ya kuanza mchakato wa mapitio ya mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nitakuwa nimekwenda mbali sana Wizara ilishakutana na Wajumbe wa Kamati inayohusiana na masuala ya elimu, Kamati ya

Huduma na kwa taarifa zilizopo ni kwamba tarehe 11 Novemba wanakutana na Wabunge wote kwa ajili ya kupokea maoni. Sasa naomba niombe sasa badala ya kujadili kuhusiana na mtaala, wajadili kuhusiana na sera, kwa sababu kwa taarifa Wizara inajaribu kurekebisha mtaala na sera *at the same time*, kitu ambacho hakiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala ni zao la sera. Bunge lako litusaidie kuifanya Serikali ituletee mjadala wa kujadili Sera ya Elimu tarehe 11, siyo mtaala wa elimu. Nasema hivi kwa sababu hatuwezi kujadili sera hatujapanga tutafanya nini kutoka mwaka 2014 kwenye sera. Wabunge sehemu pekee ambayo tunaweza kuchangia sisi, ni tunaiona wapi nchi yetu *after few years to come*, ndiyo tutaeleza malengo. Tafsiri ya tunapotaka nchi yetu ifike ndiyo itatuambia tuandike nini kwenye sera ili sera ikatusaidie watu wanaoandika mtaala wakatoe tafsiri ya tunataka nini kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo nilisema maendeleo ni elimu. Kwa hiyo kama tunapanga mpango wa maendeleo na hatujadili kuhusu nchi yetu tunataka kwenda wapi. Nitatoa mfano, Kenya wametoka kwenye *competence-based, CBC – Competence-Based Curriculum* na sasa wanajadili *talent and professions*, talanta na taaluma. Walishafanikiwa kwenye *competence-based*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 wakati tumefanya marekebisho ya mtaala ndiyo tuliweka *Competence-Based Curriculum* ambayo tunayo mpaka sasa hivi. Tukiletewa Waheshimiwa Wabunge wataona kwamba hatuna shida kwenye *documentation* kama nchi, yaani utashangaa kwani huwa tunajadili nini kuhusiana na kurekebisha mtaala. Kwa hiyo kuna shida kutoka kwenye mtaala kwenda kwa anayepelekewa, yaani kuna shida kutoka kwenye kilichoandikwa na kinachomfikia, katikati hapo ndiyo kuna shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nitapongeza jitihada ambazo zimefanyika kwa sababu kwenye mpango wametuambia kuhusiana na, kwa kweli tunahitaji maeneo

ya kujifunzia; madarasa, Walimu na vitendea kazi. Kwa hiyo tunahitaji na tumeona kwenye Mpango wameweka. Kama mdau wa elimu siwezi ku-*ignore* jitihada ambazo zimefanyika. Kwa hiyo tuna-*encourage* sana jitihada, lakini tukumbuke kwamba dunia haitusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inazungumza Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (*Fourth Industrial Revolution*) ambayo inazungumza *artificial intelligence*, inazungumza *algorithm*, vitu ambavyo vina-replace *human labour*. Sisi tunazungumza *competence based education* ambayo inafundishwa kwa *knowledge based education*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala wa 2005 unatuambia *competence based* lakini kinachokuwa *delivered* darasani ni *knowledge based*. *Knowledge based* maana yake mwanafunzi anasoma, anakariri na kukariri ili akafanye mtihani *knowledge-based*, unajaziwa madude kibao. Kwa hiyo sasa kwa sababu hatutakwenda huko leo, naomba sana kwa sababu tunatumia rasilimali zetu vizuri, dunia inazungumza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wakati tunasema dunia inazungumza *artificial intelligence*, nimpongeze sana Rais, Dkt. Mwinyi na kwa sababu kwenye umri wa vijana tunam-*consider* kama bado kijana mwenzetu, amejitahidi, kwa sababu amezungumza kuhusu *digital currency* na imechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais pia kwa sababu anajaribu kuona *opportunities*. Kwenye hili nitasubiri mjadala ambao tutajadili Sera ya Elimu ambayo tunasubiri muda mrefu kwa sababu ya *resources*, twende kwenye sera kwanza, tuone mwelekeo wa nchi kwenye elimu tunataka nini, halafu ndiyo tuje tujadili mtaala, kwa sababu najua pia *resource scarcity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*move* kwenye jambo la pili ambalo ni la jumla. Mimi ni Mbunge kijana, *thinking* yetu sisi *millennials* na hili nitalisema na watu

wanaojua *generation differences* watakuwa wanaelewa. Asilimia kubwa ya Watanzania na asilimia kubwa ya Waafrika wanaitwa *millennials*, watu waliozaliwa mwaka 1980 mpaka mwaka 1996; *thinking, smartness, activeness*, watu wanataka matokeo, tupo wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukawa tunaendelea kuendesha nchi kwenye mfumo wa tunapanga, kesho tunapanga tena na tena, *the same way*. Tunaomba tu-move. Tupo wengi tunaomba tu-move, yaani inawezekana kabisa. Watanzania wanataka majibu ya shida zao. Kwa maana tuwe tuna *flagship projects*, watu wanataka pesa mfukoni, watu wanataka bima za afya, wanataka *price fluctuation* (mfumuko wa bei) usiwepo, wanataka kula, wanataka wafanye kazi, *projects* zote tunazoziveka tunazitambua na ni vitu vizuri; *progress*, miradi mikubwa. Hata hivyo, tunakuwa *irrelevant* kama nchi kwa sababu Watanzania hawaoni kama hayo mambo yanawagusa *directly*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachajaribu kusema ni kwamba, Watanzania wanataka majibu ya shida zao na shida zao tunazijua kwa sababu ndiyo wapigakura wetu. Kwa hiyo nchi ambayo inashindwa kutoa majibu ya watu wake *definitely at the end of the day* inakuwa *irrelevant*, inakuwa haiishi wanachokitaka wapigakura.

Kwa hiyo hatutachoka kuongea, hatutachoka kushauri kwa sababu haiwezekani sekta ambayo kila Mbunge akiongea anazungumza; kilimo, tunapata chakula, inachangia pato la Taifa, lakini kila mwaka tunapanga *the same*. Kwa nini hatuweki pesa kwenye kilimo? Inachosha na inavunja moyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa sababu hii nchi, mimi Muislam, kuna kitu kinatwa masuulia, yaani ukiwa una nafasi kwenye Taifa unatakiwa ufanye maamuzi, ukishindwa kufanya maamuzi, kesho Mwenyezi Mungu atakuhoji kwa kushindwa kufanya wajibu wako.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hanje kengele ya pili hiyo.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanataka majibu ya shida zao, naomba tuwasaidie kuwapatia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje. Tunaendelea. Nilikutaja Mheshimiwa Ng'wasi, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla unafuatia.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika mjadala huu wa Mpango wa Mwaka Mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kuu itakuwa kuwazungumzia wapigakura wetu walio wengi katika nchi hii ambao ni vijana. Changamoto namba moja, ambayo nitaendelea kuipigia kelele ambayo ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu, ndani ya muda mfupi ambao ameingia vijana ni kundi ambalo ameendelea kulibeba, ameonekana kutokulisahau na hata katika maamuzi mbalimbali ameendelea kutukumbuka. Kwa hilo tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mambo machache tu ambayo ningependa katika Mpango huu ambao ni wa mwaka mmoja basi tuyazingatie kwa kuangalia vijana hawa. Kama tunazungumzia asilimia zaidi ya 60 ya watanzania wote ambao ni vijana, maana yake tulitegemea *discussion* kubwa *may be* asilimia zaidi ya 30 ya Mpango huu uwe unalenga kuliangalia kundi kubwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye hili hasa katika suala hili la ajira niongelee mambo machache. La kwanza, tangu Mheshimiwa Rais ameingia madarakani kwa hii miezi

sita kuna ajira nyingi sana zimeshatangazwa zaidi ya ajira 5000, katika taasisi mbalimbali kuna *TANAPA*, *TAKUKURU*, *POLISI*, *TRA* tunashukuru sana. Kwa hilo, tunashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vigezo ambavyo vimeduwa vinajumuishwa kwenye *qualification* za watu wanaotakiwa kuomba ajira hizi, ambazo kwetu sisi vijana tunakiri kusema kwamba zinatutatiza kidogo. Kwa mfano; kuna kigezo cha mtu awe amekwenda *National Service* au JKT. Tukiangalia katika Nchi yetu, kwanza kabisa nafasi za JKT zinazotangazwa huwa ni chache ukilinganisha na idadi kubwa ya vijana tulipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbili hata wale ambao wana ule mfumo wa kutoka *form six* kwenda JKT bado Serikali yetu haiwachukui vijana wote. Kuna baadhi ya miaka vijana wamechukuliwa kulingana na *division* zao kwamba, mwenye *division one* na *division two* peke yake ndiyo watakwendwa. Lakini kuna baadhi ya miaka wamechukuliwa vijana kwa *alphabetical order* ya majina yao. Kwamba, kwenye wale wenye walioanzia A labda mpaka J ndiyo watakwendwa wanaobaki wanabaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, naona inasikitisha sana kama tukianza kutoa ajira kwa vijana kwa kuwashukumu kulingana na *alphabetical order* ya majina yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwa vile ninaanziwa na N basi ajira fulani fulani nizisahau au kwa sababu nilipata *division three*, lakini *qualification* zote ninazo basi ajira fulani fulani nizisahau. Kigezo hiki si sawa na kama Serikali yetu ilikuwa inaona kwamba ni muhimu kutangaza ajira kwa vigezo vyaa namna hii, basi ingeanza kwanza kutengeneza mazingira ya vigezo hivi ndiyo twende kwenye ajira kulingana na vigezo hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadiriki kusema kwamba tukiendelea na vigezo kama hivi tunavunja Katiba yetu hasa Ibara ya 13(4), ambayo inakataza Kitengo chochote cha Serikali au Mamlaka kutoa maamuzi yoyote ambayo yataleta

ubaguzi kwa watanzania kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, nashauri kuanzia sasa Serikali yetu iangalie, tunapokuwa tunatoa ajira au fursa kwa vijana wetu, ili wote tuweze *kuzi-access* kwa usawa basi tuangalie vigezo ambavyo vina maana na ambavyo vina maslahi katika utekelezaji wa ajira hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili ni suala zima la mitandao. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu miezi kadhaa iliyopita, hali ya hewa ilichafuka kidogo baada ya gharama ya mitandao kupanda na akatoa maelekezo kwamba gharama hizo zirekebishwe lakini suala hili lisijitokeze tena. Sisi vijana tunatumia sana mitandao siku hizi kujiajiri, na hii imeipunguzia sana Serikali mzigo wa kutuajiri sisi vijana. Lakini si kujiajiri tu, tunatumia pia mitandao hii kusoma kwa hiyo inachukua nafasi kubwa sana katika maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto iliyokuja ni kwamba baada ya Mheshimiwa Rais kutoa maelekezo kwamba hali hiyo irekebishwe na isijirudie tena, imeanza kurudishwa kidogo kidogo, kidogo kidogo, mpaka sasa tunavyozungumza imerudi hali ile ile alioikanya Mheshimiwa Rais. Nitoe tu mfano kidogo kwamba katika takwimu zilizotolewa na *TCRA* kwa mfano mdogo tu wa mtandao wa *Airtel*. Gharama ya *MB 1* kwa takwimu za robo mwaka kwa Disemba, 2020 ilikuwa ni shilingi 5/= kwa *MB 1* kwa mtandao wa *Airtel*. Robo iliyofuata ambayo ni Machi, 2021 ilibaki hivyo hivyo shilingi 5/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Juni, 2021 imepanda mpaka shilingi 9/= *almost twice* na kwa vile tu *TCRA* hawaja *upload* taarifa ya robo iliyofuata ambayo inakwisha mwezi Septemba, 2021. Maana yake tunategemea itakuwa imepanda zaidi, ni ngumu sana kwa kijana wa Kitanzania ambaye anategemea mitandao hii kujiajiri. Kutumia gharama kubwa namna hii ambayo haistahimiliki kuweza kufanya shughuli zake na kimsingi, Serikali inakuwa imeshindwa kabisa kumsaidia Mtanzania kijana wa kitanzania kutengeneza mazingira bora ya kujiajiri mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kwamba Serikali yetu pia ni *shareholders* kwenye mitandao hii ya simu. Kwa hiyo, ina nafasi kubwa sana pia ya kutusemea na kutusaidia kutengeneza mazingira bora ili vijana tuweze kuendelea kujiajiri kupitia mitandao hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizidi kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na ama kweli ni haki kusema kwamba tumepeata mama mtafutaji kweli kweli. Mama atakwenda akirudi anawaambia nimerudi na kijisenti hiki kidogo tutagawana hivi tena kwa uwazi kabisa. Hilo tunamshukuru sana na kwa kweli sisi kama vijana, anazidi kutupa imani ya kwamba miaka hii minne inayofuata itakuwa ni miaka ya neema kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo nilitegemea basi, kulingana na fedha hizi za *Covid* ambazo tumepeata, tumepeata madarasa 15,000 ya Sekondari, tumepeata Shule Shikizi madarasa kama 3000, tumepeata *ambulance* 395. Lakini pia, kwa fedha za tozo hizi hizi kwa maarifa ya Mheshimiwa Rais tunapata pia madarasa mengi sana katika shule zetu za Misingi na Zahanati. Basi nilitegemea katika Mpango huu wa mwaka mmoja wa bajeti unaofuata tungeona basi Serikali yetu kwa kuangalia pia tuliwaahidi wapiga kura, tuliwaahidi vijana hawa ajira milioni 8 tuone ajira ambazo zitapatikana. Hasa za walimu, madereva na wauguzi au watendaji katika Sekta ya Afya zinakuwa reflected katika Mpango huu, hasa kwa mwaka unaofuata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo *nita-subscribe* kwa alichokisema Mheshimiwa Kingu jana kwamba, tutatibu kitu kimoja lakini tutazalisha changamoto nyingine ya kutokuwa na ubora. *Either* katika elimu au katika Afya kwa sababu tutakuwa na madarasa mengi, wanafunzi wengi bila kuwa na watumishi wa kutosha. Ninaomba tukuze imani ya vijana hasa kwa Serikali yetu kwa kuakisi hizi juhudii za Mheshimiwa Rais. Katika Mpango huu tuoneshe namna gani Serikali imejipanga kutangaza ajira za kutosha kwa walimu, kutangaza ajira za kutosha kwa wauguzi na madereva. Ili

tuzidi kuiamini Serikali yetu na vijana tujiandae kuweza kukidhi matakwa haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nimalizie, wakati Wabunge wengi wanazungumza, wamezungumza juu ya vipaumbele na mimi nikanukuu mchango wangu katika Mpango uliopita wa Bajeti iliyopita, niliomba kwamba ni muhimu Serikali yetu ikaja na vipaumbele ambavyo vitatuongoza katika mipango yote tunayotengeneza. Wabunge wengi wamekwishazungumza kwamba ni matakwa yetu kama wawakilishi wa wananchi tulitaka kipaumbele kiwe Kilimo. Sasa katika kilimo mwaka huu, mwaka 2021 Mpango wa Taifa wa kuwashirikisha Vijana katika Kilimo ndiyo unamalizika na umekwisha malizika Oktoba, 2021. Mpango huu ulikuwa unaanza 2016 – 2021 na kuna *observation* fulani zimeonekana katika Mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya *observation* hizo ni kwamba kilimo *it is not attractive* kwa vijana kushiriki katika Sekta ya Kilimo katika Nchi yetu. Sasa nilitegemea kwa vile Mpango huu umekwisha, basi huu Mpango unaofuata wa mwaka huu ungetuonyesha kwamba, sasa *tu-test* mafanikio ya huu Mpango wa miaka minne ulifanyika wa kuwashirikisha vijana katika Kilimo. Lakini pia una Mpango gani mpya sasa baada ya kuangalia mafanikio ya Mpango huu, wa kuhakikisha kwamba basi kilimo kinaanza *kuwa-attract* vijana ili wote tuweze kushiriki. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwasi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunakushukuru bado kidogo Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na baada ya Kigwangalla Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ujiandae.

Nilitaka kukubaliana nawe sana kwenye sharti la JKT kuwa sharti la ajira, nafikiri tuliwahi kusema mahali na kwa

kweli tunawaomba Serikali waliangalie hili jambo, ni ubaguzi tu. Juzi niliwaambieni Jimbo la Musukuma Geita Vijijini darasa la nne waliofanya mithani ni 48,000. Hivi Makambi ya JKT yana uwezo wa kuchukua vijana 48,000? Kwa hiyo, maana yake tutafika mahali ambapo Geita Vijijini peke yake inajaza Makambi yote.

Kwa hiyo, unaacha vijana wa Nchi nzima kwa sababu ya kigezo cha JKT kuwachukua kwenye ajira. *Its not fair*, kwa sababu hatuwachukui wote kama alivyosema, kuna wakati wanachukua *alphabet* tu mpaka mahali fulani basi. Kuna wakati wanafanya *ka-random sampling* fulani basi. Kwa sababu, watoto ni wengi mno hivi sasa.

Kwa hiyo, maelfu kwa maelfu hawataweza *ku-access* baadhi ya ajira za aina aina kwa saababu ya sharti hili lilikuwa na maana enzi zetu. Kwa sababu, enzi zetu sisil wote tulikuwa tukienda JKT. Lakini leo, sijui kama hata asilimia 10 ya wanaomaliza *form six* na *form four* wanakwenda. Tena ukichanganya *form six* na *form four* hata asilimia 5 haifiki inayokwenda JKT. Kwa hiyo, *ninety* nzima unaiacha haiwezi *ku-compete* kwenye ajira kwa sababu ya kipengele hicho si sawa. (*Makofi*)

Lakini pia kuna lile ambao tulishaliacha limerudi tena la urefu. *Seriously* naliongelea kama *joke* na tulishaliondoa hili sijui limerudije hill? Ni mambo ya hovyo tu kwani urefu wa mtu una uhusiano gani siku hizi mtulinga umeshaondoka kwenye mtulinga. Wanahitajika wachache tu kwa ajili ya kazi maalum basi, lakini kuwabagua tena *especially* wanawake. Wanawake wa Tanzania wengi ni wafupi wafupi mama zetu, hawana urefu huo wanawake warefu wachache sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, masharti masharti mengine kama haya yatazamwe kwenye eneo la ajira si vizuri kumbagua mtu yejote kwa kitu ambacho hii *OSHA is nothing to do with it*. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Ng'wasi kwa kusitiza masuala ya ajira na usawa katika ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla atafutiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally. Salum.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote nianze kutoa mchango wangu kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea shilingi triliion 1.3. Lakini pili niseme tu ukweli, nilihamasika kuchangia kwenye Mpango huu, awali sikuwa na mpango huo baada ya kauli yako jana, kwamba hizi shilingi triliion 1.3 zilizoletwa na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan zimeichangamsha nchi. Ni kwa nini na sisi tusiweke Mpango wetu wenyewe kwenye Bajeti inayokuja wa kutenga shilingi triliion 1.3 au shilingi triliioni 1.5 ya kwetu wenyewe kwenye Bajeti? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili kwa kweli ilinifikirisha sana na ndipo nikaona niombe kuchangia, ili kuweka msisitizo kwenye jambo hilo. Maana yake ulilisema juu juu hivi halafu likaishia pale nikasema pengine nitoe mawazo yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli nakubaliana sana na hili wazo na ninasema hivi kwa sababu, ninaona kuna haja ya kufanya hivyo kutokana na mambo kadhaa ambayo nitayataja. Mojawapo kwanza ni *affirmative action* kwamba tutakuwa tuna Mpango mahsus wa nini tufanye na fedha yetu wenyewe. Kwa ajili ya kusambaza keki ya Taifa kila kona ya Nchi yetu kwa maana ya kwenye majimbo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tutakuwa na sababu mahususi za kitu gani fedha hizi ziende zikafanye. Lakini la tatu, tuna *stress* kubwa sana kwenye uchumi wetu kutokana na namna tulivyoendesha mambo yetu hapo nyuma. Lakini pia kutokana na kuingiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa *Covid-19*. Kwa hivyo, uchumi umeathirika sana, uchumi *una-undergo stress* kubwa sana. Kwa amba ni wahangaikaji, wajasiriamali wenzangu huko mtaani watakubaliana na mimi, hali si shwari kwenye uchumi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kurudi kwenye mzunguko mzuri ni lazima Serikali ifanye mambo kadhaa. Mojawapo kiukweli ni kutoa nafasi za ajira kwa wingi zaidi ili watu waweze kuajiriwa. Ama iongeze mishahara, ama iongeze posho kwa maana ya *ku-pump* fedha kwenye jamii, ili mzunguko uwepo kule watu waweze kutumia uchumi uweze kukua tena. Lakini uchumi wetu kabla ya *Covid* na kabla ya miaka hii kadhaa hapa nyuma ulikuwa unakua kwa kiwango cha asilimia 7. Sasa hivi unakua kwa kiwango cha asilimia 4 hivi kwenda kwenye asilimia 5 hapo. Maana yake hatuko vizuri sana kwenye *economic growth* na ili uchumi uweze kukua ni lazima tufanye juhudhi za makusudi kabisa za kusukuma fedha kwa wanachi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo hii inaweza ikawa ni njia mojawapo ya kusukuma fedha kwa wananchi. Lakini mbali na hivyo nimeona kwamba tunaweza tukatumila mradili huu wa shilingi 1.3 trillioni ambao umeingia, kama chachu ya sisi wenye kuanzia tu na kuanza kutenga fedha kwa ajili ya miradi ambayo inaenda kuwagusa watu. Hususani kufuatia *stress* ambayo imeufika uchumi wetu na mambo yafuatayo ningependa kushauri yafanyike. Kwamba, katika hizi fedha ambazo tumegawiwa sasa hivi kwenye Majimbo yetu, ni lazima kutengenezwe mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi ya fedha hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kutengenezwe mfumo mzuri wa ufuatiliaji, mfumo mzuri wa tathmini na mwisho wa siku mfumo wa kupima matokeo. Na sasa kuanzia hapo kwa sababu, hizi fedha zitakwenda mpaka mwisho wa bajeti hii tuliyonayo sasa. Kwenye bajeti itakayokuja Serikali ituletee Mapendekezo ya namna ambavyo tutapata pengine shilingi trillioni 1.5 nyingine sasa ambayo tutakwenda nayo kwenye mwaka ule utakaofuata. Na hii itakuwa ni kama vile *measure* ya *ku-stimulate* ukuaji wa uchumi baada ya janga la *CORONA* ambalo limeupiga uchumi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tutakuwa tumeweka mifumo mizuri ya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini kutokana na hii shilingi trillion 1.3 tuliyopewa sasa hivi maana

yake mwakani tutaendelea tu na Mpango ule. Ambao utakuwa mzuri zaidi kwa ajili ya kutia chachu ukuaji wa uchumi tena na kuhakikisha kuna mzunguko kwenye maisha ya watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ni lazima tuweke mfumo ambao utawezesha kitu kama *pay for performance* yaani kama vile *performance basic financing*. Kwamba, tukiweka vigezo sasa hivi na fedha zimeshakwenda, wale watakaofanya vizuri basi *wata-enjoy* hiyo shilingi 1.5 trillioni ambayo itakuja kwenye bajeti ijayo. Kwa hivyo mfumo kama huu utapendeza sana kama utafanyiwa kazi, utaandaliwa na hatimaye utatekelezwa. Kwa sababu, linaweza likawa ni jambo la kudumu kwamba, tunatenga fedha kwa ajili ya miradi mahususi kila mwaka kwenye bajeti yetu sisi wenyewe na wala sio kusubiria mikopo ama fedha za wafadhili. Kwa hivyo mfumo kama huu wa kulipa kwa matokeo unaweza ukafikiriwa kutumika kwenye matumizi ya hizi fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia, kutokana na *stress* ambayo imeukumba uchumi wetu, ni lazima mbali na hayo ambayo tayari nimekwisha kuyasema Serikali ifikirie kuweka ahueni kwa wajasiriamali na wahangaakaji. Nchi nytingine tumeona makampuni ambayo yamefeli kulipa mikopo *eitherile* mikopo ikichukuliwa na Serikali kupitia *special purpose vehicles*, ama yanapewa ahueni kwamba malipo ya marejesho kwa kipindi fulani yatasimamishwa ili hizi biashara ziweze kukua ili ziweze *ku-thrive* tena kufuatia kuanguka kwa uchumi ambako kumesababishwa na *Covid-19*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kwetu tunaweza tukafanya mambo machache kadhaa ambayo napenda kuyasema. Kwa mfano, kwenye sekta ya utalii ili tuweze kuvutia watu kuja hapa nchini Tanzania inasemwa sana kwamba, ni nchi ambayo ina gharama kubwa kuja kuitembelea basi gharama hizo tunajua zinasababishwa na nini. Ni *parking fee* za ndege, *landing fee* za ndege, kodi kwenye *jet fuels* zote hizi tunaweza, tukatafuta namna ya

kwenye bajeti inayokuja pengine tukazishusha chini ili kushusha gharama ya watu kuja Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukazitangaza hizi bei mpya mwisho wa siku tukavutia watalii wengi zaidi kuja hapa Tanzania. Lakini pia, tukavutia wawekezaji wengi zaidi kuja Tanzania. Hiyo nayo inaweza ikawa ni njia mojawapo ya kuweza *ku-catalyze economic growth* kufuatia janga la UVIKO-19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, ili *ku-stimulate* pia *growth* ya biashara hapa nchini ni lazima tu-*consider* baadhi ya malipo kwa mfano, *pay as you earn, skills development levy*. Tukayasimamisha kwa kipindi fulani ili kuyafanya makampuni yetu ambayo yana madeni makubwa ambayo yanashindwa kuendesha shughuli zake, kwa sababu, kipato kimeshuka kutohana na mzunguko kuwa duni yakaweza *ku-thrive* katika kipindi hiki kigumu ambacho tunapitia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Serikali inaweza ikaangalia katika Mpango wake namna ya kufanya *stimulus*, kwenye biashara za hapa nchini ili kuvutia uwekezaji. Lakini pia ili kuwalinda wale wawekezaji ambao wanajikongoja katika kipindi tulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali inaweza ikasaidia ni namna gani benki za biashara zifanye kwa wale wafanyabiashara ambao pengine wameshindwa kulipa mikopo. Badala ya kufilisiwa na mali zao kuuzwa ama kufunga biashara basi mikopo ile ikasimamishwa kwa kipindi fulani, ikapelekwa mbele ikafanyiwa *restructuring*. Halafu biashara zile zikaruhusiwa ziendelee na mwisho wa siku *zika-thrive* zikachangamka na uchumi ukachangamka kwa ujumla wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nilikuwa napenda nitoe ushauri huo kwamba, ni lazima Mpango huu ambao umeletwa hapa tuutolee mawazo yetu ukafikiria namna fulani ya kuweka *stimulus* kwenye *economic growth* ya nchi yetu. Na jambo la mwisho ambalo napenda

kuzungumzia linahusu uwepo wa baadhi ya miradi ambayo inasemekana imekuwa *over costed*. Kwamba, anakuja mtu *ame-tender* labda shilingi 100 anaonekana ni *tenderer* mmoja, sasa na huyo mmoja anashindwa kupewa ile *tender* wana *re-advertise* inapotangazwa kwa mara ya pili anakuja *tenderer* mwingine. anasema mradi ule badala ya shilingi 100 labda yeye *ata-tender* kwa shilingi 150 anapewa mradi, akishapewa mradi anarudi kumtafuta yule aliyekuwa *ame-tender* kwa shilingi 100 anampa ile kazi aende akafanye yeye anakula shilingi 50 bila kufanya kazi yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna kila haja ya Serikali kuichunguza na kuifuatilia sana miradi yetu na namna *tender* za miradi mikubwa zinavyofanya. Kwa sababu, kumekuwepo na taarifa za *over costing* ya miradi kutokana na *tenderers* kupewa miradi kwa *style* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla. Nilikutaja Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, utafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said, Mbunge wa Konde.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi pia niungane na wenzangu kumshukuru sana Mheshimiwa Mama yetu Mpendwa Samia Hassan Suluhu, kwa hizi fedha ambazo kwa kweli zimekuja kukomboa majengo yetu katika Majimbo yetu. Mimi binafsi nilikuwa na majengo zaidi ya 150 katì ya miaka sita au miaka saba ilifika mahali sijui nifanye nini. Lakini sasa hivi kwa kweli naishukuru sana Serikali chini ya Mheshimiwa Mama Samia, tunakwenda kumaliza matatizo haya ya maboma yetu vizuri na watoto watakwenda kusoma vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia sana Mheshimiwa Kigwangalla na Mheshimiwa Abbas Tarimba, suala zima hapa ukitazama kwa upana wake matatizo yote

haya ili kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji katika mpango huu, ninashauri sana *blue print* ifanyiwe kazi. *Blue print* leo inaongelewa zaidi ya miaka mitatu, mambo yote ambayo yapo kwenye *blue print* yakifanyiwa kazi, wawekezaji siyo tu wa nje hata wa ndani watapitia humo humo na wataweza kuwekeza vizuri na kuweza kurudi kwenye ile hali ambayo wanaitaka wenyewe. (*Makofj*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongelea hapa Mheshimiwa Kigwangalla katika suala hili la *Covid-19* limeathiri sana uwekezaji, biashara na kadhalika. Ukija kwenye hii *blue print* ni mambo mengi mno ambayo ukiipiga *overall*, kwa ujumla wake na nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha itizame hii. Leo watu wanatoa viwanda vyao hapa wanapelekea Uganda kuna watu wanapeleka Uganda ili azalishe *a-export* bidhaa tena Tanzania au Congo! Yote hiyo moja katika sababu kubwa sana bado sisi hatupo vizuri sana *ku-refund VAT on export product*. Tunauza bidhaa nje lakini *ku-refund* zile *VAT* tunachelewa mno kuliko Uganda na Rwanda wanavyofanya. Leo Uganda na Rwanda wanafanya vizuri sana kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Rwanda wanapata wawekezaji wengi siyo kwa sababu ya *population* waliyokuwa nayo Rwanda. Rwanda wana *population* ndogo mno lakini uwekezaji unaofanyika katika nchi ya Rwanda *wana-target* nchi kama ya Congo, *wana-target* nchi za jirani na hata juzi kuna malori yamekwenda kupakia hivi vifaa tiba tu Rwanda wanakuja kuleta Tanzania, hivi ni *kweli*? Yote haya ni kwa sababu ya *blue print* hatuifanyii kazi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la muhimu sana siyo la kufanya mzaha tu hivi. Pitia hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe mwenyewe na Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri Mkuu uko hapa, angalieni namna ya kufanya yale ambayo hayana madhara kwenye nchi, toeni watu waje wafanye kazi wawekeze mambo yaende na nchi iweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu uwekezaji kwenye viwanda. Ni jambo jema sana kupata wawekezaji kutoka ndani ya nchi ni zuri tu. Lakini ni hatari sana kama hatutakuwa na mpango maalum wa kuwawezesha watanzania wakaingia moja kwa moja kwenye uwekezaji hasa wazalishaji wa viwanda. Itaweza kufika mahali huko mbele ya safari mkawa na wawekezaji wageni zaidi ya asilimia 80, halafu Watanzania wakawa kama wasindikizaji asilimia 10 au asilimia 15 tu, *by then* huko wakija kuungana tu wanawenza wakaiyumbisha Serikali itakayokuwepo huko mbele ya safari. Kwa hiyo, ni jambo la muhimu sasa sana tena, Serikali ione namna ya kufanya kuwawezesha watanzania waliopo katika biashara na watakaotaka kufanya kazi hiyo ni namna bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama Benki ya Afrika ya Kusini (*South African Bank*) mtu anakwenda na *proposal* yake, *proposal* yake kama ni nzuri wameipenda na haikukamilika, wanaibeba ile *proposal* wanaifanyia kazi wanakuchukua wewe mwenyewe kuna wataalam pale mpaka wanahakikisha ile *proposal* imekaa vizuri na fedha wanakupa na kazi inafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii tusipofanya hivyo, hivi ukitenga hizi Shilingi Bilioni 500 ukapeleka kwenye hizi *Developments Bank* kama *TIB* ukasema sasa Watanzania waende pale, mkapunguza riba hata asilimia 10. Fedha kama ni za Serikali wana haja gani wao Benki kutoza asilimia 18 wakati fedha ni za Serikali. Malengo makubwa ni kuwawezesha Watanzania wawe na viwanda wengi waingie kwenye ushindani huo huo ambao wawekezaji wa nje wanatoka kuja kuwekeza ndani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo mangapi tunayahitaji na unawenza ukaweka *strategy* tu kwamba, tunatoa hizi fedha katika Benki zetu za Maendeleo lakini tunataka wawekezaji wa aina hii. Wawekezaji wa viwanda vyaa pamba, wawekezaji wa mafuta, uwekezaji ambao una manufaa kwa nchi na kwenda kujibu masuala majibu ya masoko ya kilimo ambayo wakulima wanazalisha. Kwa

mfano, katika Kanda ya Ziwa zao la pamba linaajiri zaidi watu milioni 20 lakini kuna kiwanda gani Shinyanga? Hakuna viwanda vya pamba Shinyanga, hakuna kiwanda cha pamba labda Mwanza. Kuna kiwanda cha Urafiki hapa kimekufa tu, kiwanda cha Urafiki kwa historia yake ni ushirika baina ya Tanzania na China, lakini tunashindwaje kwenda kuongea na Serikali ya China kuwaomba tu bwana hiki kiwanda, naomba mkiache tupeni sisi kirudi kwenye mkono wa Serikali mkitangaze ili watu waje wawekeze.

Mheshimiwa Spika, leo pale kiwanda cha Urafiki imekuwa magofu, yule Mchima anakodisha kodisha tu maduka yale imekuwa ukiingia pale mpaka roho inakuumua, Kiwanda kiko vizuri mno yaani pale lakini kimekaa tu. Hatuoni *strategy*, hatuoni Serikali kufanya *intervention* kuongea na Serikali ya China watuachie ili tuitangaze aje mwekezaji mkubwa pale na ikiwezekana aje Mtanzania afanye kazi pale. Kwa hiyo ni suala tu... (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Pokea taarifa Mheshimiwa Ahmed Salum.

## TAARIFA

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa kwanza tu kuweka sawa maneno nafikiri alipokuwa anasema viwanda vya pamba Shinyanga, Mwanza kwamba havipo, vipo. Hata mimi mwenyewe tu nimpe taarifa ni Mwekezaji kwenye sekta ya pamba na nina kiwanda cha pamba kipo Mwanza. Tatizo tulilonalo siyo kukosekana kwa viwanda vya pamba, tatizo tulilonalo ni kwenye kilimo. Kulizuka mjadala mzito sana hapa jana kuhusu kilimo ni kweli shida tuliyonayo hatuna uwekezaji wa kutosha kwenye kilimo kwa sababu, viwanda vya pamba vyote vilivyopo hapa nchini vinagombania *raw material*, vinagombania pamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba kuna shida ya pamba na kuhusu kiwanda anachokizungumzia cha *textile*, changamoto kubwa hapa kwenye nchi yetu ukitaka kufilisika

wekeza kwenye kiwanda. Changamoto kubwa umeme, kodi, uitiri wa tozo na *involvement* ya Serikali kwenye kila hatua ya uwekezaji wako. Ndiyo maana hakuna mtu atawekeza kwenye kiwanda ambacho ni *capital intensive* kama cha *textile* hapa nchini na akafaidika. Kila atakayejaribu atafeli kwa sababu, riba za benki ni kubwa na mahali pa kuuza *finished goods* za kutoka kwenye kiwanda chake ni padogo. (Makof)

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa unajua hilo kwa nini Mheshimiwa Kigwangalla wewe umewekeza? Mheshimiwa Ahmed Salum unapokea taarifa hiyo? (Kicheko)

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Mheshimiwa Kigwangalla namheshimu sana lakini tukisema viwanda vya pamba ni viwanda vya pamba. Kiwanda cha pamba kimoja cha India kinanunua pamba yote ya Tanzania. Viwanda tulivyokuwa navyo hapa Mheshimiwa Kigwangalla ni vya nyuzi tu na *ginnery*. Kiwanda kama kiwanda ina maana kuna kiwanda *ginnery* inaunganishwa nyuzi, inakuja inazalisha nguo, hicho ndicho kiwanda. Magari 500 kwa mpigo zikishusha zinaingia pale mashine zinachukua zile pamba zinachakata. Kiwanda kimoja ukitembelea India au China kimoja kinanunua pamba yote ya Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka viwanda vya aina hiyo ambayo vinakwenda kujibu masoko ya wakulima wa pamba, vinakwenda kujibu masoko ya walimaji labda korosho na kadhalika na kadhalika. Yaani unaweka viwanda 10 vya kimkakati ndani ya nchi hii, 10 tu vinatosha kubwa kiwanda kimoja labda Dola Milioni 50, hivyo ndiyo unaongelea viwanda, ambavyo vinakwenda kujibu masuala mazima na maslahi ya wakulima wetu watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo kuhusu *Irrigation* (skimu ya umwagiliaji) hapa wewe mwenyewe umesema na watu wote wanajua baada ya muda siyo mrefu, au tuseme sijui mwaka huu sijui mwakani watu wa hali ya hewa wanasema kutakuwa kuna shida kubwa sana ya hali

ya hewa. Njaa inaweza ikatokea jua kali sana hakuna, lakini majibu makubwa hapa ni kwenye skimu ya umwagiliaji tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Jimbo la Msolwa kwa mfano na hii uchukue kama mpango Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wenzako, tukijikita sana kwenye kilimo cha umwagiliaji, mimi nina skimu za umwagiliaji saba lakini nimshukuru hata Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara yote ya Kilimo. Wamepita pale kwenye skimu moja ya umwagiliaji pale Nyida wamechukua na ninaamini kabisa katika mpango huu na fedha wa mwaka huu, Mheshimiwa Bashe alikuja Naibu Waziri namshukuru sana amejitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* tukiwa na mpango mzima wa skimu ya umwagiliaji ndani ya Jimbo la Solwa na maeneo yote yenye *advantage* kubwa ya kilimo, maana yake nini, tunaweza tukalima hata kwenye wakati ambapo msimu siyo mzuri jua kali wewe pale skimu ya umwagiliaji ipo, bwawa lipo, mnafungulia watu wanalima. Angalau tunaweza tukawa na wakulima wanaweza wakalima kwa wakati wowote ule bila kujali kuna jua ama mvua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuende kwenye wakati huo na kwenye eneo hili la skimu ya umwagiliaji ndiyo tunakwenda kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilikutaja Mheshimiwa Mohamed Said Mbunge wa Konde na utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kajage.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu kuweza kusimama leo katika Bunge lako Tukufu hili, ikiwa ni mara ya kwanza kwangu mimi kuweza kusimama na kuzungumza na mimi kutoa mchango wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ningependa kuanza na kutoa shukurani kwa sababu, mimi ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili. Ningependa kuwashukuru kwanza wapiga kura wangu wa Jimbo la Konde kwa kunichagua kwa kura nydingi sana, walinipa ushindi wa asilimia 72 katika uchaguzi ambao ulifanyika wa marudio nawashukuru sana. Pia ningependa kushukuru chama changu, Chama cha ACT-Wazalendo kwa kuniamini na *kuni-support* mpaka kufikia ushindi huo ambao leo nimepata heshima kubwa ya kuwa Mbunge katika Jimbo la Konde, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote mimi nimekaa hapa kwenye kiti baada ya msiba wa marehemu Kaka yangu Khatib Said Haji, Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho yake peponi. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe pia kwamba ulikuwa unawasiliana na familia kwa ajili ya kusimamia matibabu ya Mheshimiwa Marehemu Khatib Said Haji. Yale mawasiliano uliyokuwa unafanya ulikuwa unafanya na mimi na niliziona juhudzi zako. Kwa niaba ya familia tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru Serikali mbali ya juhudzi ulizozifanya wewe, tulikuwa tukipata mawasiliano kupitia Serikali. Kwa ajili ya kuhakikisha mpendwa wetu yule maisha yake yanaokoka lakini kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu ilikuwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu alimuhitaji zaidi. Kwa hiyo, kwa hali hiyo nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuishukuru Serikali kwa kuendesha uchaguzi wa marudio wa Jimbo la Konde. Uchaguzi ambao ulikuwa ni mfano wa kuigwa, uchaguzi ambao ulionesha kwamba Tanzania tunaweza kufanya uchaguzi wa demokrasia, demokrasia ikashika nafasi yake na watu wote wakafurahia matunda ya demokrasia. Kwa kweli naipongeza sana Serikali kwa kufanya uchaguzi

ule ambao hata kunguni hakuuliwa wala hakuguswa. Ahsanteni sana Serikali kwa kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kumshukuru pia Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na kumpongeza sana, katika hotuba yake ambayo alionesha dhahiri ana nia ya kusimamisha demokrasia katika nchi yetu pale alipokuwa kwenye kumbukizi ya maisha ya Marehemu Maalim Seif Shariff Hamad. Namshukuru sana na ninamuomba, aendelee na nia hiyo hiyo ya kusimamisha demokrasia ili Tanzania tusiwe ni wahanga wa demokrasia tuwe tunafurahia matunda ya demokrasia. Kwa hiyo, ningependa kushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo nije kwenye mpango. Mimi natoka Visiwa vya Zanzibar ni Mbunge kutoka visiwani. Uksiklia Visiwa ni kwamba tumezungukwa na bahari. Bahari sasa hivi imekuwa ikimeza visiwa kila uchao, visiwa vimekuwa vikimegwa kupitia bahari. Hili lipo katika sehemu ya mazingira. Ukija kwenye Jimbo langu la Konde nimezungukwa na bahari kupitia sehemu zangu za Msuka, Makangale, Tondoni, Mnarani kote ni bahari tupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahari imeshakula karibu nusu kilomita ya eneo la ardhi katika Jimbo langu. Sasa, nikija kwenye mapendekezo ya mpango napendekeza kwamba, katika Jimbo langu kuna kilimo kikubwa sana cha mwani, kilimo hiki mwenzangu Mheshimiwa Omar alikizungumzia jana lakini mimi nitakizungumzia katika eneo tofauti. Nitazungumzia katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni kwamba, kilimo cha mwani ni kilimo ambacho kinalimwa baharini na unapolima kilimo cha mwani maana yake bahari unaifanya ikimbie katika eneo la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiki kilimo ni kilimo ambacho Serikali inatakiwa kukiangalia sana na kukipa nguvu kubwa ili kuokoa ardhi kuliwa na bahari. Lakini lingine katika kilimo hiki unapolima kilimo hiki maana yake kunapatikana mazalia ya samaki, pia ni faida kubwa sana nimeona katika mpango, tunategemea kupata meli nane

za uvuvi pia kama tutakuwa tuna mazalia wengi sana ya samaki, maana yake hizo meli za uvuvi ndio zitawenza kupata kazi. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri katika mpango wako uweke kipaumbele katika kilimo cha mwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikihami katika sehemu hiyo nakuja katika kukuza mapato. Katika mpango umetueleza kwamba mapato yameendelea kukua kwa asilimia 7.2 ni kweli kwa *data* ulizondo wewe ni hivyo, kama tunavyojuu njia kuu ya mapato ya Serikali ni *TRA*, *TRA* ndiyo wanakusanya mapato kwa asilimia kubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge liliopita *TRA* walilalamikiwa sana kwa kufanya makadirio ambayo yalisababisha wafanyabiashara wengi kufunga biashara zao. Sasa hawa *TRA* wamekuwa kama vile sjui nisemeje mimi. Maana yake wakati ule walilalamikiwa kwa kutoa makadirio makubwa, kuwalazimisha wananchi kodi ambazo hazina msingi, sasa wamehama katika *stage* ile wamewachenga kidogo wafanyabiashara, sasa hivi wameleta *e-filing*. *E-filing* maana yake mfanyabiashara atapeleka ripoti zake kwa kutumia mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *e-filing* tuelewe kwamba wafanyabiashara wengi hawana uelewa wa mambo ya mitandao. Wafanyabiashara wetu ni wale ambao wameshindwa na maisha wakaamua kujilingiza katika biashara. Sasa basi *e-filing* walivyoileta wameweka mambo ambayo ni ya ajabu ambayo hayamsaidii mfanyabiashara. Kwa sababu, kama walikuwa na shida ya kukusanya mapato kwa kutumia *system* hii ni sawa, lakini kwanza wangetoa elimu kwa wafanyabiashara hili halikufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili wameingiza...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Said, Mbunge wa Konde. Nakushukuru sana kwa kunikumbusha, kumbe ndiyo tulikuwa tukishughulikia pamoja katika kuhangainka na ndugu yetu huyu Khatib Said Haji, Marehemu, lakini basi ndiyo hivyo. Nakumbuka sana alivyokuwa akiwasiliana nami, yeye mwenyewe akiniambia Mheshimiwa Spika, niokoe, nakufa mwenzako. Wakati huo halii imekuwa ngumu pale Muhibili, lakini sasa *Covid* ilivyokuwa, tusingeweza kumpelea India. Hapakuwa na namna ya kutoka, wala namna ya kuingia India wa mahali pengine. Kwa hiyo, ni mipango ya Mwenyezi Mungu.

Ahsante, karibu Bungeni tuendeleze kazi.

Waheshimiwa wabunge, kabla hatujaendelea, nilitaka niwaambie, Mheshimiwa Mkuchika yupo hapa kwa nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa hayupo nasi siku mbili tatu hizi. Kwa hiyo, kwa *issueszozote*, basi tumpelekee Mheshimiwa Mkuchika Mzee wetu, tumpe ushirikiano.

Mheshimiwa Dkt. Alice Kajage utakuwa mchangaji wa mwisho, halafu Mheshimiwa January Makamba. (*Makofii*)

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kuweza kusimama na kuchangia. Pia naungana na wenzangu wote kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali yake kwa jinsi ambavyo anafanya kazi kwa umahiri mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakushukuru wewe kwa kuniruhusu kuchangia mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi wa mpango huu na bajeti hii ya mpango wa maendeleo wa mwaka huu 2022/2023 ambao ni mpango wa pili katika Mpango wa miaka mitano wa 2021 mpaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina sababu zote za kumpongeza pia Waziri wetu wa Mpango na Fedha na timu yake yote; na vile vile nampongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye mapendekezo ya Mpango, eneo la vipaumbele vya Mpango. Kwenye eneo hili kuna mambo mengi sana, lakini mimi naomba nichangie kipengele cha kuchochaea uchumi shindani na shirikishi. Hapa yapo mambo mengi yamezungumzwa, mazuri sana. Kuna suala zima la mapinduzi ya TEHAMA, tunawapongeza Serikali imewezesha kabisa kuanzisha mfumo wa Taifa wa anuani za makazi, *pilot study* ikiwa Mwanza, lakini mimi nitajikita kwenye suala zima la kuimarisha miundombinu na mifumo ya kitaasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna suala zima la kuboresha mifumo ya kiutawala na Menejiment ya Utumishi wa Umma na Mifumo ya Utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi. Ukiangalia kwenye mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi, inaonekana kwamba kipaumbele cha kugharamiwa itakuwa ni masuala mazima ya miradi ya maendeleo, sensa ya watu, mishahara, deni la Serikali na huduma za jamii, yaani maji afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kwa sababu Serikali sasa imekuja na jambo zuri sana, imekuja na suala zima la mfumo wa kuwezesha mifumo kuweza kubadilishana taarifa. Hili ni jambo kubwa limeanzishwa, labda kama watu wengine hawafahamu. Huu mfumo utawezesha mifumo yote kuingiliana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Serikali ishafanya *pilot study* na mifumo mengine, kama mifumo mbalimbali ya taasisi mbalimbali kama *NIDA*, *BRELA*, *NHIF*, *TAMISEMI* yenye, Ofisi ya Ajira, Hazina kwenye *payroll*, kote sasa hivi imefanya *pilot study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumzia hilo? Kuna suala zima la kuhusisha mifumo hii ili kusaidia utumishi

na wananchi. Kwa nini nasema hivyo? Serikali sasa hivi imeanzisha mfumo wake wenyewe wa taarifa za utumishi na mishahara. Zamani tulikuwa tunatumia Lawson ya wageni, sasa hivi tuna mfumo unaitwa *Human Capital Management Information System*. Kwa hiyo, Serikali ina mfumo wake wenyewe. Kupitia huu mfumo, kuna taarifa zote za watumishi. Kwa hiyo sasa, mfumo huu unaingiliana na mfumo huu mkubwa ambao umeanzishwa ambao utakuwa unawezesha mifumo yote kubadilishana taarifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauzungumzia kwa sababu gani? Ni kwa sababu mfumo huu utasaidia sasa, kwa mfano mtumishi anatarajiwaa kustaafu mwakani, kwenye taarifa zake kwenye mfumo zinaonekana. Kwa hiyo, moja kwa moja mfumo utapeleka kwenye mfumo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambao wameshaunganisha. Kwa hiyo, moja kwa moja mtumishi atakuwa hana shida tena kuanza kutafuta *documents*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyowahi kusema, mtu kaajiriwa Kigoma kaja kustaafu Kibaha; kwa hiyo, sasa hivi huu mfumo utakuwa unarahisisha kwani taarifa zote ziko pale. Kwa hiyo, kama anataka *information* kutoka *NIDA*, inakuja kwenye ule mfumo ambao unawezesha mifumo ya kuwasiliana; kama inatoka kwenye *NHIF*, inakuja pale. Kwa hiyo, mtumishi sasa atakuwa hana shida tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiishi hapo tu. Huu mfumo unaendelea, kuna suala zima limeanzishwa linaitwa e-mfejesho. Nazungumzia suala la Serikali kuhudumia wananchi kupitia hii mifumo. Sasa hivi huu mfumo ulioanzishwa na umeanza kufanya kazi, unamwezesha mwananchi wa kawaida kuleta malalamiko yake, mapendekezo, pongezi na ushauri kupitia simu ya kawaida tu, *massage* au kupitia *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukasema kuna tatizo la TEHAMA, lakini ngoja nikwambie; naipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Mama Samia sina wasiwasi wa *speed* yao ya kuongeza mifumo ya mawasiliano. Kwa nini nasema

hivyo? Mpaka sasa hivi tumeona katika mwaka huu wa Mpango unaoishia, kumeweza kufungwa mkonga wa Taifa wenye kilomita 409, utaunganisha kutoka Msumbiji mpaka Mtwara; na pia mkongo mwingine ambao umekamilishwa ni wa kutoka Namanga mpaka Arusha. Hii inaonyesha jinsi Serikali ina dhamira kabisa ya kuhakikisha kuwasiliano yanapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la mwananchi wa kawaida kuwasiliana na Serikali au kupitia *internet*, baada ya muda kwa *speed* ninayoiona kwa ufanyakazi wa Mheshimiwa Mama Samia na Serikali yake, tutakuwa hatuna shaka. Kwa nini nazungumzia suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali au bajeti inayokuja iseme suala la kuwezesha huu mfumo. Ni mfumo muhimu sana ambao utaleta *harmonykule* chini kwa watumishi wetu. Kwa sababu kama mfumo utaweza kuwasiliana na mifumo ya hifadhi ya jamii; sasa hivi naishukuru Serikali kusema kweli, wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Serikali sasa hivi imeweza kulipa mafao shilingi trillioni 1.5, imelipa *pension* shilingi bilioni 449 mpaka sasa; na mpaka sasa hivi Serikali imeanza mchakato wa kuhakikisha kwamba unalipa Hati Fungani maalum zisizo taslimu kiasi cha shilingi trillion 2.1. Hata kama hajjalipa zote, lakini unaona nia njema ya kuendelea kulipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa mama Jenista hapa anapambana kila siku ya vikao vyta wafanyakazi pamoja na taasisi tusimvunje moyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, nia ya Serikali ni njema...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice pokea taarifa.

## TAARIFA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyozungumzwa hapa mapema ambayo inajibowi, iliyozungumzwa Mheshimiwa Bulaya, inayojibiwa na mtu ambaye hatakiwi kujibu, ni hivi, kwa mujibu wa hesabu jumuifu za Taifa, kama ambavyo imekuwa *reported* na CAG kwenye *report* iliyotolewa Machi mwaka huu, madeni ya mifuko kiujumla wake, kama inavyokuwa *reported* 2017/2018 ni shilingi trillion 19. Kwa hiyo, hoja hapa ni kwamba, kama umechukua fedha za mifuko shilingi triliioni 19, unakuja kwenye Mpango unatuambia shilingi triliioni mbili, tena inahusu *pre-1999* ambapo kwenye *pre-1999* mlikuwa mnadaiwa shilingi triliioni saba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Menyekiti, kwa mambo haya, tusifanyie mzaha. Imefika kipindi sasa mifuko inabidi makusanyo yao kwa mwezi ndio wanalazimika kulipa *pension* na hayatoshi, inabidi wakatafute kwingine. Kwa hiyo, hakuna mtu mwenye nia mbaya, hakuna mtu ambaye hatambui, kwa sababu tunasema tunatambua hicho kidogo kilichofanyika, lakini kuna mzigo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuipokea tu kiroho safi. Hapa hatutafurani mchawi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Taarifa hiyo Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage unaipokea?

**DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii siipokei kwa sababu mimi nipo katika ku-*support* na kuona nguvu ya Serikali inayofanyika kutatua *whether* ni shilingi triliioni 20 au shilingi triliioni 30, lakini nia thabiti ya Serikali tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

## TAARIFA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa anayezungumza, kwanza hakuna nia njema yoyote ya Serikali hapa. Hiyo shilingi triliuni mbili ya *non cash bond* kwenye shilingi triliuni saba, huu ni mwaka wa 22, tangu mwaka 1999. Hakuna nia nzuri ya Serikali. Serikali yenye wehaijapeleka michango, inadaiwa deni sugu shilingi bilioni 171. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage unaipokea?

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali inapokuja na Mpango huu ioneshe nia thabiti na kwa mapema sana kuhakikisha kwamba ina-support mfumo huu... (*Makof!*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alice Kaijage pokea taarifa kutoka kwa Waziri wa Nchi.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na Mheshimiwa Mbunge anayechangia kwamba nia njema ya Serikali inaonekana kwa sababu, kama nia njema ya Serikali haingekuwepo, hatungefanya utathmini wa hiyo mifuko kuangalia

sustainabilityyake; lakini kama nia njema ya Serikali ingekuwa haionekani, hatungehimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii, kazi ya mifuko hiyo kwa mujibu wa sheria ni kuandikisha wananchama, kukusanya michango, kufanya uwekezaji na kulipa mafao ya wananchama. Kwa hiyo, ili haya mambo yote yatimie, ndiyo maana Serikali kila jambo linalotokea ambalo ni hatarishi, linaloweza kuizamisha sekta, Serikali imekuwa ikisimama imara kufanya marekebisho na kuhakikisha kwamba sekta inaendelea kuwa salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli nia ya Serikali ipo. Kila tatizo ni lazima tupambane nalo ili kuweka ustawi wa sekta kwa ujumla wake. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt Alice Kaijage, unapokea hiyo taarifa.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili taarifa hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme kwamba Mpango utakapofika, bajeti ioneshe nia njema na kwa haraka ku-support mfumo huu ambao utawezesha mfumo yote kuwasiliana. Utarahisisha wafanyakazi kuhudumiwa na Watanzania kwa ujumla. Tumeona Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ameanzisha ile "Sema na Waziri wa Utumishi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimeshawasiliana kwa simu, inawezekana. Kwa hiyo, Watanzania wataweza kuwasiliana na matatizo yao yatakuwa solved haraka na pia ina uwezo wa ku-counter checkkwamba aliyeomba swalilake au hoja yake imejibowiwa, anaona. Kwa hiyo, huyo ambaye hajajibu kama ni mtumishi mtendaji anawajibishwa. Kwa hiyo, ni jambo jema sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba bajeti itakapokuja ihakikishe kwamba imechangia au imewezesha mfumo huu mkubwa ambao utawezesha mifumo yote kubadilishana taarifa, uko vizuri na umeimarika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa tunahamia upande wa Serikali na tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha moja kwa moja kabla ya mtoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa nazungumza kwa mara ya kwanza tangu nipate heshima ya kushika nafasi hii, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini katika nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakushukuru wewe kwa uongozi na ushauri wako katika kipindi hiki cha siku takribani 58 ambazo nimeduwa katika nafasi hii. Nakushukuru sana na naishukuru Kamati yako vile vile kwa miongozo mbalimbali na ushauri mbalimbali ambao umefanya mpaka tumeweza kufika hapa siku ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge kadhaa wamechangia katika Mpango kuhusu mambo yanayohusu sekta ya nishati. Kabla sijajibu, naomba nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Mpango ambao ni mzuri, unaotoa dira, pamoja na uwasilishaji na michango mizuri iliyotoka kwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo matatu ambayo ningependa kuyazungumzia ambayo yalichangiwa na Wabunge kwenye Wizara yetu. La kwanza kubwa ni suala REA. Tunaelewa kwamba usambazaji umeme vijijini ni jambo kubwa, ni jambo ambalo linagusa maisha ya Watanzania wengi, karibu Wabunge wote wana hoja na maswali kuhusu

umeme katika maeneo yao. Sisi katika Serikali tunatambua umuhimu wa jambo hilo, sasa tumejipanga upya kuhusu utaratibu bora zaidi; wa kwanza, kuwapa taarfia Waheshimiwa Wabunge kuhusu miradi iliyopo katika maeneo yao; pili, kutengeneza na kutafuta rasilimali kwa maeneo ambayo bado hayajapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na changamoto kubwa sana ya takwimu ikiwemo *classification* ya wapi ni kijiji? Wapi siyo kijiji? Kwa hiyo, changamoto imetusabaishia tuwe na namba tofauti kuhusu idadi ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho tumeamua na kwa ridhaa yako, naomba rasmi kwamba katika Bunge la mwezi wa Pili, tutawaita Wakandarasi wote hapa Bungeni, tutakuwa na maonesho ya siku tatu kule nyuma, kila Mkandarasi wa kila Mkoa atakuwa na meza; na sisi wote tutahamia hapa ikiwemo ofisi nzima ya *REA* pamoja na Wizara; tutafanya semina kuhusu suala hili na kuhusu mpango wetu mpya.

Waheshimiwa Wabunge maswali yao yote yatajibisha hapo hapo kuhusu kule ambako umeme haujaenda, umechelewa, unasuasua na unatarajiwa kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanaamini kwamba tukilifanya hili jambo kwa wakati mmoja, hata tukikaa hapa wiki nzima kujibu maswali, kero na maoni na ushauri wa Wabunge kuhusu *program* hili mpya ambayo tunakuja nayo, basi itasaidia kama namna bora zaidi ya kubadilishana taarifa kati yetu sisi na Wabunge, lakini pia itatusaidia zaidi katika kukusanya takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi atunafahamu kwamba umeme hautumiki na Kijiji, umeme unaatumika na watu. Kwa hiyo, takwimu za kijiji ni nzuri zinatupa *milestone* kwamba tume-cover maeneo ya kiasi fulani; lakini mtu ambaye hajapata umeme nyumbani kwake na haujamfikia, takwimu kwamba umefika kijiji kwake, siyo takwimu ya maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaelewa na mwelekeo mpya ni kupima nyumba zinazohitaji umeme na ambazo hazijapata umeme. Huko ndiko tunakokuja. Tunafahamu kwamba tuna idadi ya vitongoji hapa nchi 64,000; vitongoji viliviyopata umeme ni 27,000 tu na vitongoji zaidi ya 37,000 na kadhaa huko havijapata umeme. Kwa hiyo, tunakuja na mradi mkubwa zaidi ambao bahati nzuri wenzetu huko nyuma walishaanza nao kuuzungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba mahitaji ya rasilimali ni makubwa, ili vitongoji vyote 37,000 vipate umeme, tunahutaji shilingi trilioni 8. Tunafahamu kwamba haziwezi kupatikana kwa wakati mmoja, lakini *support* ya Bunge hili ni muhimu sana ili tuweze kupeleka umeme kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba atukutane mwezi wa Pili, tutakuwa na semina na maonesho ya muda mrefu. Kila Mbunge atajibuwa maswali yake yote kuhusu umeme katika maeneo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lilirozungumziwa ni kuunganisha mikoa iliyobaki kwa gridi. *Plans zipo*, mipango ipo na tumeielezea; Mkoa wa Rukwa, Kigoma, maeneo ya Mkoa wa Kagera pamoja na Mkoa wa Katavi. Tunaamini kwamba mpaka mwaka 2024 mikoa yote itakuwa imeunganishwa kwenye gridi ya Taifa kwa miradi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la mwisho nizungumze hili kubwa lilirozungumzwa na Mheshimiwa Ester Bulaya la mradi wa Julius Nyerere. Sasa sisi tulipata barua ya tarehe 3 Septemba, kutoka Ofisi ya Bunge kwamba, Kamati ingependa kupata taarifa ya tulipofikia. Tulileta taarifa hiyo ipo kwenye mtandao wa Wajumbe wa Kamati na naamini Mheshimiwa Bulaya amepata taarifa hizo huko. Kwa hiyo, ni kweli kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani iliupokea mradi huu ukiwa umechelewa kwa siku 477.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tumefikia wapi kwa kila kipengele cha mradi kwa asilimia, hazina maana sana kwa sababu zinabadilika kila siku. Hata siku ya leo kuna kazi inafanyika, maana yeke ni kwamba, nikikupa asilimia leo, wiki ijayo zitakuwa ziko tofauti. Ni kweli mradi una changamoto ambazo alipokuja Mheshimiwa Makamu wa Rais kuutembelea alizieleza na sisi tulipokutana na Kamati ya Bunge pia tulizieleza. Ni changamoto za kawaida kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya namna hii. Changamoto hizi hazifanyi mradi huu uonekane hauna maana. Changamoto hizi haziwezi kuturudisha nyuma wala katuondoa katika nia ya kuutekeleza mradi huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naambiya kuna *airport* kubwa kule Ujerumani imechelewa miaka, akataja miradi mikubwa ya kimkakati katika nchi zilizoendelea ambayo imechelewa. Kuchelewa kwa mradi ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali tumechukua hatua pale ambapo kulikuwa na uzembe hatua zimechukuliwa kwa upande wa *TANESCO* na Wizarani, hizo ni changamoto za upande wetu. Kwa upande wa mkandarasi, mkataba baina yetu na mkandarasi unayo tiba kuhusu changamoto za ucheleweshaji na sisi tunafuata tiba hiyo. Tumeanza vikao na mkandarasi kuhusu namna ya kumaliza changamoto zilizopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba, mazungumzo yanaendelea kati yetu na mkandarasi ambayo yana misingi minne. Kwanza ni kupunguza hizi siku za ucheleweshaji kutoka 477 zilizopo sasa na kujaribu kuona kama tunaweza tuka-squeeze tukaharakisha baadhi ya maeneo zikawa chache zaidi. Msingi wa pili, ni kuzuia kusiwe na ucheleweshaji zaidi. Msingi wa tatu, kazi ifanyike kwa ubora na viwango vinavyotarajiwa na msingi wa nne, kusiwe na ongezeko la gharama kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, mazungumzo yetu na mkandarasi yako katika misingi hiyo minne. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie kwamba, kauli aliyotoa Mheshimiwa Rais hapa Bungeni kwamba, miradi yote hii mikubwa ya kimkakati lazima itakamilika na lazima itatekelezwa. Naomba kuchelewa kwa mradi kwa siku 477, naomba nirudie kusonekane kwamba, ni tatizo litakalouua mradi huu. Sisi tumejipanga vizuri sana kuhakikisha kwamba, tunautekeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe ambayo inazungumzwa sana ni tarehe inayokaribia ya kujaza maji kwenye bwawa. Kwa sababu, ilizungumzwa hapa Bungeni na nimeona *clip* inazungumza, ngoja nilitolee ufanuzi kwamba, ilisemekana kwamba, tarehe 15 Novemba, basi maji yataanza kujazwa kwenye bwawa lile. Si ajabu kwa kadiri siku hii inavyokaribia itakuwa ni habari kubwa ambayo inaweza kutumika kuuchafua mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, tarehe hiyo itapita kabla hatujajaza maji na sababu ni mbili. Ili ujaze maji kwenye bwawa lazima masharti mawili yatimie; lazima uwe umejenga tuta kuu ambalo ni *main dam*, ule ukuta mkuu wa kuzuia maji kwa mita 95 juu ya usawa wa bahari, lile tuta linapaswa kuwa na mita 190 juu ya usawa wa bahari. Sasa ili uanze kujaza maji lazima uwe umefikia mita 95. Mpaka leo bahati nzuri tumeshapita mita hizo 95 juu ya usawa wa bahari kwa hiyo, sharti la kwanza la kujaza maji tumelifikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sharti la pili, ni kwamba, wakati tunajenga hili tuta kuu tulijenga njia ya kuchepusha mto pembeni, ili tupate nafasi ya kujenga. Sasa ili sasa ujaze maji lazima uzibe lile handaki ulilolijenga kuchepusha mto. Sasa ili uzibe lile handaki unahitajika milango mikubwa na vyuma takribani 14 na kila kimoja kina tani 26, ni machuma makubwa ya kuzuia lile handaki ili mto usiendelee kuchepuka wakati unajaza bwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile milango imefika, lakini inahitaji *crane* kuibeba na kuziba, ile *crane* lazima itoke nje na *crane* hiyo haijafika bado. Kwa hiyo, tumetimiza sharti la kwanza la kujaza maji, lakini sharti la pili la kutuwezesha

kuziba ule mchepusho hatujalifikia. Kwa hiyo, kwa hali na mwenendo hatutaweza kujaza maji kwenye bwawa kabla ya mwezi wa Machi. Tutawapa tarehe mahususi ya kuweza kuanza kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya nikiamini kwamba, sisi ni viongozi katika Bunge hili, mradi huu ni wakwetu, ni mradi wa kimkakati, kufanikiwa kwa mradi huu ni kufanikiwa kwa nchi. Kicheko au kejeli yoyote kwa kuchelewa kwa mradi huu haimsaidii mtu yejote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekwishatokea kwamba, katika *project management* yoyote na katika miradi mikubwa haya mambo hutoke. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba, sisi tutashirikiana na tutaomba ushirikiano wa Bunge lako kuhakikisha kwamba, malengo yaliyowekwa ya mradi huu yanatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kulizungumzia hili. Sasa hatuko hapa kumlaumu mtu, kazi hii tumepewa sisi ambao tumeteuliwa na tutaifanya kwa nguvu, uwezo na maarifa yetu yote kuhakikisha kwamba unakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho la *LNG*; naomba niwahakikishie Watanzania kwamba, mradi huu mkubwa kabisa wa kimkakati wa jumla ya shillingi trillioni 70, jana tumetengeneza historia kwa kuanza mazungumzo na makampuni ya mafuta na gesi. Kwa hiyo, nchi yetu itaenda kupata manufaa makubwa sana katika miaka ijayo kwa kuvuna gesi yetu kwa matumizi ya kuuza nje, lakini pia kwa ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Lindi na Kusini na Watanzania wote, tutapata nafasi ya kueleza fursa zitakazopatikana wakati wa utekelezaji na pia tutakuwa wawazi kuhusu mfumo wa mapato yatakayotokana na gesi hii na jinsi ambavyo nchi yetu na uchumi wetu utafaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisitumie muda mrefu. Nafahamu yako mengi, tutayazungumza kwa kadri

siku zinavyokuja ikiwemo mabadiliko ya mfumo wa uuzaji na ununuzi wa mafuta nchini ili kuweza kutoa nafuu kwa watumiaji wa dizeli na petroli na mafuta ya taa nchini, hatua ambazo nadhani mmeanza kuziona. Mengi na mazuri yatakuja katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Januari Makamba, Waziri wa Nishati. Tunakushukuru sana kwa maelezo hayo na ufanuzi wa kina.

Nilikuwa napokea taarifa hapa fupi, kuna gari la Mbunge mwenzetu ambalo mchana wa leo limeungua na kuteketea lote maeneo ya kule Kongwa. Nadhani alikuwa anakuja, ni Mbunge wa Jimbo la Mtoni, Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma. Ni matatizo ya umeme kwenye *engine*, maana haya magari tunayochukuachukua haya baada ya fungu kuwa dogo ndio mambo yake hayo.

Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha. Karibu sana, una dakika 10 pia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili niweze kuchangia kuhusiana na Mwongozo wa Mapendekezo ya Mpango. Naomba nianze mchango wangu kwa kugusia eneo la kilimo ambapo Waheshimiwa Wabunge takribani wengi sana walilizungumza kwa hisia kali, ukiwemo na mwenyewe na msisitizo wako katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukiri juu ya umuhimu ambao Waheshimiwa Wabunge wameuonesha wa kulitilia mkazo suala la kilimo zaidi katika Mpango wetu. Kwa hiyo, kama Serikali tumelichukua jambo hili kwa uzito wa aina yake na kwa kuwa, huu ni mwongozo basi niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, pale ambapo Mpango utakapowasilishwa utakuwa umetilia maanani eneo hilo kwa uzito ambao unastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati njema sana tumekuwa tukifanya kazi kwa karibu sana na Wizara ya Kilimo. Tutashirikiana nao wenzetu vizuri kabisa kupanga mpango wetu mzuri, vizuri zaidi katika eneo hili kwa kuzingatia maeneo yote. Msingi wake ni kuhakikisha kwamba, kilimo chetu kinakuwa kilimo cha biashara, kwa maana gani? Kwa maana kwamba, kwa eneo moja ambalo litasaidia katika kuhakikisha kwamba, tunajitosheleza kwa chakula chetu wenyewe hapa nchini, lakini vilevile kwa kuweka mazingira mazuri ya kuweza kusafirisha chakula hiki nje ili iweze kusaidia kuipatia nchi yetu fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maeneo ambayo tunakusudia kuyatilia maanani ni maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyazungumza. Kwa kuyataja machache kutokana na muda, eneo la kwanza ambalo tunadhani ni la msingi sana ni eneo la mbegu. Eneo la mbegu hili tutaliwekea mkakati mzuri katika mapana yake; kwanza kuhakikisha kwamba, tunashirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa *PPP*, lakini vilevile kwa kujengea uwezo taasisi zetu kwenye eneo la tafiti kwenye *RND* ili tuweze kuzalisha mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nalo vilevile ni muhimu na lenyewe tutaliangalia kwa kina ni eneo la umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza jambo hili kwa kina na hivyo tuwahakikishie kwamba, miongoni mwa miradi ya vielelezo kwenye mpango wetu ujao hili eneo la umwagiliaji tutalizingatia kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika eneo ambalo limekuwa na changamoto kubwa sana sasa hivi kutokana na changamoto ya UVIKO na upandaji wa bei za mbolea duniani, imesababisha kupanda kwa bei na hivyo basi, ni lazima kama Taifa tuje na mkakati wa muda mfupi wa kuweza kukabiliana na tatizo hili, lakini tuwe na muda wa kati na muda mrefu wa kudhibiti tatizo kama hili lisijitokeze tena. Maeneo ni mengi ambayo tutayazingatia kama ambavyo Waheshimiwa wameyzungumza. Kutokana na

muda Waheshimiwa Wabunge naomba nisiyachambue, ikiwemo masuala ya masoko, TEHAMA, ugani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata katika eneo hili ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza kwa kina sana ikiwemo jinsi gani Benki yetu ya *TADB* inavyoweza kusaidia katika eneo hili. Nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa na wengi wameyazungumza kwa uchungu kuhusiana na riba; niwahakikishie kwamba, mchakato huu hasa katika eneo la kilimo kuhakikisha kwamba riba zinashuka chini ya asilimia 10, ni mkakati ambao umeshaanza na *BOT* kwa kutoa maeneo kama matano ya kuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tayari maombi yameshapelekwa na benki kadhaa kwa ajili ya kutumia fursa hii ili riba ziweze kushuka. Bado hatujafkia katika hatua ya kusema kama *BOT* imeshindwa au hajashindwa. Naomba Wabunge waipe muda Serikali, tutaisimamia *BOT*kuhakikisha kwamba, hizi benki ama taasisi zilizoomba zihakikishe kwamba, zinatumia fursa hiyo na kutumia fursa ya kushusha riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi benki ambazo ni za Serikali ikiwemo *TADB* na benki nyingine zote, hizi tunataka ziwe ndio mfano wa kwanza wa kuhakikisha kwamba zinatenekeleza maelekezo ya Serikali. Kwa hiyo, tutazisimamia, kama kuanza kupunguza riba basi ziwe zinaanza hizi benki zetu za Serikali ikiwemo Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka nilizungumzie ni eneo la mikopo. Kwenye hili eneo la mikopo wako Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wana mashaka kwamba, pengine mikopo hii tunakopa sana; ni kweli, ni sahihi kabisa. Katika miaka ya karibuni tumekopa kwa kiwango kikubwa sana, hilo sio jambo ambalo ni la siri, ni jambo ambalo lipo dhahiri. Kukopa maana yake nini? Maana yake dhana nzima ya kukopa pale ambapo inakuwa matumizi na mapato hayaendi sambamba. Kwa maana

kwamba, mna matumizi, mna mapato halafu mna *gape* katikati ambayo inahitajika izibwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mnahitaji kufadhili miradi mingi sana mikubwa ya maendeleo ambayo itakuwa na tija katika nchi, lakini pengine mapato yakishapatikana hayakidhi kufadhili ile miradi na hili jambo sio geni kwa duniani. Nchi zote duniani zinafanya hivyo ikiwemo hato hizo nchi ambazo zimeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini ambacho tunafanya? Tunachokifanya kwanza ni kuhakikisha kwamba, katika eneo hili la mapato ama *revenue* tunafanya utaratibu wa kuwa na mikakati ya kuongeza mapato yetu kama nchi. La pili, tufanye jitihada za kupunguza matumizi ili ile *gape* iweze kupungua na hii hofu ya mikopo na yenyewe vilevile iweze kupungua mliongoni mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili eneo la kuongeza mapato kuna hatua nyingi ambazo tumezichukua na tunaendelea kuzichukua kama nchi, lakini kwa harakaharaka naomba nitaje chache:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa katika chombo kikubwa ambacho tunakitegemea katika kuhakikisha kwamba kinakusanya mapato ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). *TRA* kuna hatua ambazo tayari wamezichukua kuhakikisha kwamba, tunakusanya mapato mengi zaidi kwa wakati mmoja kulingana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika mambo ambayo Mamlaka ya Mapato inafanya ni kuhakikisha kwamba, tunaongeza vyanzo vipyta vyta mapato na mapato haya yako ya aina nyingi, kuna mapato ambayo yanatokana na walipakodi wakubwa. Niyapongeze sana maoni ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la kufanya utafiti kwenye eneo hili la mawasiliano, mashirika ya sim una kadhalika. Tumepokea haya mapendekezo na tutashirikiana

na Wizara husika ili tuliangalie. Tunaamini kwamba, eneo hili litatusaidia kuweza kupata vyanzo vikubwa vyatapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye eneo la mitandao. Kuna hoja nyngi zimezungumzwa jinsi gani tutakusanya kodi kwenye hizi huduma za mitandao. Hili lenyewe nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari linafanyiwa kazi na Mamlaka ya Mapato Tanzania, lakini na hizi jitihada ambazo Serikali imekuwa ikichukua za kuhakikisha kwamba, tunafungua fursa zaidi za uwekezaji nchini ili sekta binafsi iweze kuingia na tupate wawekezaji wakubwa, zitasaidia kuongeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la *informal sectors*; hawa watu ambao wanaitwa wafanyabiashara wadogowadogo. Tuna mikakati thabiti na juzi mmeshuhudia Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko pale Kariakoo na maeneo mengine mengi. Haya ni mambo ambayo tunafanya kama Serikali ili wale ambao wanaitwa wafanyabiashara wadogowadogo waweze kuku ana walipe kodi. Mambo mengine ni masuala ya mifumo, masuala mengi ambayo tunafanya ya kuhakikisha kwamba, *TRA* inafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyanzo vingine, mikakati ya kutafuta vyanzo mbadala vyatapato na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende harakaharaka kwa sababu ya muda, kwenye eneo lingine hili la kupunguza matumizi. Tutakapokuwa tuna njia za kuweza kupunguza matumizi kwa maana gani? Kwa maana ya kuhakikisha kwamba, mikopo ambayo tunakopa inakuwa sio mikopo ya kibiashara mpaka pale inapobidi. Kwa hiyo, kwanza tuzingatie sheria; tuna sheria kama tatu ambazo tunazisimamia, Sheria hii ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura Namba 134, lakini pia kuna sheria nyngine mbalimbali ambazo zinatuongoza jinsi ya kukopa mikopo ya kibiashara ambayo itakwenda kuwekeza katika miradi ambayo inaleta *impact* kwenye uchumi wa nchi yetu, hilo ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vipimo ambavyo vimewekwa vyा kisheria kabisa vyा kupima mikopo hiyo inakopwa viyi. Moja, ni kwa mfano kuangalia *ratio* kati ya thamani ya deni la sasa na *GDP* na nyingine kuangalia thamani ya sasa ya deni na *export*. Hayo maeneo mawili ni muhimu sana na ndio maana niungane sana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati alivyozungumza, miradi kwa mfano ya reli (*SGR*), miradi hii ya umeme, hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba, *GDP* yetu kama Taifa inakuwa, lakini vilevile na usafirishaji utasaidia kufanya tuweze kusafirisha nje bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo maana yake nini? Maana yake uhimilivu wetu kama Taifa utaongezeka. Kwa hiyo, miradi hii ya uwekezaji niwahakikishie kwamba, imizingatia sheria, lakini imeangalia miradi ambayo italeta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya msingi ni kuona kwamba, sasa tunaweza kufanya jithada na hii ndio kazi ambayo Mheshimiwa Rais Samia ameifanya kwa weledi mkubwa sana, kwamba, lazima tuweze kupata kuimarisha mahusiano yetu na taasisi za kimataifa ambazo zinatoa mikopo ya riba nafuu. Mikopo hii ni muhimu sana, juzi mmeshuhudia *1.3 trillion* iliyotolewa jinsi ambavyo imeleta *impact* kubwa sana katika nchi yetu, imeenda kuchochea shughuli za uchumi kila mahali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba hatuhangaiki kutafuta fedha zenye ghamama kubwa, masharti makubwa au riba kubwa kwa ajili ya kufanya miradi, bali miradi hiyo sasa inafanywa kwa fedha ambazo masharti yake ni nafuu mno. Kwa hiyo katika eneo la kupunguza matumizi hata kama itakapofika mahali tunahitaji tulipe deni kwa mwezi, maana yake tukilipa deni ambalo lina *grace period* ndefu, deni ambalo riba yake ni ndogo, mzigo kwa Serikali unapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kupunguza matumizi hata kama itakapofika mahali tunahitaji tulipe deni kwa mwezi, maana yake tukilipa deni ambalo lina *grace*

*period* ndefu deni ambalo riba yake ni ndogo. Kwa hiyo, mzigo kwa Serikali unakuwa unapungua.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi na muhimu ni kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika inavyostahili na hivyo basi ile hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza ni hoja ya msingi sana hoja ya kuhakikisha kwamba suala la tuliangalie kama Serikali eneo ambalo lina mapungufu na tunakiri kwamba eneo hili lina mapungufu eneo la kuangalia kuhusu eneo la sera la *M & E* ufuatiliaji na uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiandaa tukijipanga katika kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo kuna jitihada ambazo Serikali imefanya katika kuboresha ufuatiliaji na utathmini wa miradi ya maendeleo kwenye kuandaa hiyo sera ya Taifa ufuatiliaji wa tathmini, kwa kufanya mambo kadhaa. Moja ni kuandaa mfumo wa kitaifa wa kusimamia miradi ya maendeleo ambapo kimsingi utawezesha upatikanaji wa taarifa za miradi kuanzia uibuaji hadi utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jingine ambalo tunafanya ni kuandaa mwongozo wa ufuatiliaji wa tathmini ya miradi na *program* za maendeleo. Lakini kama kumbe hiyo haitoshi Waheshimiwa Wabunge walipendekeza juu ya umuhimu wa kuishirikisha sekretarieti za mikoa. Ni pendekezo zuri Waheshimiwa Wabunge pendekezo hilo tumelichukua na tutalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi maeneo ambayo nilikuwa nimejipanga kuchangia ni hayo nashukuru sana kwa hii fursa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, *Engineer Masauni* sasa nimuite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Nchemba karibu hapa mbele ili uhitimishe hoja yako tutakupa hadi nusu saa ili uweze kuhitimisha vizuri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti pamoja na wajumbe wa Kamati lakini pamoja na Wabunge wote waliochangia katika hoja hii ya leo ambayo nahitimisha muda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote baada ya hayo nitamke kwamba hoja zote zilizotolewa kuanzia hoja zilizotolewa na Kamati, hoja zilizotolewa na Wabunge, hoja zilizotolewa na Mawaziri, tumezipokea sisi kama Wizara na tuwaahidi kwamba zitafanyiwa kazi na tutakapokuja na *draft* nyingine ya Mpango ambao utakuja kwa hatua nyingine tutakuwa tumejumuisha na maoni hayo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nikuombe na Waheshimiwa Wabunge watuamini na hatutaweza kuiongelea hoja moja baada nyingine kwa sababu hoja hizo zilizotolewa ni nyingi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo machache tu ambayo nitaomba uridhie niyagusie ni yale ambayo yanahitaji ufanuzi yale ambayo tumepewa maoni na tumepewa ushauri tutachukua na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na eneo hili hili ambalo limejadiliwa muda siyo mrefu ambalo ilikuwa linaongelea masuala ya madeni kwa wastaifu. Kwanza kwa mtu akisema Serikali haina nia njema na madeni haya ya wastaifu itakuwa ni bahati mbaya sana na atakuwa hata hajazingatia kwamba hata hilo deni kiini chake kilitoka wapi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni haya ambayo tunaongelea leo mengine ilikuwa ni hiyari ya Serikali tu kwamba tunaenda kuwalipia watumishi wetu na yalichukuliwa Serikali ilikubali kubeba mzigo ili iwalipie watumishi wake. Katika hilo si kwamba tangu muda ule hamna kinachofanyika Serikali imeshafanya ni vile kwamba

kulikuwepo na *accumulation* kubwa lakini Serikali imeshafanya na imefanya kwa kiwango kikubwa tu ambacho kinastahili kupongezwa na ukichukuliwa jinsi ambavyo Serikali inafanya inatakiwa iweke matumaini kwamba hili ni jambo ambalo linaenda kukamilika na katika suala la muda tutaweza kufika katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku ambazo si nyingi sana tayari *PSSF* walishapewa bilioni 500 kwa ajili ya jambo hilo hilo na *NSSF* walishapewa bilioni 100 na katika kipindi cha ndani ya miezi mitatu kwenda minne iliyopita tuliongezea bilioni 50 nyingine kwa ajili ya masuala hayo hayo ya kuwalipa wazee. Na hata hii tuliyosema tunafanya *noncash bond* labda hii taaluma na yenyewe labda iwe na shida watu hawajui hii ni *float* ya kwanza tume-*float* ya kwanza kwa kiwango hicho na siyo ya mwisho tuna *float* ya kwanza kwa kiwango hicho na siyo ya mwisho. Tuna *float* ya kwanza tunaitekeleza halafu tuna-assess imefanyikaje tuna-assess deni halafu baada ya hapo tunaendelea na utekelezaji ule ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wengine wanaolalamika sana ni vile tu Bunge lako si kiwanja cha utani ingekuwa kiwanja cha utani hawa wangkuwa watani zangu ningeweza kukwambia wao wanadaiwa nini hata wao binafsi waone suala la madeni huwa likoje na hata sasa wanatamani uwaruhusu hata *gratuity*. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapoongelea haya mambo kwa mwingine ambaye anafanya jukumu kubwa tusiwe tunasahau undani wa mzigo wenye unavyokuwa Serikali imeshafanya jambo kubwa na itaendelea kufanya jambo kubwa na katika kipindi ambacho tayari Serikali imechukua hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatua ambazo zimewabadiilishia maisha wazee hao ni jambo kubwa ambalo limefanyika ambalo halipaswi kubezwa ilikuwa ikitokea Bunge inaendelea kama hivi unakuta wazee wengine wako misikitini wengine wako makanisani wengine wako tu wamehifadhiwa

mahali hivi. Lakini baada ya utaratibu huu wa kuanza kutoa hizo fedha tena kwa mtiririko tena kwa ukaribu karibu jambo hili limeanza kubadilika pakubwa na tunaamini baada ya hatua hii kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri anaifanya kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kukamilisha masuala ya kikokotoo tutaongeza zaidi kasi na tutaenda kulifanyia jambo hili ambalo lilikuwa tatizo kuwa ni historia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine hiki kinatajwa tu kwamba *CAG* amesema deni ni trilioni 19 hii ni namba na watu wale wale *CAG* yule yule aliposema madeni yanayodaiwa na *TRA* ni trilioni 360 walisema hii haiwezekani kwamba hizi ni namba tu *CAG* kazitaja tu kwenye hii hapa namba hii hii wanaona hiyo ndiyo namba tu. Lakini niwaambieni kila kitu kinachoitwa deni yanafanyika *verification* na yale ambayo yameshakuwa *verified* yanafanywa malipo na hilo ni jambo ambalo litafanyika na litakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeomba nilisemee kwa uzito mkubwa unaostahili ni hili ambalo na Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalielezea, sitaelezea katika *angle* ambayo tayari ameshafafanua hili jambo la deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la deni la Taifa tuna orodha ndefu sana ya miradi ambayo imeshafanyika na niwaombe watanzania hasa hasa sisi Wabunge ambao ni viongozi tusianzie mbali sana twendeni tu tuanzie wakati deni la Taifa liko katika kiwango tuseme cha trilioni 10 tuanzie hapo hapo halafu tuanze kuangalia katika mwaka 1995 tuseme tuangalie katika mwaka 1995 deni lilikuwaje halafu tuangalie pia na miradi ambayo ililetwa na fedha zilizokopwa kipi tulitakiwa tukifanyie uamuzi katika mwaka huo ambapo tunaongelea deni la Taifa likiwa dogo, hatukuwa na mikoa ambayo imeunganishwa kwa barabara za lami yaani kutoka Singida kuja Dodoma hapa tulikuwa tunahitaji siku nzima. Kutoka Singida kwenda Arusha tulikuwa tunahitaji siku nzima, kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam tulikuwa na *option* ya kupita nchi mbili kutoka Kagera kwenda Dar es Salaam

tupite nchi mbili, kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi tulikuwa tunahitaji wiki kabisa. Kutoka Dodoma hapa walioingia vipindi viwili vitatu kutoka Dodoma hapa kwenda Isimani hapa ilikuwa lazima uende kwanza Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengine ni wadogo sana hawajui haya yaani ukitaka kusafiri begi kwanza mabasi yenye we begi lilikuwa linakaa kwenye *carrier* halafu mnapofika ye ye aliyemsafiri na yule utingo wote hamtofautiani ndivyo ilivyokuwa sasa *analysis* iliyofanyika ni je, tuchukue makusanyo ya fedha tujenge barabara zetu tufungue uchumi halafu tukishafungua uchumi ule utuletee fedha tuendelee kulipa madeni ndiyo uamu zi uliofanyika. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Halafu Mheshimiwa Waziri yale mabasi yalikuwa yameandikwa ukiingia mle ndani kwamba kila abiria tunza mzigo wako wa ndani ule wa kwenye *carrier* utingo atajua endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo ilivyokuwa kwa hiyo ukatakiwa ufanyike uamu zi wa makusudi tu kwamba je tuendelee na hali kama hii hii halafu na deni letu liwe dogo au tuchukue fedha tutengeneze miundombinu tufungue nchi yetu halafu miundombinu hiyo ituletee fedha tulipe deni tunalokopa. Ndiyo uamu zi uliofanyika sasa hivi baada ya njia kuwa zimeshafunguliwa sana karibu kila eneo na hii nimeongelea tu barabara lakini ni maeneo mengine mengi kwenye umeme hivyo hivyo sehemu ya robo ya nchi ndiyo ilikuwa na umeme kwingine kote ilikuwa giza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwenye umeme hivyo hivyo na sekta zingine taja na sekta taja kwenye afya taja kwingine kote uamu zi ukafanywa kwamba je, tubakie na deni dogo halafu na miundombinu yetu yote hafifu au tukope tufungue miundombinu halafu baada ya hapo tulipe? Ndicho kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna orodha ya miradi inaelekea karibu 1000 ambayo imejengwa siwezi hata kuanza kuutaja mmoja mmoja lakini kwa sababu sisi ni viongozi kila mmoja aanze kupekua mmoja mmoja ambao ana maslahi ya kutaka kufahamu aone umejengwa kwa kiwango gani umejengwa kwa *financing* gani? Imefungua nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata masuala tu ya umeme wenyewe umeme si nguzo za umeme, umeme ni uzalishaji wenyewe wa umeme imefanyika njia hizo hizo mpaka sasa hivi watu karibu nchi nzima walishazoea masuala ya umeme watu karibu nchi nzima walishazoea masuala ya mawasiliano ya simu hayo yote ni *analysis* za kufanya uamuzi halafu likafanyika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani wakati tunasoma ilikuwa umeme unakatika ukiwaka mnashangilia kama goli la simba maana yake simba siku hizi ikifunga dakika zimeshaenda watu wanashangilia mpaka nyumbani. Watu wanashangilia kumbe umeme tu umerudi umeme. Kwa hiyo, tathmini ikafanyika uamuzi ukafanyika na madeni haya yameongezeka lakini pia miundombinu ilijojengwa na fedha hizo imeongezeka tusifanye tathmini ya deni tu kama vile tumebambikwa tufanyeni tathmini ya deni huku tukifanya na tathmini ya miradi ya fedha hizo ambazo zimefanywa kutokana na deni hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengine wanaenda mbali zaidi hizo ndiyo *cheap politics* wanaenda wanasema Serikali ya Awamu ya Sita imeingia tu kwa miezi sita imeshakopa zaidi ya bilioni tisa. Jamani ndugu zangu hivi hata ibada hamfanyagi, hamuogopi hata Mungu? Mkopo wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Sita mkopo wa kwanza wa mama ni hii triliuni 1.3 ambayo imetoka *IMF* na kwa mazungumzo yanayoendelea utakuwa mkopo ambao una masharti nafuu kuliko mikopo yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mkopo wa kwanza na mpaka sasa Serikali ya Awamu ya Sita haijakopa mkopo wowote wenyе masharti ya kibiasara bado haujakopa

labda mkopo wa kwanza utakuwa wa kukamilisha *loot* ya tatu ya nne na ya tano. Sasa hata hilo ni jambo ambalo tunatakiwa tufanye tathmini tu je, tuache tu kufunga hiyo *loot three, loot four* na *loot five?* Kwa kuogopa deni? Au tupitishe bakuli maana yake hata Yanga tulishaacha kuitisha bakuli tunachukua mzigو mkubwa tunamalizia *loot* hiyo hapo tunaanza inayoenda Kigoma tunaanza inayoenda Kalemi tunakamilisha zote tunafungua fursa za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni miradi ya msingi ambayo unafanya *analysis* kama uchukue deni au uache ubaki umeufunga uchumi wako haya ni mambo ya msingi Serikali yetu haijawahi kukopa kwa ajili ya kulipa mishahara wala kwa ajili ya kujaza mafuta kwenye magari inakopa kuweka miradi ya wananchi ambao wananchi wenyewe tumeshawatengenezea kiu kila mwananchi anataka jambo lifanyike zuri zaidi katika eneo lake na hii ni wahakikishile watanzania tuko kwenye mwelekeo ambao ni sahihi na wengine walikuwa wanassema hata kwamba Serikali imetumia *reserve* zilizoachwa. *Reserve* zilizoachwa hazijaguswa na zimeongezeka sana sasa hivi tunaumiza vichwa *ku-control* mfumko wa bei kwa sababu pia fedha zinapokuwa nydingi sana inabidi muangalie na kwenye *policy aspects* za kuangalia mfumko wa bei ukooje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda mwaka 2015 *reserve* zilikuwa *dollar* bilioni 4.3 wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia wakati Serikali ya Awamu ya Tano inamaliza ilishaongeza *reserve* kutoka bilioni 4.3 kwenda bilioni 5.04. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Machi 2021 wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia, tayari imeshapandisha kutoka bilioni 5.03 kwenda bilioni 6.4 hizo ndiyo *reserve* zetu tulizonazo ni zaidi ya miezi sita ya uagizaji wa bidhaa tuko juu kabisa mbali na kiwango kinachotakiwa katika *standard* za kimataifa. Na ukienda kwenye tathmini angalieni *IMF* wanatutathmini vipi, angalieni Benki ya Dunia inatutathmini vipi halafu ndiyo hapo muweze kuangalia ni kitu gani

ambacho kinaweza kikaangaliwa ili uweze kutoa hoja kama mtu unataka kutoa hoja katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni mambo ambayo watu wanatakiwa wayafanyie tathmini fedha zingine za miradi mikubwa hii zingine zimetoka Awamu ya Tano zimeingia Awamu ya Sita zingine zilitoka Awamu ya Nne zikaingia Awamu ya Tano hatupaswi sana kuangalia tu mambo ya fedha tunatakiwa tuangalie fedha hizi zimefanya nini unajua ingekuwa jambo la msingi sana watu wangekuwa wanasema hii fedha hamjaitumia katika eneo ambalo linaleta manufaa. Hilo ndiyo jambo la msingi kuongelea ongelea fedha tu hii watani zangu hapa sijui ni akina nani unakuwa kama Wanyaturu wanaogopa kupanda karanga kwamba nalalaje ndani halafu karanga ilale nje kumbe unavyopanda karanga ndiyo utavuna nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwekeze tunatakiwa tujadiliane kuhusu tumewekeza sahihi au si sahihi hiyo ndiyo itakuwa akili ya watu wenye maarifa ya kuwaza nchi inaelekea upande gani. Siyo kila siku watu wanawaza wanaangalia namba tu halafu na wengine wanawatisha wananchi wetu kwamba unajua zitaanza kugawanywa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat anatoa macho hapa, ahsante endelea Mheshimiwa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie fedha zilikowekezwa, na jambo lingine zuri zaidi na hata Mbunge wa Mtama Mheshimiwa Nape alitoa pendekezo, pendekezo hilo sisi tunachukua kama Wizara tutafanya tathmini halafu tuangalie kama tunaweza tukaongea na taasisi halafu tufanye *refinancing* tuangalie tufanye *refinancing* ni kitu ambacho watu huwa wanafanya. Unaweza ukakopa ulikuwa na mradi una uharaka ukakopa halafu masharti yakawa yako juu sana unaangalia kama unaweza ukapata *refinancing* kwa mfano kama hivi tunasema tumepata fedha hizi triliioni moja na zaidi zikawa hazina riba halafu *grace period* miaka 10 ukiwa na fedha nyingi za aina hiyo unaondoa zile ambazo ulikuwa na *grace*

*period* ya miaka miwili na riba ya asilimia 9 halafu unakuwa na *fiscal space* ambayo unaweza ukatekeleza shughuli zingine za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo yanaweza yakaweka ahueni kwenye upande wa deni lakini pia ikatusaidia kuendelea *ku-finance* miradi ya maendeleo ambayo wananchi wetu wanahitaji kuendelea kuona maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesema tutafungua mikoa yote ambayo bado hajamaliziwa kufunguka wapi huko Mpanda kwenda Kigoma kwenda Rukwa kwenda Tabora wapi huku Lindi maeneo yale ambayo yanauzalishaji mkubwa Mtwaraji yanauzalishaji mkubwa wa korosho lakini barabara hazifiki wapi huku kwenye mbaa na maeneo mengine huku Ruvuma maeneo mengine kule Manyara na mikoa mingine mingi kwenda Simiyu huko na maeneo mengine mengi Ifakara huku maeneo mengine yote yale ambayo yanatuletea uzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesema yaangaliwe yawekwe kwenye mpango ili tuweze kufungua uchumi unajua tunapofungua uchumi tunagusa mpaka kwenye kilimo, tukifungua barabara tunagusa mpaka kwenye uzalishaji upande wa kilimo haya yote tunaenda kuyaangalia ili yaweze kufanyika kuleta tija kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwa ajili ya muda niweze kuliongea na lenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri ameshaliongelea upande mmoja nitaongelea upande mwingine ni upande wa kilimo. Eneo hili la kilimo na Waheshimiwa Wabunge tunakubaliana wote sisi hatupingani na mawazo ya Wabunge, lakini kitu kimoja tu tunachosema ambacho tumekuwa tukijadili sana na Wizara ya Kilimo na tunaendelea kuwa na uelewa wa pamoja ili tuweze kusonga mbele na tunaongelea kilimo kwa ile dhana pana ambayo inaweka na mifugo inaweka na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari ya sekta hizi siyo fupi ni safari ndefu tu ambayo tumekubaliana tu kwamba tunaanza wapi katika huo mwelekeo wetu. Kati ya maeneo haya ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kesho ama keshokutwa nadhani hata sasa hivi tunavyoongea Mheshimiwa Naibu Waziri ameniambia kuna kazi ambazo zinaendelea lakini na Waziri tulikuwa tumekaa meza pale akasema anashughuli nyagine ambayo anatakiwa aifanye inayohusiana na masuala ya kilimo, lakini akasema angekuwepo humu Bungeni angetamani aseme neno moja tu ahaa amesharudi huyu hapa Waziri wa Kilimo. Aliniambia neno moja analotamani kusema yaani tofauti ya sasa na muda mwininge Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo sasa haijaomba fedha ikakosa na anatarajia kwamba mpaka anamaliza mwaka huenda akawa amepata asilimia 100 ya bajeti huyu hapa yupo amesema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba inawezekana kwa mwaka huu sasa Wizara ya Kilimo ikawa na asilimia 100 ya bajeti tofauti na ilivyokuwa 12, 20, 13, 20. Hiyo ni hatua ya kwanza tumewapatia fedha hata kama ni kidogo zile walizoomba, lakini hatua ya pili tumesema tutatenga fedha kwa ajili ya mbegu. Maana yake Mheshimiwa Waziri amesema *transformation* anayotaka kufanya siyo tu ya kiutawala kwenye Wizara ya Kilimo anataka hasa kwenye sekta yenye. Kwa hiyo la kwanza ni mbegu na sisi tumesema tunavyoanza kutengeneza bajeti hii tuta-*accommodate* bajeti ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu tumeongea na Mheshimiwa Waziri tukasema kwenye umwagiliaji kuna *angle* mbili, *angle* ya kwanza tunaweza tukavuna maji, duniani kwote wanatumia pia umwagiliaji wa kuvuna maji. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu ameshanunua mitambo kwa ajili ya kuchimba mabwawa. Tumeongea na Waziri na ile Idara ya Umwagiliaji wafanye tathmini kwenye mitambo ile ya kuchimba mabwawa je, kwa bwawa la umwagiliaji ni mitambo gani bado inakosekana? Walete tathmini tuiongeze na hiyo, kwa sababu wakulima wetu wengine siyo wakulima wa ma-estate makubwa ni wakulima wa mashamba ya

kawaida ambayo yanaweza wakatengeneza mabwawa ya umwagiliaji wakamwagalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano ya maeneo ambayo watu wameweza kumwagilia na wakaweza kubadilisha maisha yao. Kwa hiyo hili ni jambo lingine ambalo Rais wetu ametuelekeza tukae na wenzetu tufanye tathimini na yale ambayo yatahitajika tutafanya hivyo ili umwagiliaji uweze kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji mwingine ni ule umwagiliaji mkubwa wa kuweka mabomba ya kutoa maji kutoka eneo la mbali kupeleka eneo lingine la umwagiliaji. Haya tumesema taasisi ile ya umwagiliaji wakae na Wizara ya Maji tutakapokuwa tunafanya miradi mingine mikubwa ya maji, tutakapokuwa tunatekeleza miradi mingine mikubwa ya maji labda kutoka Mto Ruvuma kwenda Ruvuma yenewe kwenda mpaka Lindi na Mtwara au kutoka Tanganyika kwenda Katavi, kwenda mpaka Rukwa waangalie teknolojia za kisasa za kutengeneza miundombinu hiyo pawepo na *lane zinazopeleka* maji ya matumizi ya nyumbani, pawepo la *lane zinazopeleka* maji ya umwagiliaji. Tuone kama kuna namna ya *engineering* hiyo ambayo inaweza ikafanyika ambayo inaweza ikawa *cost effective* na ikatusaidia kuweza kutekeleza hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumesema tutayaangalia haya mazao ambayo ni mazao makubwa katika nchi yetu kuna mazao yalishawahi ku- *peak* mpaka *worldwide* yakawa yanajulikana ikafika mahali yakawa yameshukashuka tumesema tutayaangalia, tutaangalia pia *refinancing* yake, mifano imeshapatikana katika maeneo ambapo pembejeo zimeweza kuwa *refinanced* kutoka katika utaratibu wa ndani ya mazao yenewe. Tumesema hayo yote tutayaangalia tuone ni namna gani tunaweza tukaweka utaratibu ambao utatusaidia katika uhakika wa masuala haya ya pembejeo na jambo hili ni jambo ambalo linawezekana na litawezekana kwa mazao yote hayo na tunatambua Bodi hizi zimekuwa na viporo viporo vingi hivyo hivyo na *TFC* yote haya tutakaa na wenzetu tuone ni namna

gani tutafufua haya maeneo ili tuweze kuendelea na yaweze kupiga hatua kubwa zaidi na wakulima wetu na wananchi wetu waweze kupiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayoyasema kwenye upande wa kilimo nimesema ni hivyo hivyo na *sub-sectors* zingine ambazo zinaangukia katika eneo hilo, tutafanya hivyo kwa mifugo, tutafanya hivyo kwa uvuvi kwa sababu ni sekta hizo kubwa ambazo zinabeba eneo kubwa la wananchi wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufanya hii *transformation* kwenye hii sekta ya kilimo tutakuwa na *risk* mbili; *risk* ya kwanza *sustaining* kuendelea kupanda kwenye *rating* hizi za kipato cha kati, kipato cha kati cha chini, kipato cha kati cha juu itakuwa ni ngumu sana kwa sababu watu wenye eneo kubwa ambao wanatakiwa wafanyiwe hiyo tathimini ya kipato kwa mtu mmoja watakuwa bado wapo mbali na utaratibu wa kuweza kupata kipato kikubwa kwenye shughuli ambazo zinawaingizia kipato. Kwa hiyo tunalenga kufanikisha hili ili kipato cha mtu mmoja mmoja kiweze kupanda kwa sababu *population* iliyokubwa ipo eneo hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunalolenga katika eneo hili la kukuza hizi sekta tulizozitaja ni ili tuweze kukipeleka kizazi cha leo katika shughuli za uzalishaji. Kuna Mbunge mmoja alisema hamna utafiti ambao umeshafanyika kwenye hili eneo, niwahakikishie utafiti umeshafanyika majibu tunayo na siku si nydingi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ama Waziri Mkuu mwenyewe atatoa tamko linalohusiana na matokeo ya utafiti wa eneo hilo. Kati ya maeneo ambayo yamekuwa na yanaajiri watu wengi tena ngazi hii ya vijana ni eneo hilo hilo ambalo mmoja wa msemaji alisema halijafanyiwa tathmini nani hilo hilo ambao linahusisha mpaka upande wa kilimo, upande wa vijana wanaojajiri wamachinga na hilo ni eneo ambalo tutaliangalia vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kitu kingine ambacho tunakilenga kwenye upande wa kilimo ni kwa ajili ya ajira, tunataka tupeleke hii *generation* ya kileo iweze kufanya shughuli hizo za kilimo, mifugo pamoja na uvuvi. Tusipo-*transform* hizi sekta hii *generation* ya kisasa haitaweza kufanya hizo shughuli. Katika maeneo mengi ambayo kilimo ama mifugo ama uvuvi unafanywa kwa zile *traditional ways* katika maeneo ambayo kilimo kinafanywa kwa njia ya zamani sana kizazi cha leo hakishiriki kwa asilimia kubwa katika hicho kilimo. Kwa hiyo, inabakia kama ngoma ya kienyeji hivi inafanywa na wazee wa zamani ndiyo wanawenza wakakuimbia ukaona kumbe hii ndiyo ngoma ya kabilia letu. Kwa maana hiyo tuta-*transform* ili tupeleke kizazi cha leo hii shughuli ili tuweze kuwa *World's largest exporter* wa zao fulani tunahitaji na kizazi cha leo kishiriki katika uzalishaji wa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo na kwa upande wa machinga taarifa njema inakuja hii ya utangulizi mmeshaipata na Mheshimiwa Rais anania njema sana kwenye jambo hili na yejote ambaye atalifuatilia kwa umakini na baada ya muda fulani ataona kwamba Mheshimiwa Rais anataka awabadilishe wamachinga kutoka kwenye kutumikishwa wao wenywewe wapate mtaji wawenze kusimama wafanye hizo shughuli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya sasa hivi walichokuwa wanafanya anatembea na bidhaa za watu kwa sababu hatuwezi tukawafikia hata tukitenga hizo asilimia ngapi ngapi hizo hatuwezi kuwafikia. Sasa tukiwa na uwezo wa kuwafikia, mmeona Dar es Salaam wameshaanza, maeneo mengine wameshaanza wanatengeneza *SACCOS* zao tunaamini wakishakuwa katika maeneo ambayo yatafikiwa wataweza kupata fedha kwenye *SACCOS* zao, wataweza kutembea na bidhaa zao, wataweza kuuza bidhaa zao na tunaendelea kuangalia na Waziri wa Ardhi yupo hapa, eneo moja ambalo tutaliangalia kwa umakini na Mheshimiwa Rais ndivyo alivyoelekeza ni kuwaweka katika maeneo ambayo ni *very strategic* ili yule mtu aliyekuwa anaenda kwenye eneo lile ambalo ana-*first target* yake anavyomaliza hiyo *first target*

yake asitake kusafiri kwenda mbali sana kwenda kumtafuta huyo mtu mwingine mwenye bidhaa ndogo aweze kumfikia na yeye hapo hapo, lakini kwenye utaratibu ambao umepangiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivi vitu vingine watu wengine unaweza ukadhania kwamba wao ndiyo wanawahurumia lakini kumbe wao ndiyo hawawahurumii hawa vijana wetu kuna maeneo mengine wanafanya hata katika mazingira sana lazima tuyabadiishe. Mimi nilipita eneo lingine mvua ikija yao, jua likija lao, lakini kama tunaenda tunaendelea tuwabadiishe kuzingatia tu wawe katika eneo ambalo haliathiri wao kufikika kwa wateja wao ambao wanawategemea katika kiwango kikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kutambua michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameisema eneo lingine ambalo lilitajwa kwa kiwango kikubwa lilikuwa la riba ufanuzi wake ni mrefu na niendelee kusema kwamba hayo ni maoni yametolewa sisi tutaendelea kukaa na wataalam wetu kuyafanya kazi, lakini pia tutaendelea kuchukua hatua ambazo zitatupeleka kwenda kufanikisha riba hizo kuwa rafiki ili ziweze kuleta tija. Eneo hili la riba na lenyewe lipo *trick* kidogo, lakini kama ambavyo Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo akiwa Mwanza na ameendelea kutoa maelekezo akiwa ndani ya Serikali tunaamini kwamba tutalifanya kazi na litaweza kuleta tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kazi hii inayofanyika na kule tunakoelekea huu ni mpango ambao tunajadiliana, lakini pia tunajadiliana maeneo ambayo tumeyafanya kazi. Hata hapa tulipotaja tumetaja machache tu, yale yote ninyi mlionyataja yapo na mengine sisi tumeyataja kwa maandishi yote tutaendelea kuyafanya kazi na tutayaweka kwenye utaratibu wa kuyaboresha kwa maana ya kwenye Mpango, lakini pia tutaboresha kwa maana ya utekelezaji wake ili tuweze kuhakikisha kwamba mpango unaofuata unafanya kazi kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda pia kutekeleza miradi mikubwa moja mmetoka kumsikia Waziri wa Nishati, lakini ipo pia miradi mingine mikubwa ambayo tunategemea itaweza kutengeneza *impact* kubwa kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii mikubwa itakavyotekelawa bomba la mafuta, *LNG* pamoja na miradi mingine hii ambayo ni mikubwa na ya kimkakati inayoendelea, yote hii itaendelea ku- *inject* fedha kwenye uchumi wetu na hata hilo alilosema mdogo wangu wananchi wanataka fedha mfukoni, yaani hata hii fedha tu ambayo mkienda huko Majimboni watendaji wetu watawaambia kwamba katika kipindi cha muda mrefu hawajawahi kupokea fedha nyingi hivi kwa wakati kwa mara moja kwenye miradi mingi hivi, mwisho wa siku fedha hizo zitakwenda kwa wananchi, kwa sababu ndiyo watakaojenga madarasa, ndiyo watakaojenga vituo vya afya, hata wale wakandarasi watakaochukua kazi hizo watatengeneza ajira za watu watakao ingia katika kutengeneza iwe darasa, iwe kituo cha afya au iwe madarasa ya shule zile za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni awamu ya kwanza tunaendelea nayo, tuna maliza hii tunaenda majengo mengine hiyo yote ndiyo itakayokuwa njia ya fedha kuendelea kuzipeleka kwa wananchi. Sasa hivi kila Wilaya hawataazimana mafundi yaani kila fundi aliyepo kwenye Wilaya yake atabaki pale pale kwa sababu shughuli zinaendelea kila Kata. Trillioni moja na zaidi inaenda kwenye kila Kata, kila eneo, kila Wilaya ya nchi hii na fedha hizo zitakuwa zinazunguka kwa wananchi mle mle na hayo yote yanaendelea kuchochea fedha ziwepo nyingi kwenye mzunguko kwa sababu hatutoi mkandarasi kutoka nje ya nchi kujenga darasa maana yake atakuwa wa humo humo, maana yake hiyo fedha itakuwepo humu hiyo itaongeza fedha katika mzunguko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in long run* pia tutaendelea kutengeneza ajira za kudumu kwa sababu hatuwezi tukajenga madarasa elfu 15 halafu Walimu wakawa wale

wale, tutaongeza walimu hatuwezi tukajenga vituo vya hivyo vya afya vyote hivyo kila tarafa halafu yakawepo majengo tu, hatuwezi tukashusha *X-Ray* hizi zote kila wilaya *CT scan* kila Mkoa halafu pasiwepo na ajira ya kudumu, ajira za kudumu na zenyewe zinaenda kutengenezwa tutaongeza na wataalamu katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hili jambo siyo la mara moja yaani hii maana ya 'Kazi lendelee' hii siyo jambo la mara moja maana yake linaendelea, watu wengine baada hizi fedha kushuka nyingi hivi walidhani ni bajeti ya miaka mitano, yaani hii hapa ni bajeti inayoenda mpaka mwezi wa sita tu, na mama akasema ule mwaka mwingu unaofuata utakuwa kiboko zaidi na hivi tunavyoongea kuna fedha zingine zipo kwenye *reserve*. Kwa hiyo inayokuja itakuwa kiboko zaidi, sasa wewe chukulia madarasa ya mara hili ongeza ya mwaka kesho unakuja, ongeza vituo vya afya mwaka kesho nenda kwenye barabara hivyo hivyo fedha zinakwenda kwenye ofisi ya *TARURA* katika kiwango hicho, ongeza na mwaka mwingine, ongeza na mwaka mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi tu hapa mlioko hapa Waheshimiwa Wabunge niwaambie neno moja tu hili la kindugu kabisa, msingekuwa wakinamama mngepata kazi sana kwenye kugombea, lakini kwa kuwa ni wakinamama mkifika maeneo hayo mtakuwa mnasema mimi ndiyo Samia wa eneo hili mtapata kura, lakini ukweli wa mambo mtu yejote asijeona kazi anayofanya Mheshimiwa Rais, kwa sababu mlikuwa mnabishabisha atakuwa haitendei haki nafsi yake na atakuwa pia haitendei haki nchi hii. Kazi hii inayofanyika ni kazi ya kihistoria ni kazi ambayo inabadilisha maisha ya wananchi wetu. Kazi ya kihistoria ni kazi inayobadilisha maisha ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tukisharudi Majimboni kazi hii anayofanya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kazi ya kihistoria na nikazi inayokwenda kubadilisha maisha ya Watanzania. Waheshimiwa Wabunge tukisharudi Majimboni kwa sababu

madarasa yatakuwepo yakutosha, madawati zaidi ya laki sita halafu na Walimu tunaenda kuongeza nendeni muwashawishi hata wale ambao walishaacha masomo, wanafunzi wale ambao wengine wanatokea jamii za kifugaji kama zetu, waambieni warudi shulenii elimu yenyewe bila ada, madarasa hamna kubanana kwenye madawati, halafu hamna hata yule ambaye hajaelewaelewa hamna kukaa kwenye mawe maana yake zamani ilikuwa usipo fanyafanya vizuri hesabu wewe ndiyo unakosa nafasi ya kukaa, hii na Walimu tumesema wanaenda sambamba na majengo haya, hatutajenga majengo tu na Walimu katika kipindi hiki kifupi na Walimu wanakwenda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya aina hiyo siyo kazi ya kuibeba na kazi ya aina hiyo hajasimamisha miradi mikubwa na miradi mikubwa na yenyewe inaendelea, miradi mikubwa ya kimkakati inaendelea na kwenye shughuli za uzalishaji kama mpango tuliuso na tumesema tutaunyumbulisha kwa sababu kwa wakati huu tulileta ili tupate maoni tumeshapata, tumepata maoni mengi sana na baada ya hapa tumeyapokea na timu ya wataalam tutaendelea kukaa, lakini pia Kamati yetu na yenyewe itaendelea kuchambua, tutaendelea kupata maoni zaidi tutakapokutana tunaamini tutatengeneza jambo liliilo bora sana ambalo litatusaidia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ninalowaomba twendeni tukamsaidie Mheshimiwa Rais kusimamia fedha hizi kule zilipokwenda. Upande wa wizara tumesema tutaituma Idara yetu ya Ukaguzi wa Ndani ambao wapo kila eneo wasimamie *effectively* na siyo fedha hizi tu na fedha zingine zote ambazo zinahusu maisha ya Watanzania ambazo zinaenda katika miradi mbalimbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini haya yote yatafanyika na yataweza kubadilisha maisha ya Watanzania na Watanzania watafurahia vizuri sana kazi anayofanya Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake anayoiongoza pamoja na ushauri mzuri ambao Waheshimiwa Wabunge wa

Bunge lako Tukufu wanatupatia ili kuweza kuboresha mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimeyasema hayo nakushukuru sana. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Kwa utaratibu wetu hatutoi hoja lakini tumekuelewa Mheshimiwa Waziri. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ufanuzi mzuri kabisa uliopitia mambo mengi, kilichokuwa kinaendelea kinatawaliwa na Kanuni ya 113 inayohusu Mjadala wa Mapendekezo wa Mpango wa Taifa ambao Kanuni ya 113 (5) (c) inasema mjadala unaoendelea utahitimishwa na Serikali kwa kutoa maelezo mafupi kwamba Serikali imepokea maoni na ushauri wa Bunge basi niishie hapo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Katibu!

**NDG. ASIA MINJIA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Mpango imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa jinsi tulivyoenenda vizuri katika majadiliano yetu ambayo Serikali imeshapokea maoni na Ushauri wa Bunge. Tunawataki kila la kheri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu na timu yako yote ya Wizara ya Fedha na Wizara zingine zote katika kwenda kufanya kazi ili tunapokaribia kipindi kile cha bajeti basi matarajio yetu ni kwamba maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge utazingatiwa ili bajeti ya mwakani iwe na utofauti mkubwa sana na tulikotoka kutokana na maoni haya mazuri na mpango mzuri ambao Serikali ilikuwa imetuletea kama sehemu ya mapendekezo.

Tunategemea kwenda kuona kwenye eneo la kilimo kwa kipekee kabisa *impetus* kubwa tujenge mazingira ya uwezekano kuwa na mashamba makubwa katika nchi yetu, hata kama ita-*involve* kupata wakulima kutoka nje kwa maana ya wawekezaji kwenye kilimo ni jambo jema pia ili tujifunze watanzania na sisi kuwa na mashamba makubwa na mengine yote ambayo tumependekeza mabwawa, viwanda nya viuatilifu, viwanda nya mbolea na mambo mengine yote yanayohusiana na maendeleo ya kilimo, viwanda nya kuongeza thamani ya mazao yetu, masoko, kilimo, kilimo, kilimo na kilimo kama alivyosema Waziri wa Fedha ni pamoja na uvuvi na mifugo hata misitu ni kilimo tu, na mengine yanayoendana na hayo. Kwa hiyo, tunawatakieni kila la heri kwa kweli Wizara ya Fedha kwa sababu ninyi ndiyo mnatuwekea msingi kuwa tunaelekea wapi kama nchi, kila heri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kwamba kutakuwa na uzinduzi wa mafunzo ya mwanamke kiongozi kwa Wabunge wanawake hili linatolewa na Katibu wa Bunge anawaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote kuwa mnakaribishiwa kuhudhiria uzinduzi wa mafunzo ya Mwanamke Kiongozi kwa Wabunge yatakayofanyika kesho Jumatano tarehe 10 Novemba katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia Saa Tano Asubuhi. Mafunzo yatakayozinduliwa yataratibiwa na Chama cha Waajiri (*ATE*) na kutolewa kwa Wabunge wanawake wote yakihuisha maeneo ya Uongozi, Utawala na uwezo wa kujenga na kuwasilisha hoja. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria uzinduzi huo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, haya ni mafunzo mazuri kesho ni uzinduzi lakini wakati wa kipindi cha bajeti hasa ndiyo kutakuwa na *session* yenye we ya mafunzo. Kwa hiyo kesho ni uzinduzi, lakini wakati wa kipindi cha bajeti ndiyo yatakuwa mafunzo yenye we hasa yatachukua kama wiki mbili hivi. Mafunzo haya yanalenga wanawake katika masuala ya uongozi, utawala na uwezo wa kujenga na kuwasilisha hoja. Lakini nimewaambia kwamba pamoja na kwamba malengo ni haya yatakapofanyika tutakuwa na *batch* za baadhi ya

Wabunge Wanaume pia. Wao malengo yao ni hayo lakini mimi nimeongezea kutakuwa na Wabunge wanaume pia ambao watashiriki kwenye mafunzo haya. Kwa sababu tukitaka kutoka kwenye mambo haya lazima tuende na *gender* kwa maana ya *gender* tukienda na mambo ya wanawake haya hatuwezi kufika, ndiyo hata wanaume wanahitaji kujifunza uongozi hata wanaume wanahitaji kujifunza utawala, hata wanaume wanahitaji kujifunza uwezo wa kujenga na kuwasilisha hoja na hawa wanaume wanawawakilisha hapa Bungeni na wanawake waliopo huko Majimboni kabisa ndiyo ukweli wenyewe. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo kama *ATE* hawatakuwa na uwezo wa kulipa tutalipa sisi kama Bunge kuwalipia hawa wanaume ili waweze kupata hiyo *knowledge* pia, kwa sababu elimu ni elimu, elimu kama elimu haina *gender*. Kwa hiyo ni jambo jema tunallkaribisha, lakini sasa Wabunge wanawake muwe mbele zaidi na sisi tutawaunga mkono halafu jambo likishakuwa la wote linapendeza, ukishawajaza Wabunge Wanawake watupu kwenye mafunzo wanaanza kuparurana, wanagombana, wanununiana, au siyo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, basi ratiba yetu ni kwamba kesho tutakuwa na taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo halafu kesho kutwa tutakuwa na Muswada huu, Alhamisi na Ijumaa tutakuwa tunafunga shughuli zetu hizi na asubuhi tuna ratiba ratiba, kesho Jumatano, Alhamis kuna semina, Ijumaa kuna semina, Alhamis na Ijumaa kuna semina za Wabunge wote katika Ukumbi wa Msekwa tusikose kuja mapema, kesho Jumatano ni hii niliyoitangaza sasa hivi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Shughuli za Bunge kukamilika sasa naomba nichukue nafasi hii kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho Saa Nane kamili mchana.

*(Saa 12:45 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 10 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana)*